



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2016/17



**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO
JUNI, 2016**

YALIYOMO

| | |
|--|----|
| UTANGULIZI----- | v |
| SURA YA KWANZA----- | 1 |
| HALI YA UCHUMI ----- | 1 |
| 1.1 Uchumi wa Dunia----- | 1 |
| 1.2 Uchumi wa Taifa----- | 3 |
| 1.2.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi----- | 3 |
| 1.2.2 Ukuaji wa Shughuli Mbalimbali za Kiuchumi ----- | 4 |
| 1.2.3 Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa ----- | 5 |
| 1.2.4 Idadi ya Watu na Pato la Kila Mtu----- | 6 |
| 1.2.5 Viashiria vya Umaskini----- | 7 |
| 1.2.6 Nguvu Kazi na Ajira ----- | 8 |
| 1.2.7 Mfumuko wa Bei ----- | 9 |
| 1.2.8 Ukuzaji Rasilimali ----- | 9 |
| 1.2.9 Sekta ya Nje ----- | 10 |
| 1.2.10 Sekta ya Fedha----- | 11 |
| 1.2.11 Deni la Taifa ----- | 13 |
| 1.2.12 Mapato na Matumizi ya Serikali----- | 14 |
| 1.2.13 Matarajio ya Ukuaji wa Uchumi kwa Mwaka 2016/17----- | 15 |
| SURA YA PILI----- | 16 |
| MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO 2015/16----- | 16 |
| 2.1 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2015/16----- | 16 |
| 2.2 Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa----- | 16 |
| 2.3 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati ----- | 18 |
| 2.4 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango ----- | 40 |
| SURA YA TATU----- | 42 |
| HALI YA VIWANDA----- | 42 |
| 3.1 Historia ya Viwanda Nchini----- | 42 |
| 3.2 Mwenendo wa Sekta ya Viwanda ----- | 43 |
| 3.3 Hali ya Viwanda Nchini ----- | 44 |
| 3.4 Ubinafshishaji wa Viwanda ----- | 44 |
| 3.4.1 Utekelezaji wa Mpango wa Ubinafshishaji----- | 44 |
| 3.4.2 Viwanda Vilivyobinafshishwa----- | 45 |
| 3.4.3 Hali ya Viwanda Baada ya Kubinafshishwa ----- | 45 |
| 3.4.4 Changamoto Zilizojitokeza baada ya Ubinafshishaji wa Viwanda----- | 46 |
| 3.5 Mikakati ya Kuendeleza Viwanda Nchini ----- | 47 |
| 3.5.1 Viwanda Vikubwa----- | 47 |
| 3.5.2 Viwanda Vidogo----- | 47 |
| 3.5.3 Viwanda Vilivyobinafshishwa----- | 48 |

| | |
|---|-----|
| SURA YA NNE ----- | 49 |
| VIPAUMBELE VYA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17----- | 49 |
| 4.1 Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda----- | 49 |
| 4.2 Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Rasilimali Watu----- | 51 |
| 4.2.1 Elimu na Mafunzo ya Ufundu----- | 51 |
| 4.2.2 Afya na Ustawi wa Jamii ----- | 55 |
| 4.2.3 Maji Safi na Majitaka----- | 57 |
| 4.2.4 Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ----- | 59 |
| 4.2.5 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ----- | 60 |
| 4.2.6 Wanyamapori----- | 60 |
| 4.2.7 Misitu----- | 62 |
| 4.2.8 Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi----- | 62 |
| 4.2.9 Ardhi, Nyumba na Makazi----- | 63 |
| 4.3 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji ----- | 63 |
| 4.3.1 Nishati ----- | 63 |
| 4.3.2 Kilimo ----- | 70 |
| 4.3.3 Miundombinu----- | 75 |
| 4.3.4 Huduma za Fedha, Utalii, Biashara na Masoko ----- | 92 |
| 4.4 Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango ----- | 95 |
| 4.5 Miradi Mikubwa ya Kielelezo ----- | 95 |
| 4.6 Maeneo Mengine Muhimu kwa ukuaji wa Uchumi na Ustawi wa Taifa ----- | 99 |
| 4.6.1 Madini----- | 99 |
| 4.6.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ----- | 100 |
| 4.6.3 Utawala Bora ----- | 101 |
| 4.6.4 Utoaji haki na Huduma za Sheria----- | 101 |
| 4.7 Mikakati ya Ushiriki wa Sekta Binafsi----- | 102 |
| SURA YA TANO ----- | 103 |
| UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17 ----- | 103 |
| 5.1 Ugharamiaji wa Miradi ----- | 103 |
| 5.2 Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2011/12 – 2015/16----- | 103 |
| 5.3 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2016/17 ----- | 104 |
| 5.4 Vyanzo vya Mapato ya Ndani----- | 104 |
| 5.5 Vyanzo vya Mapato ya Nje----- | 104 |
| 5.6 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ----- | 105 |
| 5.7 Uwekezaji wa Sekta Binafsi ----- | 105 |
| 5.8 Mikopo Nafuu kutoka Taasisi za Fedha Nchini ----- | 105 |
| SURA YA SITA----- | 106 |
| UFUAMILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA----- | 106 |

| | | |
|-------|--|-----|
| 6.1 | Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini----- | 106 |
| 6.2 | Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo ----- | 106 |
| 6.2.1 | Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa ----- | 106 |
| 6.2.2 | Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati----- | 106 |
| 6.2.3 | Yaliyojitokeza katika ufuatiliaji wa miradi----- | 114 |
| 6.3 | Mgawanyo wa Majukumu ----- | 115 |
| | SURA YA SABA ----- | 117 |
| | VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO ----- | 117 |
| 7.1 | Vihatarishi katika kutekeleza Mpango----- | 117 |
| 7.2 | Mikakati ya Kukabiliana na Vihatarishi ----- | 118 |
| | KIAMBATISHO I:IDADI NA AINA YA VIWANDA NCHINI, 2015 ----- | 120 |
| | KIAMBATISHO II:IDADI YA VIWANDA VIDOGO NA VIKUBWA KIMKO, 2015----- | 122 |
| | KIAMBATISHO III:IDADI YA VIWANDA NA AJIRA KIMKO, 2015----- | 123 |
| | KIAMBATISHO IV:VIWANDA VIKUBWA (AJIRA ZAIDI YA 500) ----- | 124 |
| | KIAMBATISHO V:MIRADI YA KIPAUMBELE 2016/17----- | 127 |
| | KIAMBATISHO VI:RATIBA YA UTEKELEZAJI NA UANDAAJIWA MPANGO ----- | 188 |

UTANGULIZI

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 unalenga kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21). Mpango unakusudiwa kuwa na maeneo manne ya vipaumbele:- viwanda vya kuimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi; miradi mikubwa ya kielelezo; miradi wezeshi kwa maendeleo ya viwanda ikiwemo barabara, reli, nishati, bandari, maji na mawasiliano; na maeneo yatakayolenga kufungamanisha maendeleo ya viwanda na watu. Mpango huu unalenga kuhakikisha kuwa rasilimali na fursa za nchi zinatumika vizuri ili kujenga uchumi wa viwanda na kupunguza umaskini. Ili kufikia malengo hayo, mikakati itakayotumika ni pamoja na: kuanza na viwanda vilivyopo, hususan, viwanda vilivyobinafsishwa kwa wawekezaji binafsi kwa makubaliano ya kuviendeleza; kuhimiza na kushawishi wawekezaji kuwekeza katika maeneo mbalimbali nchini; na kuondoa vikwazo kwa kuimarisha mazingira ya kufanya biashara.

Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 yamezingatia: dhamira ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ya kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati; Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 – 2025/26); maamuzi ya Serikali ya kuunganisha mfumo wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania Awamu ya Pili (MKUKUTA II) katika mfumo mmoja jumuishi; na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Pia, yamezingatia sera na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kisekta, kikanda (EAC na SADC) na Umoja wa Afrika; Malengo ya Maendeleo Endelevu, 2030; Ilani ya CCM ya uchaguzi wa mwaka 2015; na hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wakati akifungua rasmi Bunge la 11 yenye msisitizo wa ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 kimegawanyika katika sura kuu saba. Sura ya kwanza ni hali ya uchumi wa Dunia na Taifa. Sura ya pili ni mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2015/16. Sura ya tatu ni Hali ya viwanda nchini. Sura ya nne ni maeneo ya vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Sura ya tano ni ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Sura ya sita inaanisha ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa ya miradi ya maendeleo. Sura ya saba ni mkakati wa kukabiliana na vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango.

SURA YA KWANZA

HALI YA UCHUMI

1.1 **Uchumi wa Dunia**

Katika mwaka 2015, kasi ya ukuaji wa uchumi wa Dunia ilipungua ikilinganishwa na ukuaji katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Ukuaji wa Pato la Dunia ulikuwa asilimia 3.1 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2014. Hata hivyo, mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi unatofautiana kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea. Katika mwaka 2015, ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea ulikuwa asilimia 1.9 ikilinganishwa na asilimia 1.8 mwaka 2014. Hali hiyo ilichangiwa na kuimarika kwa uchumi wa Marekani, Ulaya na Japan. Ongezeko hilo lilitokana na uwepo wa bei za chini za nishati, kuimarika kwa soko la nyumba na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha.

Kwa upande wa nchi zinazoibukia na zinazoendelea, kasi ya ukuaji wa uchumi ilikuwa asilimia 4.0 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.6 mwaka 2014. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwa nchi za China, Urusi, Brazil na Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kufuatia kuperomoka kwa bei za bidhaa/mazao katika soko la Dunia pamoja na masharti magumu ya upatikanaji wa mikopo. Aidha, kasi ya ukuaji wa pato la Nchi za Asia Zinazoendelea ikijumuisha China na India ilipungua na kuwa asilimia 6.6 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2014. Uchumi wa nchi zinazozalisha na kuuza nje mafuta ya petroli nao ulidorora kufuatia kuperomoka kwa bei ya mafuta katika soko la Dunia. Uchumi wa nchi hizo ulikua kwa asilimia 0.1 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.4 mwaka 2014.

Kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji ulipungua kutoka asilimia 5.1 mwaka 2014 hadi asilimia 3.4 mwaka 2015. Kupungua kwa kasi ya ongezeko la pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kulitokana na hali ya kibiashara duniani ambapo nchi zinazouza bidhaa nje ziliathiriwa kutokana na kuperomoka kwa mapato kulikochangiwa na kupungua bei katika soko la dunia. Vile vile, kuna baadhi ya nchi zilikabiliwa na vikwazo vya kupata mikopo kutoka masoko ya kimataifa na hivyo kushindwa kutekeleza miradi iliyopangwa katika kipindi hicho. Aidha, zipo baadhi ya nchi ambazo uchumi wao ulianguka kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kisiasa (Burundi), vita (Sudan ya Kusini),

kuporomoka kwa bei ya dhahabu (Botswana), kuporomoka kwa bei ya mafuta ya petroli (Equatoria Guinea) na kuibuka kwa ugonjwa wa ebola (Siera Leone). **Jedwali Na. 1.1** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa Pato la Dunia kuanzia mwaka 2008 hadi 2015 na matarajio ya mwaka 2016 na 2017.

Jedwali 1.1: Ukuaji wa Pato la Dunia (2008-2015) na Matarajio (2016 – 2017)

| | Halisi (Asilimia) | | | | | | | | Matarajio (Asilimia) | |
|-------------------------------------|-------------------|------|------|------|------|------|------|------|----------------------|------|
| | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
| Dunia | 3.1 | 0.0 | 5.4 | 4.2 | 3.4 | 3.3 | 3.4 | 3.1 | 3.2 | 3.5 |
| Nchi Zilizoendelea | 0.2 | -3.4 | 3.1 | 1.7 | 1.2 | 1.1 | 1.8 | 1.9 | 1.9 | 2.0 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | 5.8 | 3.1 | 7.4 | 6.2 | 5.2 | 5.0 | 4.6 | 4.0 | 4.1 | 4.6 |
| Nchi Zinazoibukia Barani Asia | 7.3 | 7.5 | 9.6 | 7.7 | 6.8 | 7.0 | 6.8 | 6.6 | 6.4 | 6.3 |
| Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara | 6.0 | 4.0 | 6.7 | 5.0 | 4.2 | 5.2 | 5.1 | 3.4 | 3.0 | 4.0 |
| Tanzania | 5.6 | 5.4 | 6.4 | 7.9 | 5.1 | 7.3 | 7.0 | 7.0 | 7.2 | 7.1 |
| Kenya | 0.2 | 3.3 | 8.4 | 6.1 | 4.5 | 5.7 | 5.3 | 5.6 | 6.0 | 6.1 |
| Uganda | 10.4 | 8.1 | 7.7 | 6.8 | 2.6 | 3.9 | 4.9 | 5.0 | 5.3 | 57 |
| Rwanda | 11.2 | 6.2 | 6.3 | 7.5 | 8.8 | 4.7 | 7.0 | 6.9 | 6.3 | 6.7 |
| Burundi | 4.9 | 3.8 | 5.1 | 4.2 | 4.0 | 4.5 | 4.7 | -4.1 | 3.4 | 3.9 |

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa, Aprili, 2016

Katika mwaka 2015, mwenendo wa mfumuko wa bei ya mtumiaji wa mwisho Duniani uliendelea kupungua kutokana na kushuka kwa bei ya mafuta, kupungua kwa bei za bidhaa na kudhoofika kwa mahitaji ya bidhaa. Mfumuko wa bei ya mtumiaji wa mwisho duniani ulipungua na kuwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2014. Aidha, kasi ya ongezeko la bei kwa nchi zilizoendelea ilipungua kutoka wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2014 hadi wastani wa asilimia 0.3 mwaka 2015. Hata hivyo, kasi ya mfumuko wa bei ya mtumiaji wa mwisho kwa kundi la nchi zinazoendelea iliendelea kubaki katika wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2015 kama ilivyokuwa mwaka 2014.

Kasi ya ongezeko la bei ya mtumiaji wa mwisho kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara iliongezeka kwa wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.4 mwaka 2014. Hali hii kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na mwenendo wa bei kwa nchi zinazouza mafuta nje na kwa nchi za kipato cha chini. Aidha, nchi za kipato cha kati za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara zilionesha kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei ya mtumiaji wa mwisho. Mfumuko wa bei kwa makundi ya nchi zinazouza mafuta nje na nchi za kipato cha chini za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa wa wastani wa asilimia 8.7 na asilimia 5.9 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa bei wa asilimia 7.1 na asilimia 4.7 mwaka

2014, kwa mtiririko huo. Kwa kundi la nchi za kipato cha kati, kasi ya mfumuko wa bei ya mtumiaji wa mwisho ilipungua kutoka wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2014 hadi wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2015.

Katika nchi za Afrika Mashariki mfumuko wa bei uliendelea kuwa katika kiwango cha tarakimu moja katika mwaka 2015 ambapo wastani wa mfumuko wa bei kwa nchi ya Rwanda ulikuwa asilimia 2.1, Uganda (asilimia 5.2), Tanzania (asilimia 5.6), Kenya (asilimia 6.6) na Burundi (asilimia 7.4). **Jedwali Na. 1.2** linaonesha mwenendo wa mfumuko wa bei wa Dunia kwa mwaka 2014 hadi 2015.

Jedwali Na. 1.2: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei wa Dunia Mwaka 2014 hadi 2015

| | Halisi (Asilimia) | |
|-------------------------------------|-------------------|------|
| | 2014 | 2015 |
| Dunia | 3.5 | 3.3 |
| Nchi Zilizoendelea | 1.4 | 0.3 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | 4.7 | 4.7 |
| Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara | 6.4 | 7.0 |
| Tanzania | 6.1 | 5.6 |
| Kenya | 6.9 | 6.6 |
| Uganda | 4.6 | 5.8 |
| Rwanda | 1.8 | 2.5 |
| Burundi | | 7.4 |

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa, Aprili, 2016

1.2 Uchumi wa Taifa

1.2.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Katika mwaka 2015, Pato Halisi la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 44.1 ikilinganishwa na shilingi trilioni 41.2 mwaka 2014, sawa na ukuaji wa asilimia 7.0. Ukuaji huu umeiwezesha Tanzania kuendelea kuwa na kiwango cha juu cha ukuaji kwa nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka 2014 na 2015. Ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi katika mwaka 2015 unaonesha kuwa sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na: Ujenzi (asilimia 16.8); Mawasiliano (asilimia 12.1); na Huduma za Fedha na Bima (asilimia 11.8). Katika kipindi husika shughuli za usambazaji maji na udhibiti maji taka na upangishaji nyumba zilikuwa na ukuaji mdogo wa asilimia 0.1 na asilimia 2.2 kwa mtiririko huo. Aidha, kilimo ambacho kinaajiri zaidi ya asilimia 70 ya watu wote nchini kiliendelea kukua kwa kasi ndogo ya asilimia 2.3 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2014. Sekta hii ndiyo ilikuwa na mchango mkubwa wa asilimia 29.0 katika Pato la Taifa mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 28.9 mwaka 2014. Sekta zilizofuatia kwa kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa ni pamoja na ujenzi

(asilimia 13.6); biashara na matengenezo (10.7); ulinzi na utawala (asilimia 6.4).

1.2.2 Ukuaji wa Shughuli Mbalimbali za Kiuchumi

Katika mwaka 2015, shughuli za **kilimo** (mazao, ufügaji, misitu na uvuvi) ilikua kwa asilimia 2.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2014. Shughuli ndogo ya **kilimo cha mazao** ilikua kwa asilimia 2.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.0 mwaka 2014. Hii ilitokana na upungufu wa mvua za masika katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji wa mazao ya kilimo katika msimu wa kilimo wa mwaka 2014/15 na mvua za vuli katika msimu wa mwaka 2015/16. Shughuli ndogo ya **mifugo** ilikua kwa asilimia 2.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.2 mwaka 2014 kutokana na utekelezaji wa sera za usimamizi wa sekta ya mifugo na upatikanaji wa takwimu sahihi za sekta ya mifugo hususan kwenye machinjio. Shughuli ndogo ya **misitu** ilikua kwa wastani wa asilimia 2.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2014 kutokana na kutekelezwa kwa sera za uvunaji wa mazao ya misitu kwa uendelevu. Shughuli ndogo ya **uvuvi** ilikua kwa asilimia 2.5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.0 mwaka 2014 kutokana na kuongezeka kwa samaki waliovunwa katika uvuvi wa bahari kuu na uvunaji katika maziwa, mito na mabwawa.

Katika mwaka 2015, shughuli za **viwanda na ujenzi** zilikua kwa kiwango cha asilimia 11.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 10.3 mwaka 2014. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za makazi, biashara na ujenzi wa miundombinu uliokuwa ukiendelea.

Katika mwaka 2015, shughuli za utoaji **huduma** (ikijumuisha biashara na matengenezo, usafirishaji na uhifadhi mizigo, malazi, habari na mawasiliano, fedha na bima, upangishaji majumba, elimu na afya) zilikua kwa kiwango cha asilimia 6.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.2 mwaka 2014. Hii ilitokana na kupungua kwa shughuli mbalimbali za utoaji huduma katika jamii zikiwemo biashara na matengenezo, usafirishaji na uhifadhi mizigo. **Jedwali Na. 1.3** linaonesha ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi mwaka 2015.

Jedwali Na. 1.3: Ukuaji wa Shughuli Mbalimbali za Kiuchumi (2010 hadi 2015)

| Shughuli za Kiuchumi | Ukuaji (Asilimia) | | | | | |
|---|-------------------|------------|------------|------------|------------|------------|
| | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 |
| Kilimo, Misitu na Uvubi | 2.7 | 3.5 | 3.2 | 3.2 | 3.4 | 2.3 |
| • Mazao | 3.7 | 4.8 | 4.2 | 3.5 | 4.0 | 2.2 |
| • Mifugo | 1.4 | 1.6 | 1.8 | 2.0 | 2.2 | 2.4 |
| • Misitu | 3.4 | 3.3 | 3.5 | 4.7 | 5.1 | 2.6 |
| • Uvubi | 0.9 | 2.6 | 2.9 | 5.5 | 2.0 | 2.5 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 7.3 | 6.3 | 6.7 | 3.9 | 9.4 | 9.1 |
| Viwanda | 8.9 | 6.9 | 4.1 | 6.5 | 6.8 | 6.5 |
| Umeme | 13.4 | -4.3 | 3.3 | 13.0 | 9.3 | 5.8 |
| Usambazaji Maji Safi na Udhibiti Maji taka | 2.2 | -1.2 | 2.8 | 2.7 | 3.7 | 0.1 |
| Ujenzi | 10.3 | 22.9 | 3.2 | 14.6 | 14.1 | 16.8 |
| Biashara na Matengenezo | 10.0 | 11.3 | 3.8 | 4.5 | 10.0 | 7.8 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 10.7 | 4.4 | 4.2 | 12.2 | 12.5 | 7.9 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 3.7 | 4.1 | 6.7 | 2.8 | 2.2 | 2.3 |
| Habari na Mawasiliano | 24.4 | 8.6 | 22.2 | 13.3 | 8.0 | 12.1 |
| Shughuli za Fedha na Bima | 12.6 | 14.8 | 5.1 | 6.2 | 10.8 | 11.8 |
| Upangishaji Nyumba | 1.8 | 1.9 | 2.0 | 2.1 | 2.2 | 2.2 |
| Sughuli za kitaaluma, Kisayansi na Kiufundi | 29.9 | 4.8 | -5.8 | 5.4 | 0.5 | 6.8 |
| Utarawala na Ulinzi | -5.0 | 15.9 | 9.1 | 7.8 | 3.9 | 4.6 |
| Elimu | 6.4 | 5.6 | 7.4 | 4.3 | 4.8 | 6.3 |
| Afya na Ustawi wa Jamii | 3.3 | 5.3 | 11.4 | 8.8 | 8.1 | 4.7 |
| Sanaa na Burudani | 7.3 | 7.7 | 11.0 | 5.7 | 5.7 | 6.2 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 6.0 | 6.2 | 6.4 | 6.5 | 6.7 | 6.9 |
| Shughuli za Kaya binafsi katika kuajiri | 2.7 | 2.7 | 2.7 | 2.7 | 2.7 | 2.7 |
| Pato la Taifa kwa bei za soko | 6.4 | 7.9 | 5.1 | 7.3 | 7.0 | 7.0 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2016

1.2.3 Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa

Katika mwaka 2015, mchango wa shughuli za **kilimo** ambao hujumuisha mazao, ufgajji, misitu na uvubi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 29.0 ikilinganishwa na asilimia 28.9 mwaka 2014. Shughuli ndogo ya **kilimo cha mazao** ilichangia asilimia 15.6 ikilinganishwa na asilimia 16.1 mwaka 2014; **mifugo** asilimia 7.9 ikilinganishwa na asilimia 7.3 mwaka 2014; **misitu** asilimia 3.5 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 3.1 mwaka 2014; na **uvubi** ilikuwa na mchango wa asilimia 2.1 ikilinganishwa na asilimia 2.2 mwaka 2014.

Katika mwaka 2015, shughuli za **viwanda na ujenzi** ziliikuwa na mchango wa asilimia 24.3 katika Pato la Taifa kutoka asilimia 23.2 mwaka 2014. Vile vile, shughuli za utoaji **huduma** (ikijumuisha biasara na matengenezo, usafirishaji na uhifadhi mizigo, malazi, habari na mawasiliano, fedha na bima, upangishaji majumba, elimu na afya) ziliikuwa na mchango wa asilimia 40.0 ikilinganishwa na asilimia 40.9 mwaka 2014. **Jedwali Na. 1.4** linaonesha mchango wa shughuli mbalimbali za kiuchumi katika Pato la Taifa kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi mwaka 2015.

Jedwali Na. 1.4: Mchango wa Shughuli Mbalimbali za Kiuchumi katika Pato la Taifa (2010 hadi 2015)

| Shughuli za Kiuchumi | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 |
|---|--------------|--------------|--------------|--------------|--------------|--------------|
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 29.9 | 29.4 | 31.1 | 31.2 | 28.8 | 29.0 |
| Mazao | 16.6 | 16.5 | 18.0 | 17.5 | 16.1 | 15.6 |
| Mifugo | 9.1 | 8.7 | 8.5 | 8.2 | 7.3 | 7.9 |
| Misitu | 2.2 | 2.2 | 2.5 | 3.1 | 3.1 | 3.5 |
| Uvuvi | 2.1 | 2.1 | 2.2 | 2.4 | 2.2 | 2.1 |
| Viwanda na Ujenzi | 20.3 | 22.8 | 21.8 | 22.7 | 23.2 | 24.3 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 4.1 | 5.1 | 4.9 | 4.2 | 3.7 | 4.0 |
| Viwanda | 6.9 | 7.6 | 7.5 | 6.4 | 5.6 | 5.2 |
| Umeme | 0.9 | 0.6 | 0.9 | 0.8 | 1.1 | 1.0 |
| Usambazaji Maji Safi na Udhibiti Maji taka | 0.6 | 0.5 | 0.4 | 0.5 | 0.5 | 0.4 |
| Ujenzi | 7.8 | 9.0 | 8.1 | 10.8 | 12.4 | 13.6 |
| Huduma | 44.2 | 42.7 | 41.9 | 41.0 | 40.9 | 40.0 |
| Biashara na Matengenezo | 10.1 | 10.6 | 10.4 | 10.2 | 10.5 | 10.7 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 5.8 | 5.2 | 4.4 | 4.2 | 4.3 | 4.3 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1.6 | 1.4 | 1.4 | 1.3 | 1.1 | 1.1 |
| Habari na Mawasiliano | 2.6 | 2.4 | 2.4 | 2.3 | 2.1 | 2.0 |
| Shughuli za Fedha na Bima | 3.2 | 3.4 | 3.4 | 3.3 | 3.4 | 3.6 |
| Upangishaji Nyumba | 4.6 | 4.3 | 4.3 | 3.8 | 3.7 | 3.2 |
| Sughuli za kitaaluma, Kisayansi na Kiufundi | 1.7 | 1.5 | 1.3 | 1.3 | 1.3 | 1.2 |
| Shughuli nyingine za Kiutawala na Huduma | 2.2 | 2.1 | 2.3 | 2.4 | 2.5 | 2.4 |
| Utarawala na Ulinzi | 6.1 | 6.3 | 6.5 | 7.0 | 6.6 | 6.4 |
| Elimu | 3.1 | 2.8 | 2.6 | 2.7 | 2.7 | 2.5 |
| Afya na Ustawi wa Jamii | 1.7 | 1.6 | 1.5 | 1.4 | 1.4 | 1.4 |
| Sanaa na Burudani | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 |
| Shughuli za Kaya binafsi katika kuajiri | 0.3 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2016

1.2.4 Idadi ya Watu na Pato la Kila Mtu

Katika mwaka 2015, Tanzania ilikadiriwa kuwa na idadi ya watu 47,351,275 na Pato la Taifa lilikuwa shilingi milioni 90,863,681 mwaka 2015 ikilinganishwa na shilingi milioni 79,718,416 mwaka 2014 kwa bei za mwaka husika. Aidha, wastani wa Pato la kila mtu lilikuwa shilingi 1,918,928 mwaka 2015 ikilinganishwa na shilingi 1,730,405 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Hata hivyo, Pato la wastani kwa kila mtu katika Dola za Kimarekani lilipungua kutoka Dola 1,047 mwaka 2014 hadi Dola 966.5 mwaka 2015 kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Hivyo, ni dhahiri kuwa bado kunahitajika msukumo zaidi wa kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa ili kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya kufikia Dola za Kimarekani 3,000 kwa Pato la kila mtu na kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

1.2.5 Viashiria vya Umaskini

Katika mwaka 2015/16, Serikali iliendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa MKUKUTA-II ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mkakati huo ambao baada ya kuongezewa muda wa mwaka mmoja wa utekelezaji, unafikia ukomo wake mwezi Juni 2016. Matokeo ya tathmini hiyo yameainisha mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa MKUKUTA-II ni pamoja na kukua kwa Pato la wastani la kila mtu kutoka Shilingi 770,464.3 mwaka 2010 kufikia shilingi 1,918,928 mwaka 2015; kuongezeka kwa kasi ya kupungua kwa umaskini wa kipato ambapo kati ya mwaka 2007 na 2012 umaskini ulipungua kwa asilimia 6.2, kutoka 34.4 hadi 28.2 na inakisiwa kupungua zaidi hadi asilimia 24.5 mwaka 2015 na matarajio ni kufikia asilimia 16.7 mwaka 2020.

Tafiti za mapato na matumizi katika kaya, zinaonesha kuwa kiwango cha umaskini mijini na vijijini kimepungua, kuashiria kuwa kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi ya wastani wa asilimia 6.5 iliyofikiwa katika kipindi cha muongo mmoja na nusu uliopita, imeanza kuzaa matunda. Tathmini ya hali ya umaskini kimaeneo iliyofanyika kwa kutumia takwimu za Sensa ya Watu ya mwaka 2012 na Utafiti wa Hali ya Kipato na Matumizi katika Kaya Binafsi mwaka 2012 inaonesha matokeo chanya na kutofautiana kimkoa na kiwilaya. Mikoa 5 ya mwanzo inayoonesha kufanya vizuri ni Dar es Salaam (5.2), Kilimanjaro (14.3), Arusha (14.7), Pwani (14.7), na Manyara (18.3). Mikoa 5 ya mwisho ni Kigoma (48.9), Geita (43.7), Kagera (39.3), Singida (38.2), na Mwanza (35.3). Kiwilaya umaskini mkubwa upo katika wilaya ya Kakonko (Kigoma) na Biharamulo (Kagera) ambapo takriban asilimia 60 ya watu wapo chini ya mstari wa maskini. Hii ina maana kuwa maeneo ya vijijini hususan pembezoni bado watanzania wengi wanaishi kwenye umaskini, uwezo wao wa kupata mahitaji ya msingi ni mdogo sana.

Mwenendo wa viashiria vya umaskini usio wa kipato vimeonesha matokeo ya kuridhisha katika kipindi cha kuanzia mwaka 1991/92 hadi 2011/12. Hali hii imetokana na juhudzi za Serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii kama vile miundombinu ya usafirishaji, afya, elimu na maji mijini na vijijini. Hali hii inadhihirishwa na kuimarika kwa ubora wa nyumba za makazi, vyombo vya usafiri, zana na nyenzo za kilimo, na umiliki wa simu za mkononi katika kaya. **Jedwali Na. 1.5** linaonesha mwenendo wa viashiria mbalimbali vya umaskini usio wa kipato kuanzia mwaka 1991/92 hadi mwaka 2011/12.

Jedwali Na. 1.5: Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini Usio wa Kipato (1991/92 - 2011/12)

| Kiashiria | 1991/92 | 2000/01 | 2007 | 2011/12 |
|---|---------|---------|------|---------|
| Asilimia ya kaya zeny paa la kisasa | 36 | 43 | 55 | 68 |
| Asilimia ya kaya zeny kuta za kisasa | 16 | 25 | 35 | 46 |
| Asilimia ya kaya zeny umeme | 9 | 12 | 13 | 18 |
| Asilimia ya kaya zinazomiliki vyombo vya usafiri (pikipiki) | 0.7 | 0.9 | 1.5 | 4 |
| Asilimia ya kaya zinazotumia vyanzo salama vya maji msimu wa kiangazi | 46 | 55 | 52 | 61 |
| Wastani wa ekari za ardhi zinazomiliiki na kaya maeneo ya vijijini | | 6 | 5 | 7 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2014

1.2.6 Nguvu Kazi na Ajira


Katika mwaka 2015, Serikali ilizindua taarifa ya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi kwa mwaka 2014. Katika utafiti huo ilibainika kuwa nguvukazi ya Taifa ilikuwa watu 25,750,116, sawa na asilimia 57 ya watu wote Tanzania Bara. Kati ya hao, wanawake walikuwa 13,390,678 (sawa na asilimia 52) na wanaume walikuwa 12,359,438 (sawa na asilimia 48). Vile vile, utafiti huo ulionesha kuwa, kati ya nguvukazi iliyokuwepo, watu wenye uwezo wa kufanya kazi walikuwa 22,321,924 na watu 3,428,192 walikuwa hawana uwezo wa kufanya kazi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ulemavu na ugonjwa wa muda mrefu. Kati ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi, walioajiriwa walikuwa 20,030,139 na wasioajiriwa walikuwa 2,291,785. Kati ya walioajiriwa, wanawake walikuwa 9,886,739 (sawa na asilimia 49.4) na wanaume walikuwa 10,143,400 (sawa na asilimia 50.6). Watu wenye ajira jijini Dar es Salaam walikuwa 1,927,367 sawa na asilimia 9.6, na katika maeneo mengine ya mijini walikuwa 5,131,422, (sawa na asilimia 25.6) na maeneo ya vijijini walikuwa 12,971,350, (sawa na asilimia 64.8). Kutokana na utafiti huo, ilibainika kuwa idadi kubwa ya kundi la watu walioajiriwa lilikuwa na umri kati ya miaka 35 hadi 64 (asilimia 42.5).

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo, asilimia 77.8 ya nguvu kazi yote ya Taifa walikuwa katika ajira. Uwiano huu wa ajira na nguvu kazi unapima uwezo wa nchi kutoa ajira. Uwiano ulikuwa mkubwa maeneo ya vijijini (asimilia 82.2), wakati jiji la Dar es Salaam lilikuwa na uwiano mdogo zaidi (asilimia 59.8). Katika utafiti huo, ilibainika kuwa wanaume walikuwa na uwiano mkubwa (asilimia 82.1) ukilinganisha na wanawake (asilimia 73.8). Vile vile, uwiano ulikuwa mkubwa kwa kundi la watu wenye umri wa miaka 35-64 (asilimia 87.2) na mdogo zaidi kwenye kundi la miaka 65 na zaidi (asilimia 56.4).

1.2.7 Mfumuko wa Bei

Wastani wa mfumuko wa bei kwa mwaka 2015 ulikuwa asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2014. Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiwango kikubwa na kushuka kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia na la ndani na utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti na za fedha. Aidha, mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 4.0 Januari 2015 hadi asilimia 6.4 Julai 2015 na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 6.8 Desemba 2015. Hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la fahirisi ya bei ya chakula iliyoongezeka kwa asilimia 8.6 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2014. Mfumuko wa bei ulishuka kufikia asilimia 5.4 Machi 2016. Matarajio ni kubaki na mfumuko wa bei katika kiwango cha tarakimu moja kwa kuongeza uzalishaji hususan wa chakula na kuimarisha sera za kifedha na bajeti. **Kielelezo Na. 1.1** kinaonesha mwenendo wa mfumuko wa bei kwa kipindi cha Januari 2015 hadi Machi 2016 ambapo kiwango cha chini kilikuwa asilimia 4.0 Januari 2015 na kiwango cha juu kilikuwa asilimia 6.8 Desemba 2015.

Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Januari 2015 – Machi 2016)



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2016

1.2.8 Ukuzaji Rasilimali

Katika mwaka 2015, ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 5.4 kufikia shilingi milioni 25,328,568 kutoka shilingi milioni 24,019,720 mwaka 2014. Hata hivyo, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2007 ulipungua kwa asilimia 1.0 kufikia shilingi milioni 13,996,865 mwaka 2015 kutoka shilingi milioni 14,140,777 mwaka 2014. Uwiano wa ukuzaji

rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulikuwa asilimia 27.9 ikilinganishwa na asilimia 30.2 mwaka 2014. Uwiano wa ukuzaji rasilimali wa sekta binafsi katika rasilimali za kudumu ulikuwa asilimia 77.4 mwaka 2015.

1.2.9 Sekta ya Nje

Mauzo ya Bidhaa na Huduma

Katika mwaka 2015, thamani ya **mauzo ya bidhaa na huduma** nje ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 9,450.0 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 8,717.4 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia hususan bidhaa za viwandani. Mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa za viwandani yaliongezeka kwa asilimia 10.1 na kufikia thamani ya Dola za Marekani milioni 1,364.5 kutoka Dola za Marekani milioni 1,239.6 mwaka 2014. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani nchi za nje hususan mazao ya katani na nyuzi za pamba. Kwa upande mwagine, thamani ya **uagizaji wa bidhaa na huduma** kutoka nje ilipungua kwa asilimia 7.8 kutoka Dola za Kimarekani milioni 13,586.5 mwaka 2014 hadi Dola za Kimarekani milioni 12,528.2 mwaka 2015. Mwenendo huu ulichangia kuimarika kwa urari wa malipo ya kawaida.

Mwenendo wa Utalii

Kwa upande wa **utalii**, katika mwaka 2015 idadi ya watalii walitembelea nchini ilipungua kwa asilimia 8.0 kufikia watalii 1,048,944 kutoka watalii 1,140,156 mwaka 2014. Kupungua kwa idadi ya watalii kulitokana na taarifa za ugonjwa wa Ebola, matukio ya ugaidi na hofu ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Vile vile, mapato yatokanayo na watalii hao yalipungua kwa asilimia 5.0 kutoka Dola za Kimarekani bilioni 2.0 mwaka 2014 hadi Dola za Kimarekani bilioni 1.9 mwaka 2015. Serikali iliendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kushiriki maonesho matano ya utalii katika nchi za Ujeruman (ITB-Berlin), Afrika Kusini (INDABA), China (COTTM), Kenya (Magical Kenya) na Uingereza (WTM).

Uwekezaji Vitega Uchumi Nchini

Katika mwaka 2015, Kituo cha Taifa cha Uwekezaji kilisajili jumla ya miradi 466 ikilinganishwa na miradi 704 iliyosajiliwa mwaka 2014. Miradi iliyosajiliwa ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani bilioni 5.89 ikilinganishwa na Dola bilioni 11.9 mwaka 2014, sawa na upungufu wa asilimia 50.5. Usajili wa miradi ulikuwa na fursa za ajira 46,250 ikilinganishwa na fursa za ajira 68,442 mwaka 2014, sawa na upungufu wa

asilimia 32.4. Upungufu huu ulitokana na marekebisho yaliyofanywa katika sheria ya kodi ya ongezeko la thamani ambayo ilipunguza misamaha ya kodi isiyo na tija. Aidha, Katika miradi iliyosajiliwa mwaka 2015, miradi 203 ilikuwa ya wazawa, 171 ya wageni na 92 ya ubia kati ya wazawa na wageni ikilinganishwa na miradi 323 ya wazawa, 203 ya wageni na miradi 168 ya ubia iliyosajiliwa mwaka 2014.

Akiba ya Fedha za Kigeni

Katika kipindi kilichoishia Desemba 2015, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani milioni 4,093.7 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 4,383.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Kiasi hiki kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.0 bila kujumuisha uagizaji wa bidhaa na huduma kwa ajili ya uwekezaji wa moja kwa moja nchini ikilinganishwa na miezi 4.1 iliyofikiwa mwaka 2014. Aidha, katika kipindi hicho, akiba ya fedha za kigeni katika benki za biashara ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 1,012.1 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 759.5 katika kipindi kilichoishia Desemba 2014.

1.2.10 Sekta ya Fedha

Ujazi wa Fedha na Karadha

Katika mwaka 2015, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha kuwa ujazi wa fedha unaendana na mahitaji halisi ya uchumi ili kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na athari za kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. **Ujazi wa fedha** kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 21,971.0 kutoka shilingi bilioni 18,614.2 mwaka 2014, sawa na ukuaji wa asilimia 18.0. Ukuaji ulikuwa juu kidogo ya lengo lililowekwa la asilimia 17.6 kwa mwaka 2015. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa rasilimali za fedha za kigeni katika mabenki na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Rasilimali za fedha za kigeni katika mabenki ziliongezeka kwa asilimia 25.8 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 0.4 mwaka 2014.

Mikopo ya Benki za Biashara kwa Shughuli za Kiuchumi

Katika mwaka 2015, mikopo katika benki za biashara kwa sekta binafsi ilikuwa kwa asilimia 24.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 19.4 mwaka 2014 na lengo la ukuaji wa asilimia 24.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kupungua kwa ukuaji wa madai rasmi kwa Serikali. Aidha, thamani ya mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi ilikuwa sawa na asilimia 17.3 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 15.6 katika mwaka 2014.

Ukuaji wa mikopo kwenye shughuli za uchukuzi na mawasiliano, watu binafsi na shughuli za viwandani uliongezeka mwaka 2015 ikilinganishwa na mwaka 2014. Katika kipindi hicho, sehemu kubwa ya mikopo ilielekezwa katika shughuli za biashara ambazo zilipata wastani wa asilimia 20.2 ya mikopo yote ikifuatiwa na shughuli za watu binafsi (asilimia 18.0).

Amana Katika Benki za Biashara

Katika mwaka 2015, amana katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 18.4 na kufikia shilingi bilioni 19,149.4 kutoka shilingi bilioni 16,177.8 mwaka 2014. Kati ya hizo, sekta binafsi ilichangia shilingi bilioni 18,292.5 ambazo ni sawa na asilimia 95.5 ya amana zote. Aidha, amana za fedha za kigeni na amana za akiba na za muda maalum zilichangia sehemu kubwa ya amana zote kwenye benki za biashara mwaka 2015. Uwiano wa amana za fedha za kigeni katika amana zote uliongezeka na kufikia asilimia 32.9 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 28.8 mwaka 2014 wakati ambapo uwiano wa amana za akiba na za muda maalum ulikuwa asilimia 32.4 mwaka 2015.

Mwenendo wa Viwango vya Riba


Kiwango cha riba za amana za muda maalum kiliongezeka kutoka wastani wa asilimia 8.76 Desemba 2014 hadi asilimia 9.22 Desemba 2015. Aidha, kiwango cha riba za amana za mwaka mmoja kiliongezeka hadi asilimia 11.08 Desemba 2015 kutoka asilimia 10.66 Desemba 2014. Vile vile, wastani wa kiwango cha riba za mikopo kiliongezeka kutoka asilimia 15.75 Desemba 2014 hadi asilimia 16.41 Desemba 2015. Tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 4.14 Desemba 2014 na kufikia asilimia 3.14 Desemba 2015. Mwenendo huu wa viwango vya riba unaonesha kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kufanya biashara na ushindani nchini hivyo kuvutia zaidi uwekezaji wa sekta binafsi.

Thamani ya Shilingi

Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani iliendelea kupungua katika kipindi chote cha mwaka 2015. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani ilipungua kwa wastani wa asilimia 16.8 ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2014. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 1,985.4 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,652.5 mwaka 2014. Kuporomoka kwa thamani ya shilingi hususan robo ya pili (Oktoba hadi Desemba 2015) ya mwaka 2015 kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuimarika kwa Dola

ya Marekani kutokana na kuimarika kwa uchumi wa Marekani, kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za kigeni kwa ajili ya bajeti ya Serikali pamoja na mapato kidogo ya fedha za kigeni yasiyokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma. Mwishoni mwa mwaka 2015, Dola moja ya Marekani iliuza kwa wastani wa shilingi 2,148.5 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,725.8 mwishoni mwa mwaka 2014. Hadi Februari 2016, Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi 2,189.1.

Kielelezo Na. 1.2: Mwenendo wa Thamani ya Shilingi Januari 2015 hadi Februari 2016



Chanzo: Benki ya Tanzania, 2016

1.2.11 Deni la Taifa

Deni la Taifa lilifika shilingi bilioni 45,443.2 Machi 2016 ikilinganishwa na shilingi bilioni 35,010.4 katika kipindi kinachoishia Machi 2014 sawa na ongezeko la asilimia 29.8. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 38,826.5 lilikuwa deni la Serikali na shilingi bilioni 6,592.3 lilikuwa deni la sekta binafsi. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mikopo mipyka kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Kimarekani na malimbikizo ya riba kwa mikopo ya nje kwa nchi zinazotakiwa kutoa msamaha wa madeni kwa mujibu wa *Paris Club* lakini bado hazijatoa.

Deni la nje lilikuwa Dola za Kimarekani milioni 15,435.3 Machi 2016 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 14,265.00 Desemba 2014, sawa na ongezeko la asilimia 13.3. Kati ya kiasi hicho, Dola za Kimarekani milioni 13,158.78 zilikuwa ni deni la Serikali na Dola za Kimarekani milioni 3,009.59

zilikuwa ni deni la sekta binafsi. Kuongezeka kwa deni kulitokana na kupokelewa kwa mikopo mipyga kwa ajili ya miradi ya maendeleo na malimbikizo ya riba kwa nchi ambazo siyo mwanachama wa kundi la Paris.

Deni la ndani liliongezeka kwa asilimia 6.9 kutoka shilingi bilioni 9,376.85 Machi 2014 hadi kufikia shilingi bilioni 10,027.34 Machi 2016. Deni hili linajumuisha dhamana za Serikali za muda mfupi kwa ajili ya kudhibiti mfumuko wa bei kwenye uchumi kiasi cha shilingi bilioni 24.42. Ongezeko la deni la ndani lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya Serikali kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

1.2.12 Mapato na Matumizi ya Serikali

Katika bajeti ya mwaka 2015/16, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 22,495.5 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Sera za mapato ya ndani katika mwaka 2015/16 zililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 13,475.6 sawa na asilimia 14.3 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 12,363 na mapato yasiyo ya kodi shilingi bilioni 1,112.7. Aidha, mapato yatokanayo na vyanzo vya Halmashauri yalikadiriwa kufikia shilingi bilioni 521.9 sawa na asilimia 0.6 ya Pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Aprili 2016, makusanyo ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 11,481.4 sawa na asilimia 99 ya makadirio ya shilingi bilioni 11,550.8 katika kipindi hicho. Mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 10,170.1 ikiwa ni asilimia 100 ya lengo.

Kwa upande wa **matumizi** ya mwaka 2015/16, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 22,495.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 16,576.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 5,909.1 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Aprili 2016, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 16,856.9 kwenye mafungu mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti, sawa na asilimia 90 ya lengo katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 13,647.1 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3,209.8 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Makadirio ya mwaka 2016/17 ni kuwa, Serikali imepanga kukusanya na kutumia shilingi bilioni 29,539.6. Jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 18,463.5 sawa na asilimia 62.5 ya mapato yote. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga

kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya shilingi bilioni 15,105.1 sawa na asilimia 82 ya mapato ya ndani. Aidha, mapato yasiyo ya kodi na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 2,693.0 na shilingi bilioni 665.4 kwa mtiririko huo. Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia shilingi bilioni 3,600.8 ambayo ni asilimia 12 ya mapato yote. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 7,475.3 kutoka soko la ndani na nje kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva, mikopo mipywa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo pamoja na kulipia malimbikizo ya madai yaliyohakikiwa. Kwa upande wa **matumizi**, katika mwaka 2016/17 Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 17,719.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo yatakuwa shilingi bilioni 11,820.5 sawa na asilimia 40 ya matumizi yote ambapo kiasi cha shilingi bilioni 8,702.7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,117.8 ni fedha za nje.

1.2.13 Matarajio ya Ukuaji wa Uchumi kwa Mwaka 2016/17

Katika mwaka 2016/17, shabaha na malengo ya uchumi jumla na bajeti ni kama ifuatavyo:-

- (i) Pato Halisi la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2016 kutoka 7.0 mwaka 2015;
- (ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 5.0 na asilimia 8.0 mwaka 2016;
- (iii) Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri kufikia asilimia 14.8 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16, na kuendelea kuongezeka kufikia asilimia 16.9 ya Pato la Taifa mwaka 2016/17;
- (iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.8 ya Pato la Taifa mwaka 2016/17 kutoka asilimia 12.6 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16;
- (v) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 23.2 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16 hadi asilimia 27.0 mwaka 2016/17;
- (vi) Nakisi ya abjeti inakadiriwa kuwa asilimia 4.5 ya pato la taifa mwaka 2016/17 kutoka makadirio ya bajeti ya asilimia 4.2 mwaka 2015/16;
- (vii) Nakisi katika urari wa malipo ya kawaida kuwa asilimia 7.9 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16 na kupungua hadi asilimia 7.5 mwaka 2016/17; na
- (viii) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne Juni 2017.

SURA YA PILI

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO 2015/16

2.1 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2015/16

Katika mwaka 2015/16, Serikali ilitenga shilingi bilioni 5,909.1 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 4,246.9 na fedha za nje ni shilingi bilioni 1,662.2. Fedha zilitotengwa kwa ajili ya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni shilingi bilioni 739.4 ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 595.0 na fedha za nje ni shilingi bilioni 144.4. Kwa upande wa Wizara, Taasisi, Wakala na Idara zinazojitegemea zilitengewa shilingi bilioni 5,169.7 ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 3,651.9 na fedha za nje ni shilingi bilioni 1,517.8.

Fedha za miradi ya maendeleo zilitotolewa hadi Aprili 2016 ni shilingi bilioni 3,209.8. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 2,819.9 na fedha za nje ni shilingi bilioni 398.841. Fedha hizo za maendeleo zilitotolewa ni sawa na asilimia 65 ya lengo la shilingi bilioni 4,922.5. Fedha za ndani zilitotolewa ni sawa na asilimia 79 ya lengo la kutoa fedha za ndani shilingi bilioni 3,537.4 na fedha za nje zilitotolewa ni sawa na asilimia 29 ya lengo la shilingi bilioni 1,385.2.

2.2 Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa

Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa ilitokana na uchambuzi wa kimaabara kwa sekta sita za mwanzo uliofanyika mwaka 2013. Nchi ya Malaysia ambayo inatumia mfumo huo ilishirikiana na Tanzania katika uchambuzi wa kimaabara wa maeneo ya Kilimo, Elimu, Maji, Nishati, Uchukuzi, Utafutaji wa Rasilimali Fedha na baadaye kwa Afya na Mazingira ya Kufanya Biashara. Malengo makuu yalikuwa ni kuwezesha ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo iliyoainishwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano (2011/12 – 2015/16). Mfumo huo ulikusudiwa kuanza kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu (2013/14 – 2015/16) chini ya usimamizi wa Ofisi ya Uratibu na Ufuatiliaji (PDB). Katika kipindi cha utekelezaji wa mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

2.2.1 Sekta ya Kilimo: Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kupata hatimiliki kwa mashamba makubwa matano yenye jumla ya hekta 123,394 ya Pangani, Kitengule, Bagamoyo, Lukulilo na Mkulazi; kuendelea taratibu

za uhaulishaji wa ardhi ya mashamba makubwa ya uwekezaji ya Tawi na Muhoro (Rufiji), Kasulu na Mahurunga (Mtwara Vijijini); kupatikana kwa watoa huduma binafsi kwa ajili ya skimu 30 za umwagiliaji katika Wilaya za Mbarali, Kyela na Iringa na kupelekea uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka tani 4.1 mwaka 2014 hadi tani 6.0 kwa hekta mwaka 2015; ujenzi wa maghala 8 katika Wilaya za Mbarali (4), Kyela (2) na Iringa vijijini (2) ambapo upo katika hatua za mwisho kukamilika na kukamilika kwa ghala moja kati ya maghala mawili (2) ya Wilaya ya Kyela.

2.2.2 Sekta ya Elimu: Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilika ujenzi wa vyumba vyaa madarasa na maabara katika shule 167 sawa na asilimia 63.25 ya lengo; kutoa mafunzo kwa walimu 1,559 ya jinsi ya kutumia teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kufundishia masomo ya Sayansi na Hisabati; kutoa mafunzo kwa walimu 3,819 wa Hisabati, Baiolojia, Kiingereza na Kiswahili; kupatiwa mafunzo ya usimamizi wa shule kwa walimu 3,001; na kuongezeka kwa ufaulu wa shule za msingi kutoka asilimia 57 mwaka 2014 hadi asilimia 67.8 mwaka 2015. Aidha, ufaulu kwa shule za sekondari ulikuwa asilimia 67.5 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 70 mwaka 2014.

2.2.3 Sekta ya Nishati: Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilika kwa ujenzi wa bomba la gesi (km 542) kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam na ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi Madimba (Mtwara) na Songosongo (Lindi); kuunganisha umeme kwa wateja wapya 8,078 kuitia mradi wa usambazaji wa umeme vijijini awamu ya pili. Idadi ya wateja waliounganishiwa umeme chini ya miradi ya REA na TANESCO imefikia 241,401 mwaka 2015 na upatikanaji wa huduma za umeme umeongezeka kutoka asilimia 18 mwaka 2012 hadi asilimia 40 mwaka 2015.

2.2.4 Sekta ya Uchukuzi: Katika eneo la **Bandari**, hatua zilizofikiwa ni: kupungua kwa muda wa meli kukaa bandarini kwa ajili ya kupakia na kupakua mizigo kutoka siku 4.8 hadi 2.8 ikilinganishwa na lengo la siku 4; kuongezeka kwa uwezo wa bandari kupakua magari kwa kila shifti moja ya saa 8 kutoka magari 800 hadi magari 859; kuongezeka kwa idadi ya shehena zilizohudumiwa na bandari ya Dar es Salaam kutoka tani milioni 10.3 hadi 14.6 ikilinganishwa na lengo la tani milioni 9.87. Katika eneo la **Reli**, mafanikio ni pamoja na: kukamilika kwa utandikaji wa reli nzito ya ratili 80/yadi kati ya stesheni za Kitaraka na Malongwe

(km 89 kutoka Dar – es - Salaam); kukamilika kwa ujenzi wa madaraja 3 kati ya stesheni za Bahi na Kintiku (km 517 kutoka Dar es Salaam) na madaraja 2 kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe (km 293 na km 303 kutoka Dar es Salaam); ukarabati wa eneo la reli kati ya Kilosa na Gulwe lililoathiriwa na mafuriko; ununuzi wa vichwa vipyta vya treni 13, mabehewa mapya 22 ya abiria kwa ajili ya huduma ya treni maalum (Deluxe), kupokelewa kwa mabehewa mapya ya mizigo 274 na mabehewa ya breki 34; kukamilika uundaji upya wa vichwa 10 vya treni, mabehewa ya mizigo 89 na mabehewa 31 ya abiria katika karakana ya Morogoro.

2.2.5 Sekta ya Maji: Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilika kwa ujenzi wa miradi ya maji 975. Walionufaika na kukamilika kwa miradi hii ni wananchi milioni 5.75 ambapo jumla ya vituo 24,129 vya kuchotea maji vimejengwa katika Halmashauri 148; na kuanzisha Jumuiya za Watumia Maji (COWSOs) 1,802 kati ya hizo Jumuiya 875 zimesajiliwa na Halmashauri za Wilaya ili kutoa huduma za maji vijijini kwa ufanisi.

2.2.6 Utafutaji wa Rasilimali Fedha: Utekelezaji ni pamoja na: kuanza kutumia kanzidata bora inayohifadhi taarifa na kuthaminisha bidhaa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, hivyo kutoa makadirio bora zaidi ya viwango vya kodi; na kuanza kutoza tozo maalumu kwa ajili ya uwekezaji katika elimu ikiwa ni asilimia 2.5 ya mapato ghafi ya kampuni za simu.

2.3 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati

2.3.1 Miundombinu

A. Reli

- (a) **Mradi wa kubadilisha km 197 za njia ya reli na kuweka kiwango cha ratili 80 kwa yadi:** Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuufanya ukarabati mgodi wa kokoto wa Tura kwa kununua na kufunga vipuri vipyta, kuondoa vipuri vilivyochakaa, kununua mafuta na vilainishi na kufanyiwa majoribio. Mgodi huu uliana tena uzalishaji wa kokoto Februari 2016.
- (b) **Ukarabati na Ununuzi wa Vichwa Vya Treni, Mabehewa na Vifaa Mbalimbali na Matengenezo ya Kawaida ya Njia ya Reli:** Kazi zilizofanyika ni kukamilisha uundwaji upya wa vichwa 3 kati ya 9; matengenezo ya madaraja yenye hali mbaya ili kuruhusu treni kupita; kuboresha mfumo wa mawasiliano ya njia ya reli kati ya Dar es Salaam na Dodoma; na ununuzi wa vipuri kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa breki za

- mabehewa.
- (c) **Mradi wa uboreshaji wa njia ya Reli ya TAZARA:** Ukarabati wa mtambo wa kuzalisha kokoto wa Kongolo – Mbeya unaendelea na kukamilika kwa kubadilishwa mataruma 8,900 ya zege na 3,422 ya mbao.
- (d) **Mradi wa usafiri wa Treni ya Abiria Dar es Salaam:** Mshauri mwelekezi (Kampuni ya GIBB) kutoka Afrika Kusini amesaini mkataba Machi, 2015 na ameanza kufanya kazi ya upembusi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia mpya za reli Jijini Dar es Salaam. Kazi hii inategemewa kukamilika Desemba, 2016.

B. Bandari

(a) Bandari za Bahari Kuu

(i) Bandari ya Dar es Salaam

Ujenzi wa gati Na. 13 na 14: Kukamilisha kazi za maandalizi ya mradi, hususan upembusi yakinifu na tafiti zitakazotoa picha halisi ya mradi na gharama zake, ikijumuisha uondoshaji wa gati la mafuta (KOJ) na mabomba yake katika eneo linalotarajiwa kujengwa gati Na. 13 na 14, Kurasini.

Uboreshaji wa gati Na. 1 – 7: Kuendelea na taratibu za zabuni kwa ajili ya kupata mkandarasi wa kazi za ujenzi. Uboreshaji wa gati Na. 1 – 7 utajumuisha ujenzi wa gati Na. 4 la magari (RoRo terminal) pamoja na kubadili gati Na. 5 - 7 kuwa gati la makasha (*container terminal*).

(ii) Bandari ya Mtwara

Maandalizi ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa gati nne (4) kwa awamu yanaendelea ambapo Mamlaka ya Bandari Tanzania inaendelea na upembusi yakinifu wa ujenzi wa gati zote nne (4). Aidha, majadiliano kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na kampuni binafsi ya Dangote yanaendelea kwa ajili ya ujenzi wa gati la tano katika eneo la Kisiwani mkoani Mtwara litakalotumika kuhudumia mizigo ya kampuni hiyo.

(iii) Bandari ya Mbegani – Bagamoyo

Kusainiwa kwa makubaliano ya awali (MOU) Oktoba 2014 kati ya wabia watatu ambao ni Serikali, Kampuni ya China Merchants Holding International (CMHI) na General State Reserve Fund (GSRF) ya Oman. Shughuli zinazoendelea ni kukamilisha malipo ya fidia yanayokadiriwa kufikia shilingi bilioni 58 katika eneo la hekta 800 lililotengwa kwa ajili ya shughuli za bandari.

(iv) Bandari ya Mwambani – Tanga

Kazi ya awamu ya pili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuthibitisha manufaa (viability) ya ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani unaendelea. Awamu ya pili itazingatia ujenzi wa reli mpya na makisio ya shehena ya kutosha kuvutia wawekezaji ambayo haikuzingatiwa kikamilifu katika awamu ya kwanza.

(b) Bandari za Maziwa Makuu

(i) Bandari za Ziwa Tanganyika

Ujenzi wa bandari ndogo za Sibwesa, Kagunga na Karema zipo katika hatua mbalimballi kama ifuatavyo:- (i) **Sibwesa**: Mkataba wa ujenzi wa gati la Sibwesa ulisainiwa Mei, 2015 kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na M/S Saxons Building Contractor Ltd kwa utekelezaji katika kipindi cha miezi 12; (ii) **Kagunga**: Mkataba wa ujenzi wa gati la Kagunga ulisainiwa Aprili, 2015 kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na M/S Kashere Enterprises Ltd ambapo ujenzi unaendelea na umekamilika kwa asilimia zaidi ya 25; na (iii) **Lagosa**: Mamlaka ya Bandari Tanzania inaendelea na majadiliano na Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa gati la bandari ndogo ya Lagosa; na **Kigoma**: kukamilika kwa tathmini ya mazingira kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria katika bandari ya Kigoma.

(ii) Bandari za Ziwa Victoria

Kuboresha Bandari ya Mwanza, upanuzi wa Bandari za Musoma na Bukoba: kazi ya upembuzi yakinifu inayotekelawa na kampuni ya Royal Haskoning ya Uholanzi kwa ajili ya uboreshaji wa bandari zilizopo katika Ziwa Viktoria (Mwanza, Musoma and Bukoba) inaendelea.

Ujenzi wa gati za Ntama, Lushamba na Kyamkwiki: Mkataba wa ujenzi wa gati la Ntama ulisainiwa Oktoba, 2014 kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mkandarasi M/s Gemen Engineering Company Ltd na ujenzi wa gati la Lushamba ulisainiwa Novemba, 2014 kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mkandarasi M/s Nangh'ware Mhando Ltd.

(iii) Bandari za Ziwa Nyasa

Ujenzi wa gati ya bandari ya Itungi pamoja na gati la Ndumbi: Ujenzi wa gati ya Bandari ya Itungi umefikia asilimia 90, zabuni ya ujenzi wa

gati la Ndumbi zilifunguliwa Juni 2015 na tathmini imekamilika. Hata hivyo gharama zilizowasilishwa na wazabuni zilikuwa juu sana kuliko bajeti iliyotengwa. Kutohana na hali hii, Mamlaka ya Bandari Tanzania inakusudia kutekeleza mradi huu kwa kutumia wataalamu wa ndani (in-house).

C. Barabara

(a) Miradi ya Barabara Kuu

Kukamilika kwa ujenzi wa km 323.42 za barabara kuu ikilinganishwa na lengo la kilomita 523 kwa kiwango cha lami; na kukamilika kwa ukarabati wa km 29 za barabara kuu kwa kiwango cha lami ikilinganishwa na lengo la kilomita 113;

(b) Mradi wa Barabara zenyenfungua Fursa za Kiuchumi

(i) **Barabara zilizokamilika:** Tunduma – Sumbawanga (km 223.2); Ndundu - Somanga (km 60); Mbeya - Lwanjilo – Chunya (km 72); Iringa – Dodoma (km 259.8); na Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35)

(ii) **Barabara zinazoendelea kujengwa**

- Itoni – Mkiu – Ludewa – Manda (km 211) ujenzi umeanza;
- Sumbawanga – Mpanda - Nyakanazi (km 770.9) na Kidahwe - Nyakanazi (km 310): sehemu ya Sumbawanga - Kanazi (km 75) asilimia 68.6; Kanazi – Kizi - Kibaoni (km 76.6) asilimia 50.3; Sitalike – Mpanda (km 39.9) asilimia 76; Kidahwe – Kasulu (km 50) asilimia 14; Kasulu – Nyakanazi (km 50) asilimia 13.6 na Kibondo - Nyakanazi (km 50) asilimia 12.95.
- Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7): sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35) ujenzi umekamilika na sehemu ya Tabora – Nyahua (km 85) asilimia 92.15
- Mbeya – Makongorosi - Mkiwa (km 528): sehemu ya Mbeya – Lwanjilo - Chunya (km 72) umekamilika asilimia 100; Manyoni – Itigi – Tabora (km 264.35): sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35) ujenzi umekamilika; Nyahua – Tabora (km 85) asilimia 90.1;
- Dodoma – Babati (km 251.4); sehemu ya Dodoma – Mayamaya km (43.65) asilimia 80; Mayamaya – Mela (km 99.35) asilima 54.09; na Mela – Bonga (km 88.8) asilimia 56.26;
- Masasi - Songea – Mbamba Bay (km 868.7); Tunduru-Mangaka- Mtambaswala (km 202.5) sehemu ya Mangaka – Nakapanya (km 70.5) asilimia 59.62 ; Nakapanya – Tunduru (km 66.5) asilimia 56 ; Mangaka – Mtambaswala km (65.5) asilimia 51.81. Namtumbo – Tunduru (km 193), sehemu ya Namtumbo – Kilimasera (km 60.7)

asilimia 93.78; Kilimasera – Matemanga (km 68.2) asilimia 33.1 na Matemanga – Tunduru (km 58.7) asilimia 57.2;

- Mwigumbwi – Maswa – Bariadi - Lamadi (km 171.8); Bariadi – Lamadi (km 71.8) asilimia 97; na Mwigumbi - Maswa (km 50.3) mkandarasi amekwisha andaa vifaa kwa ajili ya kuanza ujenzi.

- (iii) **Barabara zilizo katika hatua ya upembuzi yakinifu/usanifu wa kina:** Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396); Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 359); na Bagamoyo (Makurunge) - Sadani – Tanga (km 178)

(c) Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani:

- (i) **Barabara zilizokamilika** ni Arusha – Namanga (km 105), Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5) na Isaka – Ushirombo (km 132), Nyanguge – Musoma (km 183);
- (ii) **Barabara zinazoendelea ni pamoja** na: mchepuko wa Usagara – Kisesa (km 17) asilimia 60; Nyamuswa – Bunda –Kisorya – Nansio (Km 121.9), sehemu ya Bulamba – Kisorya (km 51) asilimia 12.85; Isaka – Ushirombo - Lusahunga (km 242), sehemu ya Isaka – Ushirombo (km 132) ujenzi umekamilika na sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110) asilimia 50.81; Lusahunga – Rusumo (km 92) na Nyakasanza – Kobero usanifu wa kina umekamilika; Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112) asilimia 52.8, Arusha – Moshi – Holili na Arusha Bypass (km 140) mkandarasi wa ujenzi umeanza.

(d) Barabara za Mikoa: Malengo kwa mwaka wa fedha 2015/16 yalikuwa ni kujenga kilomita 109.28 za barabara kwa kiwango cha lami. Utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa kilomita 12.25 za barabara kwa kiwango cha lami.

(e) Barabara za Kupunguza Msongamano Mijini (km 109.35)

- (i) **Barabara zilizokamilika:** Ubungo Bus Terminal – Mabibo - Kigogo Roundabout (km 6.4); Jet Corner – Vituka – Devis Corner (km 10.3); Ubungo Maziwa – External (km 2.25); Kibamba – Kisopwa (Kibamba – Mloganzila section) (4 km).
- (ii) **Barabara zinazoendelea kujengwa:** Kigogo Roundabout - Bonde la Msimbazi - Twiga/Msimbazi Junction (km 2.7) asilimia 86; Tabata Dampo – Kigogo (km 1.65) asilimia 53 na Mbezi (Morogoro Road); Mbezi Mwisho – Malambamawili - Kifuru - Kinyerezi –Banana (km 14) asilimia 30; Tegeta Kibaoni - Wazo – Goba - Mbezi Mwisho (km 20) asilimia 83; Tangi Bovu - Goba (km 9) asilimia 69; Kimara Baruti – Msewe - Changanyikeni (km 2.6) asilimia 40; Kimara - Kilungule –

External (km 3) asilimia 64; na Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi (km 20) asilimia 85.

- (iii) **Barabara ambazo zipo kwenye taratibu za kuwapata wakandarasi:** Banana- Kivule – Msongola, Ardhi - Makongo – Goba pamoja na Maji Chumvi - Chang'ombe – Barakuda.
- (iv) **Mradi wa Mabasi yaendayo haraka (Dar es Salaam Bus Rapid Transit – BRT):** ujenzi wa awamu ya kwanza ya mradi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka na vituo vyake umekamilika na usafirishaji wa abiria ulianza rasmi Mei, 2016.

(f) Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyover)

Mkataba wa ujenzi barabara za juu eneo la TAZARA ulisainiwa Oktoba, 2015 kati ya Serikali na mkandarasi M/s Sumitomo Mitsui Construction Co. Ltd ya Japan, wenge thamani ya shilingi bilioni 87.156. Ujenzi umeanza na unatarajiwu kukamilika katika kipindi cha miezi 35. Serikali pia imetangaza zabuni ya ujenzi wa barabara za juu (Interchange) katika makutano ya Ubungo Januari, 2016.

(g) Mradi wa Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 200)

Mtaalam Mshauri (*Transaction Advisor*) anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za ununuzi kwa ajili ya kuwapata wawekezaji.

(h) Madaraja

Katika mwaka 2015/16 malengo yalikuwa ni kukamilisha ujenzi wa madaraja 15 katika barabara kuu na madaraja 21 katika barabara za Mikoa. Mafanikio ya utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa madaraja ya Mwalimu Nyerere - Kigamboni, Maligisu, Nangoo, na Ruhekei katika barabara kuu na madaraja 2 katika barabara za Mikoa. Aidha, Daraja la Kigamboni (Nyerere Bridge) lilizinduliwa rasmi na kuanza kutumika Aprili, 2016 na kuanza kutumika. Madaraja 6 ambayo ujenzi wake unaendelea ni: Kavuu (asilimia 50), Kilombero (asilimia 42.45), Lukuledi II (asilimia 25), Mbutu (asilimia 95) na Sibiti (asilimia 22); kukamilika kwa taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kupitia usanifu wa nyaya zinazoshikilia daraja la Kirumi (Mara) na kusimamia kazi ya ukarabati wa daraja hilo; kukamilika kwa usanifu wa daraja la Ruhuhu (Ruvuma) na daraja la Momba (Songwe); na kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa daraja jipya la Selander (Dar-es-Salaam).

(i) Vivuko na Maegesho

Vivuko: ukarabati wa kivuko cha MV Nyerere ulikamilika na ujenzi wa kivuko kipywa cha Magogoni – Kigamboni umeanza.

Maegesho: Kukamilika kwa ujenzi wa maegesho ya Iramba – Majita, Msangamkuu – Msemo, Ilagala – Kajeje, Luchelele, Igogo na Sweya kwa ajili ya kivuko cha kasi ili kupunguza msongamano jijini Mwanza, na ujenzi wa maegesho ya muda katika eneo la Magogoni (Dar es Salaam) na Mbegani (Bagamoyo).

(j) Usafiri wa Majini

Meli: Kuanza ukarabati wa meli mbili (2) za abiria na mizigo na matishari (Self-Propelled cargo Barges) katika Ziwa Nyasa: Mkataba wa uundaji wa matishari mawili (2) ulisainiwa Januari, 2015 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2016 kwa gharama ya shilingi bilioni 11.252.

D. Nishati

(a) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam (km 542): Kukamilika kwa ujenzi wa bomba la gesi na mitambo ya kusafisha gesi katika maeneo ya Madimba na Songosongo; na kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 32 zenyewe uwezo wa kuhudumia wafanyakazi 172 katika maeneo ya Madimba na Songosongo;

(b) Mtambo wa Kufua Umeme Kinyerezi I (MW 150): Kukamilika kwa usimikaji wa mitambo 4 ya kufua umeme yenye uwezo wa kuzalisha MW 150 na kuzinduliwa rasmi na Rais wa Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Oktoba, 2015; Mitambo imefanyiwa majaribio ambapo inazalisha umeme wa MW 150 na umeingizwa kwenye gridi ya Taifa pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 220 kutoka Kinyerezi hadi Kimara na njia ya umeme wa msongo wa KV 132 kutoka Kinyerezi hadi Gongo la Mboto.



Mradi wa Kuzalisha umeme (MW 150) kwa kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I ukiwa umekamilika, Desemba 2015.

- (c) **Mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi II (MW 240):** Serikali kukamilisha malipo ya dola za Kimarekani milioni 51.6 (sawa na shilingi bilioni 110) ambayo ni mchango wa Serikali kwenye ugharamiaji wa ujenzi sawa na asilimia 15 na kuanza kwa shughuli za ujenzi wa mitambo hii.
- (d) **Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo kV 220 Makambako – Songea (km 250):** Mradi umegawanyika katika sehemu mbili: ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea; na ujenzi wa njia za usambazaji umeme wa kV 33/0.4. Mkataba wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ulisainiwa Agosti, 2015 na kazi ya kusanifu Ujenzi wa mradi inaendelea; mkandarasi wa mradi wa njia ya usambazaji umeme alianza kazi rasmi Desemba, 2014; na zoezi la ulipaji fidia takriban shilingi bilioni 7.2 katika mkoa wa Njombe na Ruvuma limekamilika.
- (e) **Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 Iringa - Shinyanga (km 670):** Ujenzi wa nguzo 594 kwa Lot Na. 1 (Iringa – Dodoma), umekamilika; nguzo 571 kati ya 586 zimesimikwa kwa Lot Na. 2 Dodoma – Singida) na nguzo 571 kati ya 594 zimesimikwa kwa Lot Na. 3 (Singida – Shinyanga). Kazi ya kuvuta nyaya ili kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa inaendelea.

- (f) **Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 North West Grid (Mbeya – Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi km 1,148):** Shughuli zinazoendelea ni kazi ya kufanya uthamini wa ardhi na mali katika eneo la mradi na kuboresha upembuzi yakinifu na usanifu wa kubadilisha msongo wa umeme kutoka kV 220 hadi kV 400 unaotekelawa na kampuni ya SWECO ya Sweden. Shughuli zilizokamilika ni taratibu za kupata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupozea umeme Geita upimaji wa kilomita 321 za mkuza wa njia ya umeme kutoka Mbeya hadi Sumbawanga.
- (g) **Mradi wa msongo wa kV 400 North - East Grid (Dar es Salaam – Tanga – Arusha km 682):** Upimaji wa ardhi na kuweka mipaka ya eneo la mradi kutoka Kinyerezi (DSM) hadi Chalinze (Pwani) na tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi imekamilika. Aidha, Serikali na Benki ya Exim ya China wamekamilisha majadiliano kuhusu mkopo wa Dola za Marekani milioni 588.79.
- (h) **Mradi wa kusambaza umeme katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Shinyanga na Geita (Mradi wa Electricity V):** Shughuli zilizokamilika ni pamoja na ukarabati na ufungaji wa mitambo katika kituo cha Ilala; ukarabati na upanuzi wa kituo cha cha kupozea umeme Njiro na ujenzi wa msingi katika kituo cha Sokoine umefikia asilimia 70. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2016 wateja 4,243 wameunganishiwa umeme na TANESCO kupitia mradi huu.
- (i) **Miradi ya Umeme Vijijini (REA Turnkey Phase II):** Kazi zilizotekelawa ni pamoja na ujenzi wa vituo sita (6) vya kuongeza nguvu za umeme wa kV 11/33 katika miji ya Kigoma, Kasulu, Kibondo, Ngara, Mbinga na Tunduru; ujenzi wa njia za kusambaza umeme zenye urefu wa km 15,000 za msongo wa kV 33; ujenzi wa vituo vidogo 3,100 vya kupoza na kusambaza umeme (33/0.4/0.23); na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme wenyewe urefu wa km 7,000. Mradi umeunganisha wateja 74,379 wa awali kati ya wateja 250,000 hadi kufikia 31 Machi 2016. Aidha, kazi za kuunganisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya 13 za Mkalama, Kakonko, Uvinza, Mlele, Kalambo, Nyasa, Buhigwe, Nanyumbu, Momba, Itilima, Busega, Chemba na Kyerwa zinaendelea.

E. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

(a) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Ujenzi na upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano awamu ya I na II

umekamilika katika mikoa 24 ya Tanzania Bara kwa km 25,954. Kati ya hizo, km 7,560 zimejengwa na Serikali katika awamu ya I na ya II ya mradi wa *National ICT Infrastructure Backbone*, km 18,000 zimejengwa na Kampuni ya Mawasiliano ya *Viettel* na km 394 za mkongo wa mjini (metrol fiber) zimejengwa kwa ubia kati ya Serikali na Umoja wa kampuni ya simu za mikononi. Mafanikio mengine ni pamoja na: kuunganisha Tanzania na mikongo ya baharini ya SEACON na EASSy na kutoa maunganisho ya mawasiliano kwa nchi za jirani zikiwemo Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi; kutoa huduma za maunganisho kwenye mkongo wa kimataifa wa SEAS (Seychelles East Africa System) unaouanganisha nchi za Seychelles na Tanzania na Dunia kwenye mikongo mingine ya Kimataifa; kuendelea na kazi ya kuunganisha Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; kukamilika kwa ujenzi wa Mikongo ya mijini katika mikoa ya Mwanza (km 36) na Arusha (km 58) na kuendelea na ujenzi katika mikoa ya Morogoro (km 18), Dodoma (km 42), Kilimanjaro (km 35.08) na Tanga (km 43.28); na kuendelea na ujenzi wa jengo la Data Center katika eneo la Kijitonyama.

(b) Maeneo Maalum ya TEHAMA (ICT Park)

Mradi unalenga kuvutia uwekezaji katika sekta ya TEHAMA ili kuboresha upatikanaji wa huduma za TEHAMA na utumiaji wa TEHAMA katika shughuli za uzalishaji pamoja na utoaji huduma. Kazi zilizotekelawa ni kukamilika kwa malipo ya fidia ya shilingi bilioni 1.7 katika eneo lenye ukubwa wa ekari 438 lililopo EPZ Bagamoyo.

(c) Anuani za makazi na misimbo ya posta

Mradi unaendelea na awamu ya II ya utekelezaji katika jiji la Dar-es-Salaam na Zanzibar. Shughuli zilizotekelawa katika jiji la Dar-es-Salaam ni ukusanyaji wa taarifa mbalimbali za mitaa, kuweka majina ya mitaa na namba za nyumba katika kata 18 za Manispaa za Dar-es-Salaam (Ilala 6, Kinondoni 7 na Temeke 5). Malengo ni kuanzisha utaratibu wa kutumia anuani za makazi na simbo za posta katika kutambua maeneo mbalimbali ya mitaa Nchini.

F. Maji

- (a) Mradi wa Maji wa Ruvu Chini – Pwani:** Ulazaji wa bomba la kusafirisha maji kutoka mtambo wa Ruvu Chini (Bagamoyo) hadi Dar es Salaam (km 55.38) umekamilika ambapo majoribio ya kusukuma maji kwenye bomba na kuunganisha kwenye matanki yaliyopo Chuo Kikuu Ardhi yanaendelea. Hivyo, kukamailika kwa upanuzi wa mradi wa maji wa Ruvu Chini na upanuzi wa mtambo wa kusafirisha maji kumeongeza uzalishaji maji kutoka lita milioni 180

hadi lita milioni 270 kwa siku. Maeneo ambayo wakazi wake wananaufaika na mradi huu ni maeneo ya uwekezaji (EPZ) Bagamoyo, Chasimba, Buma, Zinga, Kerege na Mpiji kwa mkoa wa Pwani, na Bunju, Wazo, Salasala, Madale na Kinzudi Mbezi Juu, Goba, Kawe, Makongo, Mwenge, Msasani, Mikocheni, Mlalakua, Masaki, Sinza, kijitonyama, Manzese, Kinondoni, Magomeni, Kigogo, Vingunguti, Buguruni, Kariakoo na Ilala kwa mkoa wa Dar es salaam.



Eneo la ndani la mtambo wa kuzalisha maji ukiwa umekamilika baaada ya kufungwa pampu mpya zenye uwezo wa kusukuma maji kiasi cha lita milioni 270 kwa siku kwenda Dar es Salaam na maeneo ya Mkoa wa Pwani, Machi, 2016.

- (b) Mradi wa Maji Ruvu Juu – Pwani:** Upanuzi wa chanzo cha maji eneo la Ruvu Darajani, ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara na ujenzi wa tanki jipya la Kibamba umekamilika na mradi upo katika hatua za majaribio. Mradi huu umeongeza uwezo wa kuzalisha maji kutoka lita milioni 82 kwa siku hadi lita milioni 196 kwa siku. Maeneo yanayonufaika na mradi huu ni pamoja na Mlandizi, Kibaha, Kibamba, Kiluvya, Kinyerezi, Mbezi, Kimara, changanyikeni, Segerea, Vingunguti, Airport, Ukonga, Kibangu, Makuburi na Kipawa.



Pampu za Kusukuma Maji, Ruvu Juu.

- (c) Mradi wa Visima Virefu vya Kimbiji - Dar es Salaam na Mpera - Pwani:** Kukamilika kwa uchimbaji wa visima 5 na kufanya idadi ya visima vilivyokamilika kuwa 9 katika ya visima 20 vya uzalishaji maji. Visima hivi vitatumika kama vyanzo vya maji kupitia mradi wa Usambazaji Maji Jijini Dar es Salaam. Vile vile, uchimbaji wa visima 11 vilivyobaki unaendelea. Aidha, mkandarasi amechimba visima 7 vya uchunguzi wa mwendo wa maji chini ya ardhi katika mwamba wa Kimbiji na Mpera katika maeneo ya Chanika, Mkuranga, Mwasonga, Kibada, Buyuni, Changani na Nzasa - Chanika. Mradi huo ukikamilika utazalisha maji lita milioni 260 kwa siku na kunufaisha wakazi wa maeneo ya Kurasini, Mkuranga, Kongowe, Chanika, Ukonga, Pugu, Kinyerezi, Kigamboni, Mbogala, Mtoni na Kisarawe.
- (d) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda - Morogoro:** Kukamilika kwa usanifu wa bwawa na barabara kutoka Kidunda hadi Ngerengere (km 75). Vile vile, fidia kiasi cha shilingi bilioni 7.85 imelipwa kwa wananchi 2,603 kupisha mradi katika maeneo ya vijiji vya Kwanyagongo, Kwatupa, Kariakoo, Bwira chini, Bwira juu, Vikunge na Mikoroshini vilivyopo ndani ya eneo la mradi.
- (e) Miradi ya Maji Vijijini:** Kukamilika kwa miradi mipy 1,160 ya maji ya vijiji 10 katika vijiji 1,206 yenye vituo 28,499 vya kuchotea maji katika Halmashauri 148. Miradi hiyo imeboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama

kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi kutoka asilimia 40 Julai, 2013 hadi asilimia 72 Machi, 2016 ambapo idadi ya wananchi walionufaika na huduma hiyo imeongezeka kutoka milioni 15.2 hadi milioni 21.9. Aidha, katika kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakuwa endelevu, Jumuiya 909 za watumia maji zimesajiliwa.



Tanki la mradi wa maji wa Vijiji Kumi katika Manispaa ya Shinyanga - Bushola likiwa limekamilika ambalo litahudimia watu 2,438, Januari 2016

- (f) Upanuzi wa Mradi wa Maji Ziwa Victoria – Shinyanga – Kahama:** Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa usanifu wa ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya miradi ya maji kwa miji ya Tabora, Igunga na Nzega; kukamilika kwa usanifu wa kina wa mradi na kuanza majadiliano baina ya Serikali ya Tanzania na India ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za kugharamia utekelezaji wa mradi.
- (g) Miradi ya Maji ya Kitaifa:** Serikali imeendelea kuhudumia miradi ya Maji ya Kitaifa ya **Makonde, Wanging'ombe na Handeni Trunk Main** kwa kukarabati miundombinu ya maji, ununuzi wa pampu, mabomba na kugharamia umeme kwa ajili ya kuendesha mitambo; kuanza usanifu na upembusi yakinifu katika mradi wa **Mugango – Kiabakari**; na kukamilisha usambazaji wa maji katika vijiji vya Mihuga, Masimbani, Kweikonje, Mandamazingara, Mkange, Kwan'gandu, Pongwe Kiona, Kifuleta na Kwaruhombo katika awamu ya pili ya mradi wa **Chalinze**.

2.3.2 Kilimo

A. Kilimo cha Mazao

(a) Uwekezaji katika Kilimo cha Miwa na Mpunga: Kuhakikiwa kwa mipaka ya mashamba manne (4) ya Muhoro, Kumsenga, Mahurunga na Tawi na kuanza kwa taratibu za uhaulishaji (recategorisation) wa mashamba hayo; kuandaa hatimiliki za Kimila 1,513 kwa wakulima wanaozunguka mashamba ya Lukulilo na Ngalimila; na kukamilika kwa mpango - kina wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji vinavyozunguka mashamba ya Bagamoyo na Mkulazi.

(b) Skimu 78 za Umwagiliaji Mpunga

Mradi umewezesha kuanza ujenzi wa maghala sita (6) katika skimu sita (6) za umwagiliaji katika wilaya za Kilombero, Korogwe, Bagamoyo, Mbarali, Mvomero na Arumeru ambapo ujenzi wa ghalia la Lekitatu (Arumeru) umekamilika; ujenzi wa maghala mengine upo katika hatua mbalimbali; kuajiri Mshauri elekezi na kuanza usanifu kwa kwa ajili ya ujenzi wa skimu nne (4) za mfano za Mkindo, Mkula, Msolwa - Ujamaa na Tulo-kongwa; na kupatikana kwa watoa huduma binafsi kwa ajili ya skimu nne (4) za umwagiliaji, hivyo kuongeza idadi ya skimu zenyenye watoa huduma binafsi kufikia 34 na kunufaisha wakulima 4,554.

(c) Kilimo cha Mahindi

Ujenzi wa maghala mapya mawili (2) katika Wilaya ya Mlele na Nsimbo umekamilika ikilinganishwa na lengo la kujenga maghala 10; kukamilika kwa ukarabati wa maghala 36 ikilinganishwa na lengo la maghala 55 katika Wilaya za Iringa, Njombe na Songea; na kupatikana kwa Mtaalam Elekezi wa kujenga mfumo wa kanzidata ya COWABAMA kwa ajili ya kurahisisha uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko kwa wadau.

(d) Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhi Chakula

Kukamilika kwa ujenzi wa ghalia moja kati ya maghala mawili (2) lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 za nafaka katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea na ujenzi wa ghalia katika halmashauri ya wilaya ya Mbozi umefikia asilimia 50.

(e) Tafiti za Kilimo

- (i) Kukamilika kwa ukarabati wa ofisi 4, ujenzi wa barabara na miundombinu ya umwagiliaji katika kituo cha Kilimo cha Mpunga cha KATRIN (Kilombero) na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 10 za mafunzo kwa vitendo katika kituo cha Ukiliguru;
- (ii) Kugundua na kuidhinisha aina 29 za mbegu bora kwa mazao ya

- mahindi, mpunga, karanga, chai na alizeti;
- (iii) Kuzalisha tani 8.2 za mbegu mama na tani 522 za mbegu za awali za mazao mbalimbali; na
- (iv) Kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu ya umeme katika kituo cha utafiti cha KATRIN.

B. **Mifugo**

(a) **Miundombinu ya Maji na Malisho**

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: Kuainishwa kwa maeneo yatakayochimbwa mabwawa kwa ajili ya kunywesha mifugo katika wilaya tatu (3) za Handeni (Msomera), Chemba (Pangalua) na Ngorongoro (Masisu) ambapo ujenzi wa mabwawa mawili (2) katika eneo la Masisu (Ngorongoro) na Olypasei (Kiteto) umekamilika; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya Kwamaligwa (Kilindi) na Mbangala (Chunya) unaendelea; na kuainisha na kutenga maeneo ya ufugaji yenze jumla ya hekta 64,070.18 na hivyo kuongeza maeneo ya ufugaji kufikia hekta milioni 2.02 kwa ajili ya malisho.

(b) **Vituo vya Uhamilishaji**

Hatua ya utekelezaji ni pamoja na: Ununuzi wa vifaa vya uhamilishaji ikiwemo mitungi 9 kwa ajili ya kituo cha *Sao Hill*; Kituo Cha Taifa Cha Uhamilishaji kimetoa mafunzo kwa wahimilishaji 38; kuzalishwa kwa dozi 80 za mbegu bora za uhamilishaji ambazo zilisambazwa na kuhamilisha ng'ombe 221,390 na kukamilisha ujenzi wa kituo cha uhamilishaji cha Katavi na ununuzi wa mashine ya LN2.

(c) **Ujenzi wa Minada na Masoko**

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: Ukarabati wa minada ya upili ya Pugu (Ilala), Lumecha (Songea), Kirumi (Butiama); Nyamatala (Misungwi); Kizota (Dodoma); na Kasesya (Sumbawanga); kukamilika kwa barabara ya kuzunguka mnada wa upili wa Kizota (Dodoma); kukamilika kwa ujenzi wa kisima katika mnada wa Pugu; na kukamilika kwa ujenzi wa ofisi, mazizi na barabara ya kuingilia mnadani na sehemu ya kunadia mifugo katika mnada wa upili wa Kasesya (Kalambo).

C. **Uvuvii**

(a) **Huduma ya Uzalishaji wa Samaki**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuimarishwa kwa vituo vya Kingolwira (Morogoro), Machui (Tanga), Ruhila (Songea), Mwamapuli (Tabora) na Mtama (Lindi) kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya kuzalisha vifaranga; kuzalisha na

kusambaza vifaranga 500,000 kwa wafugaji wa samaki katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Ruvuma, Lindi na Mtwara; kuimarika kwa uzalishaji wa vifaranga kutoka katika vituo vya sekta binafsi ambapo jumla ya vifaranga milioni 18 vilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wa samaki katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Kilimanjaro, Tanga, Geita, Pwani, Mara na Kagera.

2.3.3 Viwanda

(a) Maeneo Maalum ya Uwekezaji

(i) Bagamoyo SEZ

Serikali kuititia Mamlaka ya Usimamizi wa Maeneo Maalaum ya Uwekezaji na Mamlaka ya Bandari Tanzania iliingia mkataba wa utatu na kampuni za *China Merchant Holding International* (CMHI) ya *China na State General Reserve Fund* (SGRF) ya Oman kuwekeza katika eneo maalum la uwekezaji Bagamoyo katika eneo la hekta 2,500. Kati ya eneo hilo hekta 1,700 ni kwa ajili ya kuanzisha eneo maalum la viwanda na hekta 800 ni kwa ajili ya ujenzi wa bandari. Hatua ya utekelezaji wa mradi iliyofikiwa ni pamoja na kulipa fidia ya shilingi bilioni 26.9 kati ya shilingi bilioni 58.8 zinazohitajika kulipa eneo la hekta 5,743 zilizofanyiwa uthamini mwaka 2008.

(ii) Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini - Dar es Salaam

Ujenzi wa mradi huu utatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania kuititia Mamlaka ya Usimamizi wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji na Serikali ya China kuititia kampuni ya *Yiwu Pan-African International Company*. Mradi utahusisha ujenzi wa kituo cha kisasa cha biashara na huduma kwa ajili ya bidhaa kutoka China. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ulipaji wa fidia ya shilingi bilioni 3.04 na hivyo kufanya jumla ya fidia yote iliyolipwa katika eneo hilo la hekta 60.4 kufikia bilioni 101.04.

(b) Mradi wa Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga

Ukarabati wa barabara ya Mkiu – Liganga (km 46), Mchuchuma (Mchuchuma access road km 7) umekamilika; Itoni (Njombe – Ludewa – Nkomang’ombe km 168.5) na Mchuchuma - Liganga kwa kiwango cha changarawe; kuanza uthamini wa mali za wananchi watakaopisha eneo la mradi Mchuchuma na Liganga lenye kilomita za mraba 151 na Liganga kilomita za mraba 179 mwaka 2015, na kuendelea na mazungumzo kati ya wawekezaji (*Tanzania – China Mineral Resources Limited*) na TANESCO juu ya mkataba wa kuuziana umeme utakaozalishwa Mchuchuma wa MW 600.

(c) Kiwanda cha Viuadudu Kibaha, Pwani

Kukamilika kwa ujenzi na ufungaji wa mitambo ambapo kiwanda kilizinduliwa Julai 2015; kukamilika kwa ujenzi wa barabara za kuingia kiwandani kwa kiwango cha lami (mita 400); kuanza ujenzi wa bwawa la kusafisha maji taka (*oxidation pond*); kuanza maandalizi ya kujenga kituo kidogo cha umeme (*power substation*); na kuanza maandalizi ya tafiti kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha mbolea (*Bio-Fertilizer*).

2.3.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu

A. Maendeleo ya Ujuzi Maalum

Kutoa mafunzo katika fani za mafuta na gesi kwa ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa wanafunzi 159. Kati ya wanafunzi hao, 124 wanagharamiwa na Serikali na wanafunzi 35 wanagharamiwa na nchi wahisani.

B. Elimu na Mafunzo ya Ufundu

(a) Vyuvo Vikuu

Katika mwaka 2015/16 mikopo na ruzuku kiasi cha shilingi bilioni 467.43 imetolewa kwa wanafunzi 124,243 wa elimu ya juu ikilinganishwa na lengo la wanafunzi 101,129 ambapo shilingi bilioni 5.514 ni ruzuku kwa wanafunzi 1,957 katika mafunzo ya masomo ya udaktari wa binadamu. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.596 bakaa ya mwaka 2014/15 na shilingi bilioni 27.024 ni makusanyo ya mikopo. Aidha, Bodi pia ilitoa mikopo kwa wanafunzi 7,996 wa Diploma ya Ualimu wa Hisabati na Sayansi na wanafunzi 270 wa mafunzo ya sheria; na kuendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 9 la hospitali ya kufundishia katika Kampasi ya Mloganzila ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Kampasi hii ikikamilika itaongeza udahili wa wanafunzi katika kada ya afya kutoka wanafunzi 3,100 hadi wanafunzi 15,000 kwa mwaka.



Ujenzi wa jengo la hospitali ya kufundishia ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Dar es Salaam - Kampasi ya Mlonganzila ukiendelea, Februari 2016

(b) Elimu ya Msingi na Sekondari

(i) Miundombinu ya Sekondari

Ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya madarasa, vyoo, maabara na nyumba za walimu katika shule za sekondari 264 umekamilika; upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya madarasa, vyoo, maabara na nyumba za walimu katika shule za Serikali 528 pia umekamilika.

(ii) Kiongozi cha Mwalimu

Kitabu cha Kiongozi cha Mwalimu cha kuimarisha utendaji wa shule za Msingi na Sekondari kimeandaliwa, kuchapishwa na kusambazwa katika shule zote za Msingi na Sekondari. Aidha, mafunzo ya uongozi yalitolewa kwa Wakuu wa Shule zote za Msingi na Sekondari ili kuimarisha utendaji kazi wao.

(iii) Tathmini ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK)

Imeandaliwa miongozo mbalimbali ya kusaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK kwa kuzingatia matokeo ya upimaji wa stadi za KKK kitaifa uliofanyika mwaka 2013. Jumla ya walimu 24,237 wa shule za msingi wanaofundisha darasa la I & II

wamepatiwa mafunzo juu ya ufundishaji wa stadi za KKK.

(iv) Kuwajengea Uwezo Walimu wa Sayansi na Sanaa

Walimu 33,322 wakiwemo 20,200 wa shule za msingi na 13,122 wa shule za sekondari wamepatiwa mafunzo kazini kuitia program ya kujenga uwezo wa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji.

(v) Ruzuku ya Uendeshaji wa shule

Ruzuku ya uendeshaji wa shule imeendelea kutolewa kila mwaka, Kuanzia Januari 2016, kiasi cha shilingi bilioni 18.77 kimekuwa kikitolewa na Serikali kila mwezi ambapo shilingi bilioni 15.71 zimekuwa zikipelekwa shule za Msingi na Sekondari moja kwa moja na shilingi bilioni 3.06 zimekuwa zikipelekwa NECTA kama fidia ya Ada ya Mitihani ya Kidato cha Nne.

(c) Elimu ya Mafunzo ya Ufundi (TVET)

- (i) Programu ya Mafunzo Jumuishi ya Kuhamasisha Ujasiliamali (*Integrated Training for Entrepreneurship Promotion*) imeanzishwa na kuwafikia watu 3,481 waliopo katika mfumo usio rasmi;
- (ii) Ujenzi wa chuo cha mafunzo ya ufundi cha Wilaya ya Makete umekamilika na chuo kimeanza kudahili wanafunzi katika fani 4;
- (iii) Kuanzishwa kwa programu mpya 8 katika Chuo cha Ufundi Arusha na kuwezesha kuongezeka kwa programu za mafunzo hadi 14. Programu hizo ni: Sayansi na Teknolojia ya Maabara, Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji, teknolojia ya Umeme wa Magari, Teknolojia ya Madini na Vito, Uhandisi wa vifaa Tiba na Teknolojia ya Mawasiliano;
- (iv) Programu mpya za Uhandisi wa vifaa Tiba na Teknolojia ya Mawasiliano zimeanzishwa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT);
- (v) Watumishi 527 (Wanataaluma 269) wa Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Elimu ya Ufundi wamepata mafunzo ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujenga uwezo wa utendaji kazi;
- (vi) Mafunzo maalum ya mfumo wa *Complementary Basic Education Training - CBET* yametolewa kwa walimu 100, wakuu wa vyuo na waratibu kwa ajili ya vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi pamoja na kuandaa mitaala ya mfumo wa CBET na kusambazwa katika vyuo hivyo 25.

C. Afya na Ustawi wa Jamii

Hospitali ya Taifa Muhimbili: kuendelea na ujenzi wa jengo la dharura kwa watoto na ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya Kituo cha Tiba na Mafunzo ya Upasuaji wa Moyo na kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kibingwa;

- (a) **Taasisi ya Mifupa Muhimbili:** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la ghorofa 7 litakalokuwa na sehemu za kutolea huduma pamoja na malazi kwa wagonjwa. Hadi sasa sehemu ya jengo hilo limeanza kutumika kwa ajili ya malazi ya wagonjwa. Sehemu ya kutolea matibabu itaanza kutumika baada ya kununuliwa vifaa tiba;
- (b) **Taasisi ya Saratani Ocean Road:** ununuzi wa vifaa na kuanza ujenzi wa vyumba maalum (bunkers) kwa ajili ya kusimika mashine za kisasa kwa ajili ya kutolea tiba ya mionzi unaendelea ambapo sifa za kiufundi za mashine (*specifications*) ya LINAC zimeandaliwa na kupitishwa;
- (c) **Hospitali za Rufaa za Kikanda:** Kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa kanda ya kati iliyopo Singida; kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la tiba ya mionzi katika Hospitali ya Bugando na ununuzi wa vifaa tiba ikiwemo *CT Simulator*; ukarabati wa wodi 6 katika hospitali ya Kibong'oto; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la *X-rays* katika hospitali ya rufaa ya Mbeya; na kuanza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje la hospitali ya Kanda ya Kusini – Mtwara;
- (d) **Hospitali ya Kisasa ya Benjamin Mkapa Ultra Modern Hospital Dodoma:** Kukamilika kwa ujenzi wa hospitali kwa ajili ya kutoa huduma za kibingwa za uchunguzi na tiba ya magonjwa. Hospitali itatumika kwa tafiti na mafunzo kwa wanafunzi wa afya wanaosoma katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Aidha, ujenzi wa majengo mengine ya kutolea huduma na wadi ya kulaza wagonjwa umefikia asilimia 50;
- (e) Jumla ya zahanati 77, vituo vya afya 33 na hospitali za wilaya 7 zimefanyiwa ukarabati, upanuzi na ujenzi, kuweka vifaa tiba na samani;
- (f) Wafanyakazi wa sekta ya afya 3,260 katika mikoa ya Mara, Mtwara na Tabora wamepatiwa mafunzo katika stadi za afya zaidi ya lengo la kutoa mafunzo kwa wafanyakazi 2,830;
- (g) Kukamilika kwa ujenzi wa maghala ya kuhifadhia dawa yenyе ukubwa wa mita za mraba 10,209 katika mikoa ya Mbeya, Dar es Salaam, Dodoma, Tabora na Tanga;
- (h) Ujenzi wa jengo la madarasa, ukarabati wa maabara ya kujifunzia kwa vitendo, bwalo la chakula na miundombinu ya majitaka katika chuo cha Tabibu Musoma umekamilika kwa asilimia 85; na
- (i) Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la utawala, ukumbi wa mikutano, madarasa, mabweni, maktaba, maabara, nyumba za watumishi na

ujenzi wa uzio katika chuo cha Utabibu Mpanda.

2.3.5 Huduma za Utalii, Biashara na Fedha

A. Utalii

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji mapato ambapo Idara za Utalii na Wanyamapori zimeunganishwa katika mfumo huu kwa awamu ya kwanza; Hadidu za rejea za kumpata Mtaalamu Elekezi wa kupitia Sera ya Taifa ya Utalii zimeandaliwa pamoja na Mpango kazi wa utekelezaji; na kukamilika kwa Kanuni ya Waongoza Misafara ya watalii iliyosainiwa Julai, 2015. Aidha, Idadi ya watalii kutoka nje ilipungua kwa asilimia 8 kutoka watalii 1,140,156 mwaka 2014 hadi watalii 1,048,944 na mapato kutokana na watalii yalipungua hadi Dola za Marekani bilioni 1.9 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani bilioni 2 zilizopatikana mwaka 2014.

B. Biashara na Masoko

Sheria ya Soko la Mazao na Bidhaa (*Commodity Exchange*) ilipitishwa na Bunge Juni 2015; kupatikana kwa ofisi pamoja na Jukwaa la mauzo kwa ajili ya Soko la Mazao na bidhaa katika Jengo la LAPF lililopo Kijitonyama - Kinondoni mkoa wa Dar - es – Salaam; kutolewa mafunzo kwa wasimamizi watunga Sera, baadhi ya Wakurugenzi wa Serikali, Sekta Binafsi na madalali wa soko (*Marketing intermediaries*) kwa lengo la kurahisisha uendeshaji wa soko hilo. Aidha, mshauri Elekezi anaandaa Mpango Biashara (*Bussiness Plan*) na kubainisha mapungufu yaliyopo kati ya mfumo wa stakabadhi za ghala na Soko la mazao na bidhaa ili yaweze kupatiwa ufumbuzi. Vile vile, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ambapo usajili wa majina ya biashara unafanyika kwa njia ya mtandao wa kompyuta (online application and registration) uliozinduliwa Oktoba, 2015; Mtaalamu Elekezi anaendelea kuandaa Dirisha la Taarifa za Biashara (National *Business Portal-NBP*) ambalo litakuwa na taarifa zote muhimu zinazohusu taratibu, sheria, kanuni, adhabu, masharti yanayotakiwa kutimizwa wakati wa kuomba kuanzisha biashara hapa nchini; na kuendeleza miundombinu ya masoko ya mikoa na kuanzisha masoko katika vituo vya mipakani ili kukuza biashara ya ndani na kikanda.

C. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

Kukamilika kwa vituo vya utoaji huduma kwa pamoja mpakani vya Holili/Taveta (Tanzania na Kenya) na Rusumo (Tanzania na Rwanda). Aidha, ujenzi unaendelea katika kituo cha Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi). Vilevile, usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia) umekamilika ambapo ujenzi utagharamiwa na

TradeMark East Africa na ujenzi wa kituo cha Songwe/Kasumulu (Tanzania na Malawi) upo katika hatua ya usanifu wa kina. Pia, Serikali imeendelea na ukarabati wa jengo la ghorofa 9, makazi ya Balozi na Mkuu wa utawala katika ubalozi wa Tanzania Maputo - Msumbiji.

D. Huduma za Fedha

Benki ya Rasilimali Tanzania

Benki imeongeza mtaji kufikia shilingi bilioni 152 na kupata leseni ya kuwa Taasisi ya Fedha ya Maendeleo. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na utoaji wa mikopo ya shilingi bilioni 550 kwenye sekta mbalimbali zikiwemo wajasiriamali wadogo, viwanda, makampuni binafsi na wachimbaji wadogo. Aidha, shilingi billioni 58.8 zilitolewa kwa makampuni 121 kupitia dirisha la kilimo na kuwafikia wananchi 1,000 kupitia *out-grower system* na SACCOS 78 ambazo zimewfikia wananchi 4,000. Katika eneo la wachimbaji wadogo benki ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 8 ambazo zilitolewa kwa vikundi 17.

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania

Hadi sasa, Serikali imetoa mtaji wa shilingi bilioni 60 kwa ajili ya benki hii. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kutoa mafunzo kwa vikundi vya wakulima 89 vyenye wakulima 21,526 mkoa wa Iringa. Aidha, benki imebuni bidhaa mbalimbali za mikopo zitakazokidhi mahitaji ya uzalishaji ikiwemo mikopo ya muda mfupi ya hadi miezi 24 yenye riba ya asilimia 8, muda wa kati wa hadi miezi 60 yenye riba ya asilimia 10 na muda mrefu hadi miezi 180 yenye riba ya asilimia 12.

Benki ya Wanawake Tanzania

Mtaji wa Benki ya Wanawake Tanzania umefikia bilioni 20 mwaka 2015. Benki ya Wanawake Tanzania imefungua vituo vya kutolea mafunzo na mikopo katika Mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Njombe. Benki hiyo imetoa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo kwa wananchi 12,874 wakiwemo wanawake 9,693 (1,485 wanawake wa vijijini) na wanaume 3,181. Mikopo ya masharti nafuu iliyotolewa ni shilingi bilioni 20.1. Kati yao, wanawake walipata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 12.8 na wanaume shilingi bilioni 7.2.

D. Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Katika Ukanda wa Pwani na Zanzibar: Kazi zilizotekelawa ni pamoja na: kuwezesha vikundi 27 katika Wilaya ya Rufiji kupanda hekta 1,000 za mikoko; kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ukarabati na uimarishaji wa kuta za kingo za bahari za

barabara ya Barack Obama na Kigamboni; kuajiri Wataalam Elekezi wa kuboresha matumbawe na upandaji wa mikoko katika fukwe za Dar es Salaam; na kuratibu utekelezaji wa mradi wa kujenga uwezo wa jamii za pwani ya bahari ya Hindi ili kuhimili mabadiliko ya tabianchi kutokana na kuongezeka kwa usawa wa bahari kupitia mafunzo kuhusu upandaji na usimamizi endelevu wa mikoko yalitolewa kwa wananchi wa maeneo ya Rufiji, Pangani na Zanzibar.

Mkataba wa Stockholm wa kudhibiti kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu: Kazi zilizotekelizwa ni: kukamilika kwa mapitio ya Mpango wa Taifa wa utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm; kutoa elimu na mbinu bora za usimamizi wa viwanda na wajasiriamali; kuandaa mikakati na mipango kazi ya kusimamia mkataba; na kutoa mapendekezo ya njia bora za kudhibiti uzalishaji kemikali na matumizi yake ikiwemo njia bora ya kudhibiti taka za plastiki ambazo zinachangia kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa kemikali.

E. Utawala Bora

- i. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliendelea na ukamilishaji wa jengo la ofisi ya kanda ya Mtwara na ununuzi wa maeneo ya kujenga ofisi za kanda katika mikoa ya Mwanza na Dodoma.
- ii. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iliendelea na usajili na utambuzi wa watu katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, na Lindi. Kazi zilizotekelizwa ni: kusajiliwa kwa wananchi 335,627 ambapo kati yao wananchi 6,546 walichukuliwa alama za kibaiolojia na kupigwa picha; ugawaji wa vitambulisho 73,434 katika mikoa ya Dar es Salaam; Pwani pamoja na Zanzibar; kuongezwa kwa watumishi na vitendea kazi katika ofisi za wilaya zote za mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, na Wilaya ya Arusha mjini; kuendelea na ujenzi wa kituo kikuu cha kutunzia kumbukumbu katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha ambapo ujenzi wa msingi umekamilika; na kukamilika kwa uzio na kuanza kwa ujenzi wa msingi wa kituo cha uokozi wakati wa majanga - Morogoro.

2.4 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango

Katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/16, zipo changamoto zifuatazo:

- (a) Uhakika na upatikanaji wa fedha za ulipaji fidia na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- (b) Taratibu ndefu na gharama kubwa za ununuzi wa umma;

- (c) Madeni ya wakandarasi, hususan ya ujenzi wa barabara;
- (d) Urasimu wa upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji;
- (e) Utegemezi wa bajeti ya maendeleo, hususan, misaada na mikopo kutoka nje;
- (f) Ushiriki mdogo wa sekta binafsi;
- (g) Mazingira yasiyo wezeshi kwa uwekezaji na uendeshaji biashara; na
- (h) Uhaba wa miundombinu wezeshi (barabara, maji na umeme) ya kuwezesha utekelezaji wa miradi.

Hata hivyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na hali hiyo, ikiwemo:

- (a) Kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha kugharamia miradi ya maendeleo;
- (b) Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia uwekezaji wa moja kwa moja na ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma;
- (c) Kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuchochea uwekezaji, hususan wa viwanda;
- (d) Kuendelea kuimarisha miundombinu wezeshi katika maeneo ya mradi ya maendeleo; na
- (e) Kuendelea kupunguza madeni ya wakandarasi hususan wa ujenzi wa barabara.

SURA YA TATU

HALI YA VIWANDA

3.1 Historia ya Viwanda Nchini

Kiwanda ni shughuli ya kiuchumi inayofanyika mahali pamoja ili kuongeza thamani kwenye malighafi kwa njia ya kifizikia na kikemikali na yenye mmiliki au msimamizi mmoja au zaidi kisheria. Malighafi zinazobadilishwa zinatokana na kilimo, misitu, uvuvi pamoja na bidhaa zingine (*intermediate products*) zinazotumika kuzalisha bidhaa zenye thamani zaidi viwandani. Mfano; utengenezaji wa samani, ushonaji, na usindikaji wa vyakula.

Kwa nchi yoyote Duniani ambayo uchumi wake unaendelea kukua ni dhahiri kuwa sekta ya viwanda inakua kwa kasi inayoridhisha. Kabla na baada ya Tanzania kupata uhuru mwaka 1961 idadi ya viwanda nchini ilikuwa na ongezeko kubwa la idadi ya viwanda nchini kati ya mwaka 2005 na mwaka 2013 lililotokana na mikakati mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ikijumuisha mfuko wa uwezeshaji wa "Mabilioni ya JK" na utekelezaji wa sera ya uendelezaji wa viwanda vidogo kupitia SIDO. Ongezeko hili lilitokea katika viwanda vidogo vinavyoajiri wafanyakazi 1 hadi 4. **Jedwali Na. 3.1** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa viwanda nchini.

Jedwali Na. 3.1: Idadi ya Viwanda Nchini

| Kipindi | Kabla ya Uhuru | 1961-1970 | 1971-1980 | 1981-1990 | 1991-1995 | 1996-2000 | 2001-2005 | 2006-2010 | 2011-2013 |
|------------------|----------------|-----------|-----------|-----------|-----------|-----------|-----------|-----------|-----------|
| Idadi ya Viwanda | 61 | 64 | 411 | 1,188 | 1,176 | 3,430 | 5,153 | 12,849 | 50,656 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Taktamu, 2016

Tanzania ikiwa mionganii mwa nchi nyingine za Afrika, maendeleo katika sekta ya viwanda yamekuwa katika vipindi mbalimbali. Kabla ya azimio la Arusha mwaka 1967, sekta ya viwanda iliendelezwa na sekta binafsi na Serikali. Katika kipindi hicho kulikuwa na viwanda 125 ambavyo vingi vilikuwa ni vya kutumia nguvu kazi kubwa (*labour intensive*) na vilitoa ajira 200,000 na mchango wa wastani wa asilimia 4 katika Pato la Taifa. Baadhi ya viwanda hivyo ni pamoja na *Coca-Cola*, *East African Breweries*, *Tanganyika Packers*, *British American Tobacco*, *Metal Box* na kiwanda cha viatu Bata ambavyo vyote hivyo vilikuwa vinamilikiwa na sekta binafsi. Baada ya Azimio la Arusha 1967 nchi ilianza kutumia mfumo wa uchumi wa siasa ya ujamaa na kujitegemea ambapo shughuli zote za kiuchumi zilimilikiwa na kuendeshwa na Serikali ikiwemo viwanda. Msisitizo ulikuwa kuendeleza viwanda kwa ajili ya kuzalisha bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nje (*import substitution*) na viwanda vya

kuchakata mazao ya kilimo kwa ajili ya kuza nje ya nchi sambamba na kuwa na sera ya kudhibiti biashara.

Katika kipindi cha mwaka 1967 hadi 1985 Serikali ilichukua umiliki wa viwanda na mashirika ikiwa ni pamoja na kusimamia uendeshaji na uzalishaji, kudhibiti uagizaji wa bidhaa, udhibiti wa bei na soko la fedha za kigeni. Kutokana na udhibiti wa soko la fedha za kigeni pamoja na mauzo hafifu ya bidhaa na huduma nje ya nchi, upungufu wa fedha za kigeni nchini ulijitokeza hivyo kuzorotesha uagizaji wa bidhaa muhimu. Kuongezeka sana kwa bei za mafuta duniani (*the global oil crisis*) mwaka 1973 kuliongeza upungufu wa fedha za kigeni. Hali hii ilisabisha kushuka kwa kiwango kikubwa uzalishaji viwandani na kupunguza ukuaji wa uchumi. Aidha, kutokana na mageuzi ya kiuchumi ya Dunia (1986-1995) Serikali ilibinafsisha viwanda na mashirika ya Umma ili kuendana na dhana mpya ya soko huria na kupunguza mzigo wa uendeshaji kwa Serikali.

3.2 Mwenendo wa Sekta ya Viwanda

Sekta ya viwanda imeendelea kuwa tegemeo kubwa la ajira na mauzo ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, ukuaji wa sekta ya viwanda umekuwa wa kuridhisha licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali. Sekta hii ilikua kutoka wastani wa asilimia 9.6 mwaka 2005 hadi asilimia 11.5 mwaka 2007 kabla ya kupungua hadi asilimia 4.7 mwaka 2009 kutokana na madhara ya m dororo wa uchumi wa dunia uliosababishwa na kuporomoka kwa masoko ya fedha duniani. Hata hivyo, imeendelea kuimarika taratibu na kufikia ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2014 na kupungua kidogo kufikia asilimia 6.0 mwaka 2015. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa viwanda na uzalishaji wa bidhaa za viwandani zikiwemo nguo, chuma, saruji, vinywaji, sigara, vifaa vya ujenzi na bidhaa nyingine za kilimo na mifugo. Aidha, katika kipindi hicho wastani wa mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.0. **Jedwali Na. 3.2** linaonesha mwenendo wa ukuaji na mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa kwa kipindi cha mwongo mmoja.

Jedwali Na. 3.2: Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa (2005 – 2015)

| | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 ¹ |
|--|------|------|------|------|------|------|------|------|------|------|-------------------|
| Ukuaji wa Sekta ya Viwanda (Asilimia) | 9.6 | 8.4 | 11.5 | 11.4 | 4.7 | 8.9 | 6.9 | 4.1 | 6.5 | 6.8 | 6.0 |
| Mchango wa Viwanda katika Pato la Taifa (Asilimia) | 7.3 | 7.5 | 7.0 | 7.0 | 6.9 | 6.9 | 7.6 | 7.5 | 6.4 | 5.6 | 4.2 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2016

¹ Takwimu za awali za Pato la Taifa

3.3 Hali ya Viwanda Nchini

Kwa mujibu wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013, Tanzania ina jumla ya viwanda 50,656 ambavyo vipo katika mikoa mbalimbali nchini. Viwanda hivyo vinajumuisha viwanda vya kati na vikubwa 1,769 sawa na asilimia 3.5 ambavyo vinaajiri wafanyakazi 10 na kuendelea, na viwanda vidogo 48,887 sawa na asilimia 96.5 ambavyo vinaajiri wafanyakazi 1 hadi 9. Takriban ajira 231,176 zimetengenezwa kutokana na viwanda hapa nchini, ambapo viwanda vikubwa na vya kati vimetoa ajira 107,732 na viwanda vidogo ajira 123,364. Aidha, viwanda vinavyoajiri wafanyakazi 10 na kuendelea mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kuwa na idadi kubwa ya viwanda 516 (asilimia 29.2) ikifuatia Arusha 144 (asilimia 8.1), Shinyanga 101 (asilimia 5.7), Kilimanjaro 96 (asilimia 5.4) na Mwanza 88 (asilimi 5.0). Vile vile, aina ya viwanda vingi vilivyopo nchini ni vya uzalishaji chakula 20,228 (asilimia 39.9) ikifuatia na mavazi (kanga na vitenge) 13,758 (asilimia 27.2) na samani 7,071 (asilimia 14.0). Hata hivyo, zipo fursa zaidi katika viwanda vingine ambayo havifanyi vizuri kama vile nguo 817 (asilimia 1.6), TEHAMA 3 (asilimia 0), mashine na vifaa 30 (asilimia 0.1), madawa 9 (asilimia 0), ngozi 216 (asilimia 0.4), kemikali 102 (asilimia 0.2) na vifaa vya umeme 269 (asilimia 0.5).

3.4 Ubinafsishaji wa Viwanda

3.4.1 Utekelezaji wa Mpango wa Ubinafsishaji

Serikali ilianza kutekeleza Mpango wa Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma mwaka 1992. Lengo la ubinafsishaji lilikuwa ni kushirikisha sekta binafsi na wananchi walio wengi kumiliki, kuendesha na kuwekeza katika mashirika ya umma ambayo utendaji wake ulianza kulegalega kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukosefu wa mitaji na kukosa usimamizi makini wa mashirika hayo.

Katika kutekeleza mpango huo, Serikali iliunda Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma mwaka 1993. Ubinafsishwaji ulifanywa kwa njia mbalimbali kama vile Uuzaji wa Mali, Uuzaji wa Hisa, Ubia, Ukokishaji, Uuzaji wa Shirika kwa menejimenti na Wafanyakazi pamoja na Ufilisi. Tofauti za njia za ubinafsishaji zilitokana na utendaji na hali halisi ya Shirika wakati wa ubinafsishaji. Tangu mpango wa ubinafsishaji uanze kutekelezwa mwaka 1993 hadi sasa jumla ya mashirika 337 yamebinafsishwa. Kwa sasa majukumu hayo yako chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina baada ya Shirika Hodhi la Mali za Serikali (*Consolidated Holdings Corporation*) kumaliza muda wake mwaka 2013.

Matarajio ya Serikali katika ubinafsishaji yalikuwa kama ifuatavyo:

- i. Kuongeza ufanisi katika Sekta ya mashirika ya Umma na uzalishaji mali;
- ii. Kuongeza mapato ya Serikali na hivyo kuboresha uwiano wa mapato na matumizi;
- iii. Kupunguza/kuondoa nafasi ya Serikali katika uendeshaji wa shughuli za kibiashara ili kuiwezesha kutoa huduma za msingi kwa jamii, ujenzi na uendelezaji wa miundombinu, kuhakikisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao, usimamizi wa sheria na utawala bora;
- iv. Kushirikisha sekta binafsi katika maendeleo ya uchumi wa nchi hususan katika maeneo ambayo Serikali imeamua kujitoa;
- v. Kuongeza ajira;
- vi. Kupunguza utegemezi wa Mashirika ya Umma kwa Serikali kupitia ruzuku na mitaji mipya; na
- vii. Kuongeza mitaji na kuanzisha teknolojia ya kisasa katika uzalishaji mali na usambazaji huduma.

3.4.2 Viwanda Vilivyobinafsishwa

Katika kukidhi mahitaji ya soko huria na ushindani wa kibiashara viwanda 106 vilibinafsishwa kwa watanzania na wawekezaji kutoka nje ya nchi. Kati ya viwanda vilivyobinafsishwa, uzalishaji katika viwanda 34 umekuwa wa ufanisi na hivyo kuongeza ajira na mapato ya kodi kwa Serikali. Aidha, viwanda 33 vinaendeshwa kwa hasara. Viwanda 39 vilivyokuwa vinazalisha bidhaa mbalimbali kama vile ngozi, chuma, korosho, zana za kilimo, sabuni na mafuta ya kupika vimefungwa kabisa kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo za kiutendaji, mitaji, teknolojia, nishati, malighafi na kutozingatiwa kwa mikataba ya mauzo.

3.4.3 Hali ya Viwanda Baada ya Kubinafsishwa

(a) Viwanda Vilivyobinafsishwa Vinavyofanya Kazi kwa Faida

Kati ya viwanda vilivyobinafsishwa, viwanda 34 vinafanya kazi iliyokusudiwa kwa faida ikiwemo kiwanda cha *Tanzania Portland Cement Company, Minjingu Phosphate Company Ltd, Metalbox Tanzania Limited, Kibo Paper Industries Ltd, Auto Mech Limited, Kilombero Sugar Company, Tanga Cement, Mbeya Cement* na *Tanzania Breweries LTD*. Uwekezaji katika viwanda hivyo umechangia kuongezeka kwa mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa pamoja na ajira. Pamoja na mafanikio hayo viwanda hivyo vinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ushindani mkubwa katika soko hususan kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kwa kiwango kidogo cha ushuru hususan saruji, vyakula na bidhaa nyingine za viwandani; na upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa ajili ya uzalishaji viwandani.

(b) Viwanda Vilivyobinafsishwa Vinavyofanya Kazi kwa Hasara

Viwanda 33 vinajиndesha kwa hasara ikiwa ni pamoja na viwanda hivyo kuzalisha chini ya kiwango tarajiwa, baadhi kubadili matumizi ya viwanda na vingine vinapata hasara kutokana na mabadiliko katika soko. Viwanda hivyo ni pamoja na *Tanzania Concrete Articles Ltd – Mbeya* ambacho kwa sasa kimebadilishwa matumizi na kuwa ghala la kuhifadhi makasha badala ya matumizi ya awali ya uzalishaji wa vifaa vya ujenzi, *na Ubungo Spinning Mill ambacho mwekezaji amebadili matumizi ya kiwanda baada ya kupata ridhaa ya Serikali na kwa sasa kiwanda kinazalisha bidhaa za plastic badala ya uzalishaji wa awali wa nyuzi.* Viwanda vingine vinavyojiendesha kwa hasara ni pamoja na: *Musoma Textile Mills Limited, Keko Pharmaceutical Industries Ltd, Tanzania Pharmaceutical Industries Ltd, Concrete Roof Tile Plant, The Giraffe Extract Company (T), Kiwanda cha Urafiki (Tanzania – China Friendship industries) na Moshi Leather Goods Ltd.* Changamoto kubwa zilizosababisha viwanda hivi kujiendesha kwa hasara ni pamoja na: ushindani katika soko; kubadilishwa matumizi kwa baadhi ya viwanda na kufanywa maghala ya bidhaa; uchakavu wa mitambo ya baadhi ya viwanda; nishati na baadhi ya wawekezaji kuzalisha bidhaa tofauti na zilizokusudiwa awali.

(c) Viwanda Vilivyobinafishwa na Kufungwa

Viwanda vilivyobinafsishwa na kufungwa ni 39 ikijumuisha viwanda vya *CMSC; Tanzania Bag Corporation LTD (Moshi); Kisarawe Brick Manufactures Ltd; Mbeya Ceramics Company Ltd; Steel Rolling Mills; Tanganyika Packers Ltd, (Shinyanga Meat Plant); Ubungo Garmets Ltd; Tanzania - China Friendship Textile Mills; na Arusha Metal Industries Ltd.* Changamoto kubwa zilizovikabili viwanda hivi na kusababisha kufungwa ni pamoja na: ufinyu wa mitaji; uchakavu wa mitambo na kung'olewa kwa baadhi ya mitambo ya viwanda; upatikanaji wa nishati; na uwekezaji hafifu katika majengo na mashine za viwanda; na baadhi ya wawekezaji kuvitumia viwanda kama dhamana ya mikopo katika mabenki na kutumia fedha za mikopo kwa matumizi mengine tofauti na viwanda.

3.4.4 Changamoto Zilizojitokeza baada ya Ubinafsishaji wa Viwanda

Changamoto kubwa zinazovikabili viwanda vilivyobinafishwa ni:

- (i) Baadhi ya mikataba ya uwekezaji kutoonesha mipango ya uwekezaji wa viwanda;
- (ii) Kubadilishwa malengo ya baadhi ya viwanda na kuzalisha bidhaa tofauti na zilizokusudiwa awali au kutumika kama maghala ya kuhifadhi bidhaa;

- (iii) Baadhi ya viwanda kushindwa kutekeleza Mpango wa Kibiashara (*Business Plan*) uliokubalika wakati wa mauziano;
- (iv) Uchakavu wa mitambo na teknolojia duni kwa baadhi ya viwanda;
- (v) Baadhi ya wawekezaji kutoendeleza kwa makusudi viwanda walivyobinafsishwa;
- (vi) Baadhi ya mitambo ya viwanda imeng'olewa na kuuzwa kama vyuma chakavu;
- (vii) Baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa kutumika kama dhamana ya kupata mikopo ya benki, mikopo ambayo ilitumika kugharamia shughuli nyingine; na
- (viii) Upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa ajili ya uzalishaji viwandani;

3.5 Mikakati ya Kuendeleza Viwanda Nchini

3.5.1 Viwanda Vikubwa

- (i) Kuendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini ili kuinua nafasi ya Tanzania katika ushindani wa kibiashara;
- (ii) Upatikanaji wa Ardhi: Serikali itaendelea kulipa fidia kwa maeneo maalum ya uwekezaji yaliyotengwa nchini na kuweka miundombinu wezeshi itakayovutia Sekta Binafsi kuwekeza. Aidha, maeneo ya viwanda kulingana na mipango miji yataendelea kutengwa kuititia TAMISEMI kwa ajili ya viwanda katika mfumo wa vijiji vya viwanda (*industrial village*), Makongano ya viwanda (*industrial clusters*) na *Industrial parks*;
- (iii) Upatikanaji wa rasilimali fedha: Serikali kuititia Benki ya Rasilimali Tanzania inatekeleza mpango wa kuiongezea benki mtaji kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- (iv) Kuendelea kuboresha miundombinu ya msingi kuwezesha maendeleo ya viwanda nchini hususan, miradi ya nishati ya umeme, maji, barabara, reli na bandari.

3.5.2 Viwanda Vidogo

- (i) Kuendeleza miundombinu ya SIDO;
- (ii) Kuendelea kuboresha miundombinu ya msingi kuwezesha maendeleo ya viwanda nchini hususan, miradi ya nishati ya umeme, barabara, reli na maji;
- (iii) Kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini ikiwa ni pamoja na kodi mbalimbali zilizo kikwazo kwa wajasiriamali wadogo wadogo;
- (iv) Kuwezesha upatikanaji wa Teknolojia rahisi na nafuu hususan kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati kwa ajili ya kuchochea uanzishaji wa viwanda vikubwa;

- (v) Kuanzisha dirisha katika Benki ya Rasilimali lenye lengo la kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa viwanda;
- (vi) Kuanzisha kongane za viwanda (*Industrial Clusters*) za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na ya misitu;
- (vii) Kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi kupitia elimu na mafunzo ya kuendesha na kuendeleza viwanda, ujasiriamali na uwekezaji; na
- (viii) Kuongeza mtaji zaidi kwenye mfuko wa Taifa wa kuendeleza ujasiriamali (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF) pamoja na mfuko wa dhamana kwa wajasiriamali (*SME Credit Guarantee Scheme*) kuwezesha kuwafikia walengwa wengi zaidi.

3.5.3 Viwanda Vilivyobinafsishwa

- (i) Kutathmini kwa kina viwanda vyote vilivyobinafsishwa ili kuandaa mikakati ya kuviendeleza;
- (ii) Kupitia mikataba yote ya ubinafsishaji na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria;
- (iii) Kufufua viwanda vilivyobinafsishwa na kuviendeleza kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; na
- (iv) Kudhibiti uagizwaji wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyta hapa nchini.

Takwimu zaidi za hali ya viwanda nchini zipo katika kitabu cha Mpango **Kiambatisho I - IV**.

SURA YA NNE

VIPAUMBELE VYA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17

4.1 Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

(a) Mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka, Arusha

Mradi wa uchimbaji Magadi Soda unatekelezwa na Shirika la Maendeleo la Taifa - NDC katika bonde la Engaruka, Wilaya ya Monduli (Arusha). Utafiti katika eneo hili umebaini uwepo wa Magadi Soda mita za ujazo bilioni 4.68 na huongezeka kila mwaka kwa kiasi cha mita za ujazo milioni 1.9. Mradi utahusisha ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha magadi soda tani milioni moja kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya viwanda hususan vya madawa, vioo na sabuni. Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 1.7 fedha za ndani kwa ajili ya utafiti wa teknolojia na uchumi (*Techno-Economic study*); utafiti wa kina wa athari za kimazingira; tathmni ya ardhi na mali kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi, kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi na kuanza kulipa fidia. Mradi utakapokamilika utaliingizia Taifa wastani wa mapato ya shilingi bilioni 400 kwa mwaka.

(b) Mradi wa kufufua Kiwanda cha General Tyre - Arusha

Kiwanda cha General Tyre Arusha kilianzishwa mwaka 1970 kwa ajili ya kuzalisha matairi kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali za kiuendeshaji, mtaji na soko, uzalishaji wa matairi ulisimama kuanzia mwaka 2009. Serikali kwa kuona umuhimu wa kiwanda hicho, iliazimia kukifufua kwa kuanza na ununuzi wa hisa zote (asilimia 100) za kiwanda kutoka kwa mwekezaji kampuni ya *Continental AG* ya Ujeruman. Mradi unalenga kuwezesha kiwanda kuanza uzalishaji. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi milioni 150 fedha za ndani kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa kupata gharama za kufunga mitambo mpya wa kuzalisha matairi na kuanza maandalizi ya zabuni za kupata mbia. Mradi unakusudiwa kutekelezwa kwa ubia kati ya Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa na Sekta Binafsi.

(c) Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO, Kibaha

Eneo la viwanda TAMCO lina ukubwa wa hekta 94 kwa ajili ya uwekezaji katika kuendeleza viwanda. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 9.0 fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa

kituo kidogo cha Umeme; ujenzi wa miundombinu ya msingi kwa ajili ya viwanda ikiwemo mfumo wa maji safi na maji taka, bwawa la maji taka na tanki la maji; na ujenzi wa mtandao wa barabara.

(d) Uendelezaji wa Viwanda Vidogo – SIDO

Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 6.05 kwa ajili ya kuimarisha na kuendeleza maeneo ya viwanda vidogo (*Industrial Estates/Parks*) katika mikoa ya Morogoro, Dar es salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha.

- (i) **Morogoro:** Mradi utatekelezwa katika eneo la viwanda Kihonda kwenye kiwanja namba 79 kinachomilikiwa na SIDO ambacho kina ukubwa wa hekta 6. Shilingi bilioni 2.4 zimetengwa kwa ajili ya: kukamilisha ujenzi wa jengo la kituo cha mafunzo ya kusindika vyakula kwa wajasiriamali wadogo pamoja na ununuzi wa mashine; ujenzi wa ofisi ya SIDO ya mkoa; na ujenzi wa majengo manne (4) kwa ajili ya wajasiriamali wadogo.
- (ii) **Dar es Salaam:** Mradi utatekelezwa katika eneo la viwanda Vingunguti kwenye kiwanja namba 24 - 27 kinachomilikiwa na SIDO ambacho kina ukubwa wa hekta 12.9. Eneo hili lina huduma za msingi za maji, umeme na barabara. Shilingi bilioni 1.1 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la kituo cha mafunzo ya kusindika vyakula pamoja na ununuzi wa mashine; ukarabati wa majengo na kuboresha miundombinu na ujenzi majengo mawili (2) kwa ajili ya wajasiriamali wadogo.
- (iii) **Mbeya:** Mradi utatekelezwa katika eneo la viwanda Mbeya kwenye kiwanja namba 54 kinachomilikiwa na SIDO ambacho kina ukubwa wa hekta 8.44. Eneo hili lina huduma za msingi za maji, umeme na barabara. Shilingi milioni 200 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo na kuboresha miundombinu.
- (iv) **Mwanza:** Mradi utatekelezwa katika eneo la viwanda Nyakato kwenye kiwanja namba 128 kinachomilikiwa na SIDO ambacho kina ukubwa wa hekta 2.7. Eneo hili lina huduma za msingi za maji, umeme na barabara. Shilingi milioni 800 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo 4 ya wajasiriamali wadogo.
- (v) **Arusha:** Mradi utatekelezwa kwenye viwanja namba 42 – 47 na 72-85 (Block E) vinavyomilikiwa na SIDO ambavyo vina ukubwa wa hekta 4.56. Maeneo hayo yana huduma za msingi za maji, umeme na barabara. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na: ukarabati wa karakana; kuboresha miundombinu na kununua mashine mpya za kuzalisha vipuri na mashine zingine.

- (vi) **Mfuko wa Mikopo:** Shilingi bilioni 2.4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali (NEDF) unaotoa mikopo midogo kwa wenyewe viwanda na wafanyabiashara wadogo. Kiasi hiki kitaongeza wigo wa kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wengi zaidi.

4.2 Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Rasilimali Watu

4.2.1 Elimu na Mafunzo ya Ufundu

- (a) **Kuimarisha mifumo, majengo na miundombinu mingine katika shule za awali, msingi na sekondari**

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA): Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 18 fedha za ndani na shilingi bilioni 30 fedha za nje kwa ajili ya kuwezesha ukarabati wa majengo ya shule kongwe 7 za sekondari za Serikali na kuzipatia vifaa vya maabara; kuwezesha ujenzi wa nyumba 30 za walimu wa sekondari katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi; kuwezesha ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum kwa shule za msingi na sekondari; kuwezesha uanzishwaji wa Mifuko ya Elimu ya Wilaya na kugharamia ujenzi wa vyumba 25 vya madarasa na matundu 200 ya vyoo katika shule zenye uhitaji mkubwa kutokana na ongezeko la udahili; kuwezesha uratibu, ufuatiliaji na uendeshaji wa shughuli za Miradi ya Mfuko wa Elimu na Mamlaka ya Elimu Tanzania; na kuwezesha utekelezaji wa mradi wa “*Education and Skills for Productive Jobs*” kwa kuanzisha mfuko wa kujenga ujuzi kwa vijana.

(b) **Ukarabati, Upanuzi na Ujenzi wa Vyuo Vikuu**

- (i) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam:** Mradi unalenga kukarabati na kupanua miundombinu ya chuo ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 9.44 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukarabati hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara, kituo cha polisi cha chuo, nyumba za wahadhiri na miundombinu ya mfumo wa maji taka.
- (ii) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu - Mkawawa:** Mradi wa chuo unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2016/17

shilingi bilioni 4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya chuo pamoja na kukamilisha jengo la mihadhara la Chuo.

- (iii) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu - Dar es Salaam:** Mradi unalenga kukarabati na kupanua miundombinu ya chuo. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa maabara za sayansi na kumalizia ujenzi wa jengo la utawala.
- (iv) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dodoma:** Mradi unalenga kuimarisha miundombinu ya chuo. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 5 fedha za ndani kwa ajili ya kujenga madarasa na hosteli za Chuo cha "Earth Science" pamoja na chuo cha "*Natural and Mathematical Science*".
- (v) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Huria:** Mradi unalenga ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya vituo vya chuo vya kikanda. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika vituo vya mikoa (6) ya Ruvuma, Rukwa, Kilimanjaro, Singida, Mara na Pwani.
- (vi) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ardhi:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya chuo. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa maabara ambayo itakuwa na matumizi mbalimbali (Multi Purpose Laboratory) pamoja na ukarabati wa hosteli za wanafunzi awamu ya VI.
- (vii) **Mradi wa Ukarabati na Ujenzi Chuo Kikuu Mzumbe:** Mradi unalenga kukarabati hosteli 5 za wanafunzi na maktaba. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hosteli za wanafunzi na maktaba katika Kampasi ya Mbeya.
- (viii) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine:** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 4

fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukarabati kumbi za mihadhara, maabara na hosteli za wanafunzi.

- (ix) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili:** Mradi unalenga kuongeza udahili wa wanafunzi katika fani mbalimbali za kada ya afya. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 13 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali ya kufundishia - Kampasi ya Mloganzila na ukarabati wa hosteli na jengo la utawala Kampasi Kuu ya Muhimbili.
- (x) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 4.1 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukarabati majengo na miundombinu mingine katika kampasi kuu ya Moshi na kampasi ya Kizumbi.
- (xi) **Mradi wa Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwl. Julius K. Nyerere:** Mradi unalenga kuongeza udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu katika fani za masomo ya sayansi. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 10 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa maabara, madarasa, hosteli na ofisi.
- (xii) **Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya chuo. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kujenga na kuweka samani kwenye jengo la maktaba ili kuhimili ongezeko la udahili wa wanafunzi.
- (xiii) **Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – Arusha:** Mradi unalenga kuwezesha taasisi kujitegemea. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 3 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuzisaidia kifedha taasisi za elimu ya juu ili ziweze kufundisha ujuzi unaohusiana na sayansi na teknolojia.
- (xiv) **Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu:** Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inalenga kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni

427.55 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi 270,000 wa elimu ya juu wenye vigezo vya kupata mikopo na ruzuku hizo. Aidha, Bodi itakusanya marejesho ya mikopo kiasi cha shilingi bilioni 43.8 ambazo pia zitatumika kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

- (xv) **Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Vyuo Vikuu:** Mradi unalenga kujenga miundombinu ya Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU). Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 3 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Tume ya Vyuo Vikuu, Dar es Salaam.
- (xvi) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Ufundis Arusha:** Mradi unalenga kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la uhandisi wa umwagiliaji pamoja na kuweka vifaa vya kufundishia.
- (xvii) **Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hosteli katika kampasi ya Kivukoni na kununua samani kwa ajili ya Kampasi ya Bububu.
- (xviii) **Ukarabati na upanuzi Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundis (NACTE):** Mradi unalenga kununua samani za ofisi na kukamilisha ujenzi wa jengo la Baraza. Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 700 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kununua samani za ofisi, kukamilisha malipo ya deni la mkandarasi na kukamilisha ujenzi wa jengo la mitihani la Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundis.
- (xix) **Mradi wa Ujenzi wa Jengo la kufundishia Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam:** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 5 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 10 la kufundishia (DIT Teaching Tower) na kuweka umeme na samani katika Kampasi Kuu, Dar es salaam

na kukarabati miundombinu ya majitaka kwa Kampasi ya Mwanza.

- (xx) **Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH:** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 8 fedha za ndani na bilioni 2.98 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kujenga uwezo wa Watafiti 90 katika ngazi ya Uzamivu (PhD) wa TEHAMA na sayansi; kufadhili miradi mipy 18 ya utafiti ya kipaumbele kwa kushirikiana na Serikali za Afrika ya Kusini, India, na Korea ya Kusini; na kufadhili miradi ya utafiti 22 inayoendelea na 32 mipy ya utafiti kwa kushirikiana na SIDA; ufuutiliaji na tathmini ya miradi ya utafiti na maendeleo na masuala ya teknolojia; kugharamia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya utafiti ikijumuisha maabara, vifaa vya utafiti, na miundombinu ya majoribio ya utafiti.
- (c) **Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu:** Mradi unalenga kuboresha mazingira kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 8 fedha za ndani na shilingi bilioni 15 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya vyuo vine (4) vya Ualimu vya Kitangali, Ndala, Shinyanga na Mpuguso.
- (d) **Ujenzi wa vyuo vya Ufundisti**
Mradi unalenga kuendeleza ujenzi wa vyuo vya ufundisti katika mikoa 4 isiyokuwa na vyuo hivyo kwa sasa. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa vyuo vya Ufundisti katika mikoa ya Njombe; Rukwa; Geita na Simiyu.

4.2.2 Afya na Ustawi wa Jamii

- (a) **Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa:** Mradi unalenga kuanzisha vituo vya upokeaji na utoaji damu. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 11 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.5 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa benki za damu katika mikoa ya Kigoma na Geita na kuwezesha huduma za matengenezo ya vifaa vya uchunguzi wa magonjwa kupitia mpango wa ORIO.

Hospitali ya Rufaa Mbeya: Mradi unalenga kuendeleza ujenzi na ununuzi wa vifaa katika Hospitali ya rufaa ya Mbeya. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ghorofa 2 za jengo la mionzi na ununuzi wa vifaa

tiba. **Hopitali ya Rufaa Mtwara:** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali. **Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza Kibong'oto:** Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi milioni 876 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa wodi na kununua vifaa tiba. **Hospitali ya Mirembe na Isanga:** Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 1.45 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ukuta uzio na ukarabati wa wodi ya hospitali ya Mirembe; na kukamilisha jengo la Itega la wagongwa wa nje walioathirika na matumizi ya madawa ya kulevya. **Taasisi ya Saratani Ocean Road:** Katika mwaka 2016/17 shillingi bilioni 5 zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa tiba. **Hospitali ya Taifa Muhimbili:** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa tiba na kujenga mfumo wa kujikinga. **Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI):** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 4.8 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na kulipa deni la Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. **Hospitali ya Bugando:** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ununuzi na usimikaji wa vifaa tiba. **Hospitali ya KCMC:** Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

(b) Mradi wa Huduma za Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi:

Mradi unalenga kuboresha hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi nchini. Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 251.5 fedha za ndani kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vyote vyaa umma vyaa kutolea huduma za afya.

(c) Mradi wa Kudhibiti Magonjwa ya Kuambikiza: Mradi unalenga kuimarisha huduma za kupambana na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza kuitia huduma za chanjo, afya ya uzazi na mtoto, usafi wa mazingira, afya mipakani na uzazi wa mpango. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 10 fedha za ndani na shilingi bilioni 103.677 fedha za nje kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na ununuzi wa chanjo.

(d) Programu ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI: Programu hii inalenga kuendeleza vita dhidi ya maambukizi ya Virusi vyaa UKIMWI (VVU) na kuboresha huduma kwa watu wanaoishi na VVU. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 29.896 fedha za nje kwa ajili ya ununuzi, uhifadhi na usambazaji wa dawa za kupunguza makali ya VVU, dawa za

kutibu magonjwa nyemelezi, dawa za kutibu magonjwa ya ngono, vitendanishi na vifaa vya maabara.

4.2.3 Maji Safi na Majitaka

- (a) Mradi wa Kuboresha Huduma za Maji katika Jiji la Dar es Salaam:** Mradi unalenga kuongeza na kuboresha upatikanaji wa huduma za maji katika jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 128.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 54.53 fedha za nje kwa ajili ya kukamilisha miradi ya Ruvu Juu, Ruvu Chini na Visima virefu vya Kimbiji na Mpera; kuanza ujenzi wa mradi wa usambazaji na uondoaji maji taka; na utekelezaji wa miradi mipyä chini ya mpango maalum wa kuboresha huduma za maji katika jiji la Dar es Salaam.
- (b) Miradi ya Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Huduma za Maji Mijini:** Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 89.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 75.5 fedha za nje kwa ajili ya kukamilisha miradi 6 katika miji ya Mtwara, Sumbawanga, Lindi, Kigoma, Musoma na Babati; kukamilisha na kuendelea na upanuzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa mipyä ya Geita, Simiyu, Njombe, Katavi, na Songwe; kuanza ujenzi wa miradi ya maji katika miji midogo na makao makuu ya wilaya 9 zenyé uhaba mkubwa wa maji za Kisarawe, Chunyu, Orkesumet, Ilula, Makambako, Korogwe, Tunduma, Kilwa Masoko, Mangaka, na Kayanga; na kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika miji ya Ruangwa, Liwale, Nanyumbu, Kibaya, Mbulu, Magugu, Galapo, Dareda, Bashnet, Mahenge, Ifakara, Mvomero, Mikumi, Chamwino, Bahi, Gairo, Kondoa, Nyang'hwale, Katoro na makao makuu ya Wilaya mpyä; kuanza ujenzi wa mradi wa kutoa maji mto Ruvuma kwenda Manispaa ya Mtwara – Mikindani; kukamilisha maandalizi ya mradi ya uondoaji maji taka katika mikoa 6 ya Morogoro, Kilimanjaro, Tanga, Iringa, Arusha na Dodoma; na ukarabati na upanuzi wa mifumo ya maji katika miradi 7 ya kitaifa ya Mugango-Kiabakari, Makonde, Maswa, Wanging'ombe, Masasi-Nachingwe, Handeni na Chalinze.
- (c) Miradi ya Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Huduma za Maji Vijijini:** Mradi unalenga kuwapatia maji safi na salama wananchi waishio vijijini kutoka asilimia 72 hadi 77 kwa kukamilisha miradi inayoendelea na kuanza utekelezaji wa miradi mipyä vijijini katika Halmashauri zote nchini. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 373.34 fedha za ndani na shilingi bilioni 48.22 fedha za nje

zitakazotolewa na DFID pamoja na washirika wengine wa maendeleo JICA, *Water Aid* na Serikali ya Ubelgiji kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji na vituo vipyta 631 vya maji vijijini katika mkoa wa Tabora; kujenga miundombinu ya usambazaji maji Njombe vijijini, Urambo, Singida vijijini, Mbulu, Babati, Iramba na Kilosa; na kujenga miundombinu ya usambazaji maji katika vijiji vya mkoa wa Morogoro.

- (d) **Mradi wa Maji Ziwa Victoria – Kahama – Nzega – Igunga – Tabora - Sikonge:** Mradi unalenga kusambaza maji katika miji na vijiji katika mikoa ya Kahama, Shinyanga na Tabora. Utekelezaji wa mradi utagharamiwa kwa ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (INDIA) kwa awamu. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 12 fedha za ndani na shilingi bilioni 11 fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika miji ya Kagongwa, Isaka, Tinde, Nzega, Igunga, Sikonge, Tabora na vijiji 89 pembezoni mwa bomba kuu la maji kutoka ziwa Victoria; ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji katika miji ya Kwimba, Malampaka, Sumve, Mallya, Busega, Bariadi, Langambilili, na Mwanhuzi; ukarabati na upanuzi wa mifumo ya usambazaji maji katika miji ya Mwadui, Kishapu, Kolandoto, na Maganzo.
- (e) **Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda:** Mradi wa bwawa la Kidunda unalenga kuhifadhi maji mita za ujazo milioni 190. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 10.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 7 fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kidunda - Ngerengere (km 75) na ulipaji wa fidia kwa wananchi 2,603 watakaopisha ujenzi wa barabara.
- (f) **Mradi wa maji Same - Mwanga – Korogwe:** Mradi unalenga kujenga miundombinu ya usambazaji wa maji yenye uwezo wa kuhudumia watu 456,931 katika miji ya Same, Mwanga na vijiji 38 na kutosheleza mahitaji ya maji hadi mwaka 2038. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 19.22 fedha za ndani na shilingi bilioni 34.17 fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika miji ya Same, Mwanga na Korogwe; na kujenga vituo 1,828 vya maji katika vijiji mbalimbali katika eneo la mradi.
- (g) **Mradi wa Maji wa Masasi – Nachingwea:** Mradi unalenga kujenga miundombinu ya usambazaji maji na vituo vya kuuzia maji katika miji midogo. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 1 fedha za

ndani kwa ajili ya ukarabati wa mifumo ya usambazaji maji katika miji ya Masasi na Nachingwea.

- (h) Mradi wa Uendelezaji na Utunzaji wa Rasilimali za Maji Pamoja na Ubora wa Maji:** Mradi unalenga kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 50.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 12.75 fedha za nje kwa ajili ya kukamilisha uandaaji wa mipango ya mabonde ya Pangani, Ziwa Victoria, Wami na Ruvu na kuanza utekelezaji wa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde ya Rufiji, Ruvuma, Ziwa Tanganyika, Rukwa na Nyasa; utekelezaji wa mkakati wa teknolojia ya kutoa madini ya fluoride kwenye maji; utekelezaji wa mkakati wa usimamizi wa ubora wa maji na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji; ujenzi wa majengo ya Maabara za maji katika mikoa ya Tabora, Geita, Kilimanjaro na Manyara; kujenga vituo 70 vya uchunguzi wa mwenendo wa rasilimali za maji nchini; kuanza maandalizi ya ujenzi wa mabwawa mawili ya kimkakati ya Farkwa na Ndembera na kukarabati mabwawa 4 ya Nkiniziwa na Itobo (Nzega), Lemioni na Enguikment II (Monduli); na kukamilisha ujenzi na ukarabati wa ofisi za mabonde.

4.2.4 Kazi, Vijana, Ajira na Wenyewe Ulemavu

- (a) Mfuko wa Maendeleo ya Vijana:** Mfuko huu uliundwa kutokana na Azimio la Bunge kwa lengo la kusaidia Vijana kiuchumi katika juhudi za Serikali za kupunguza tatizo la ajira miongoni mwa vijana. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 1 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana kulingana na miradi waliyobuni; kujenga uwezo wa Vijana, Maafisa wa Vijana wa Halmashauri na Viongozi wa SACCOS za Vijana katika kuhamasisha uundwaji na usimamizi wa SACCOS imara na endelevu pamoja na kujifunza namna nzuri ya matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; na kufanya ufuataliaji na tathmini ya miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.
- (b) Programu ya Kukuza Ujuzi:** Programu inalenga kuendeleza ujuzi kwa wasiokuwa na ujuzi unaohitajika (*skills mismatch*) katika soko la ajira kuajirika. Programu itatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 15 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuandaa na kusambaza miongozo ya mafunzo kwa vitendo; kutoa mafunzo ya

uanagenzi (apprenticeship) kwa watu 4,600; kutoa mafunzo kazini kwa kuongeza ujuzi na mafunzo mtambuka kwa wafanyakazi 13,400 ili kuongeza tija na kuboresha huduma; kuwezesha wahitimu 4,000 kufanya mafunzo ya ujuzi kwa vitendo mahala pa kazi (internship); kutambua na kurasimisha ujuzi uliopatikana katika mfumo usio rasmi wa mafunzo kwa watu 5,000; kuimarisha vituo vya ajira mikoani na mfumo wa taarifa za soko la ajira; na kufuatilia utekelezaji wa programu ya kukuza ujuzi.

- (c) **Mradi wa Kubaini Ajira zenyne Tija Nchini:** Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Wizara ya Ushirikiano na Maendeleo ya Ujerumani chini ya mpango ujulikanao kama "Employment for Sustainable Development in Africa". Mradi unalenga kubaini ajira zenyne tija kwa wananchi ili kuiwezesha Serikali ya Tanzania kutunga Sera, Sheria na Miongozo katika kukuza na kuboresha ajira nchini hususani kwa watu wenye ulemavu. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 1.49 fedha za nje kwa ajili ya kufanya utafiti wa kubaini ajira zenyne manufaa katika maeneo na sekta mbalimbali za uzalishaji mali na utoaji huduma nchini.

4.2.5 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mradi unalenga kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutenga shilingi milioni 50 kwa kila kijiji kama mfuko wa uwezeshaji (*revolving fund*) kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wajasiriamali kuptitia ushirika wa kuweka na kukopa katika vijiji. Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 59 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huu. Mradi utasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu – Baraza la Taifa Uwezeshaji Kiuchumi na uratibu wa matumizi ya fedha hizo utaandaliwa ili kuwezesha kufikia malengo ya Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015.

4.2.6 Wanyamapor

(a) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili Nchini (Sustainable Natural Resource Management in Tanzania)

Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ujerumani kuptitia Shirika la Maendeleo ya Ujerumani – GIZ. Mradi unalenga kuimarisha matumizi endelevu ya maliasili hususan za wanyamapor kwa kujenga uwezo wa taasisi na ushiriki wa wananchi katika kuhifadhi maliasili. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 4.88 fedha za nje kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri Wilaya za Ngorongoro na Serengeti katika masuala ya

sera, sheria na taratibu za kuwezesha halmashauri hizo kunufaika na mapato yatokanayo na uhifadhi na utalii; na kuziwezesha Halmashauri hizo kutoa mafunzo ya uhifadhi na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

(b) Mradi wa Kilombero and Lower Rufiji Wetland Ecosystem Management Project (KILORWEP)

Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ubeligiji. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2.08 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha uanzishwaji na usimamizi wa maeneo ya hifadhi ya jamii- WMAs na usimamizi shirikishi wa maliasili katika wilaya za Ulanga, Rufiji na Kilombero; kuwezesha usimamizi wa mpango wa matumizi bora ya ardhi; na upembuzi yakinifu na tathmini ya shughuli za kiuchumi za wananchi zinazotegemea maliasili katika wilaya za Ulanga, Kilombero na Rufiji.

(c) Mradi wa Kuimarisha Kitengo Cha Kukabiliana na Ujangili Katika Mapori Tengefu Nchini (Capacity Building in Game Reserves and Anti-Poaching Unit in Tanzania)

Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za watumishi katika mapori ya akiba na vikosi dhidi ya ujangili, kujenga miundombinu ya maji, umeme, afya na kuwajengea uwezo watumishi wa vikosi dhidi ya ujangili.

(d) Mradi wa Kukabiliana na uhalifu wa Wanyamapor (Support to Combating Wildlife Crime and Advancing Conservation Project)

Mradi huu unalenga kutekeleza mkakati wa Taifa wa kuzuia ujangili na unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa - UNDP. Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 830 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha doria nchini ili kukabiliana na wahalifu wa makosa ya jinai ya wanyamapor; tathmini ya kuanzishwa kwa kitengo kinachoshughulikia makosa ya jinai ya wanyamapor; tathmini kitaifa ya makosa ya uhalifu wa rasilimali za wanyamapor na hatua zilizochukuliwa kwa makosa hayo; na kuendesha mafunzo maalum kwa mahakimu wa mahakama za wilaya na waendesha mashitaka kuhusu sheria za wanyamapor na utunzaji wa ushahidi.

4.2.7 Misitu

(a) **Mradi wa Uendelezaji wa Misitu Binafsi na Mnyororo wa Thamani (Private Plantation Forestry and value Chain)**

Mradi unatekelezwa kwa ufadhilli wa Serikali ya Finland na unalenga kupunguza umaskini wa kipato kwa kuhakikisha kuwa sekta binafsi zinashiriki katika kupanda miti na kuongeza wigo wa misitu binafsi, kuimarisha taasisi za mafunzo ya misitu na kutoa mafunzo ya namna bora ya kunufaika na misitu kwa wananchi. Mradi huu unatekelezwa katika wilaya za Mufindi, Kilolo, Njombe, Makete, Ludewa na Kilombero. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 2.64 fedha za nje kwa ajili ya kujenga mazingira wezeshi ya kuendeleza misitu binafsi; kuwezesha utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi; na kuwezesha vikundi vinavyojishughulisha na kilimo cha miti kwa kutoa elimu wa shughuli mbadala za kiuchumi zaidi ya upandaji miti.

(b) **Mradi wa Kuimarisha Mtando wa Hifadhi ya Misitu kwa Utunzaji wa Bionuai Tanzania (Enhancing the Forest Nature Reserve Network for Biodiversity Conservation in Tanzania)**

Mradi huu unafadhiliwa na UNDP na utatekelezwa katika hifadhi asilimia 11 za misitu kwa kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa hifadhi hizo na kuboresha miundombinu ya hifadhi ili kuvutia utalii na ustawi wa ikolojia. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 1.32 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kupitia mipaka na kuandaa mipango ya usimamizi ya hifadhi asilia za misitu sita (6); Kuwezesha sekta binafsi kuwekeza miundombinu ya utalii katika hifadhi asilia za misitu; kuwezesha utangazaji wa utalii wa vivutio vilivyopo katika hifadhi asilia za misitu; na kuwezesha jamii zilizo karibu na hifadhi asilia kutekeleza miradi ya kujiongezea kipato.

4.2.8 Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

(a) **Program ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi:** Program hii inalenga kujenga miundombinu ya kukabiliana na kuongezeka kwa usawa wa bahari (ukuta wa bahari maeneo ya Ocean Road, Kigamboni, Pangani na Kisiwa Panza – Pemba na Makinga bahari Kilimani – Zanzibar). Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 3.20 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.69 fedha za nje kwa ajili ya kujenga ukuta wa kuzuia maji ya bahari ili kupunguza madhara ya kuongezeka kwa kina cha bahari kwa wananchi; kupanda mikoko Rufiji, Pangani, Kilimani (Unguja), Bwawani (Unguja), Kisiwa Panza (Pemba), Tumbe (Pemba), Ukelele na Tovuni (Pemba) ili kupunguza athari za

mmomonyoko wa maeneo ya Pwani kutokana na kuongezeka kwa usawa wa bahari; kukarabati na kuimariswa ukuta wa bahari (Ocean Road na Kigamboni); kurekebisha maeneo ya ukanda wa Bahari ambayo yameathiriwa na kuongezeka kwa maji ya bahari; na ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika jiji la Dar es Salaam.

- (b) **Mradi wa Kudhibiti na Kuhifadhi Tabaka la Ozoni:** Mradi unalenga kulinda tabaka la Ozoni na kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yatokanayo na kuharibika kwa tabaka hilo. Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 80 fedha za ndani na shilingi milioni 147 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu shughuli za mkataba wa "Montreal"; kuwezesha mafunzo kuhusu kemikali zinazosababisha mmomonyoko wa tabaka la ozoni; kutekeleza Mpango wa kitaifa wa kupunguza/ kusitisha matumizi ya kemikali aina *Hydrochlorofluocarbons* (HCFCs); na kukusanya taarifa kuhusu uagizaji na matumizi ya kemikali zinazosababisha uharibifu wa tabaka la ozoni.

4.2.9 Ardhi, Nyumba na Makazi

Mradi wa Kuwezesha Kumilikisha Ardhi: Mradi unalenga kupima ardhi na kutoa hatimiliki katika ngazi ya vijiji, miji na majiji. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 3 fedha za ndani na shilingi bilioni 10 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutoa hati ya hakimiliki za kimila 100,000 katika wilaya tatu (3) za mfano za Kilombero, Ulanga na Malinyi; kubaini mipaka ya vijiji na kutatua migogoro katika vijiji 75; kuandaa na kutoa vyeti vya ardhi ya kijiji katika vijiji 75; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 100; kuandaa Mipangokina ya vitovu vya vijiji katika vijiji 100; kupima vipande 150,000 vya ardhi; kuboresha masijala za ardhi katika wilaya 3 za mfano; kukarabati masijala za ardhi za vijiji 75; na kuimariswa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Aidha, shilingi bilioni 5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanzisha Mfuko wa Fidia ya Ardhi.

4.3 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji

4.3.1 Nishati

- (a) **Miradi ya Uzalishaji Umeme**

i. **Kuungeza Uwezo wa Uzalishaji Umeme wa Mitambo ya Kinyerezi I (MW 185).**

Mradi unalenga upanuzi wa mtambo wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I kwa kuungeza mitambo itakayozalisha MW 185 zaidi kutoka kiwango

cha umeme unaozalishwa kwa sasa katika mtambo huo ambacho ni MW 150. Mradi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 na kwa sasa taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa upanuzi wa mitambo hiyo zinaendelea. Katika mwaka 2016/17 shillingi bilioni 119 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Shughuli zitakazotekelawa ni kuanda eneo la ujenzi wa mitambo ikiwa ni pamoja na kujenga msingi katika eneo itakapowekwa mitambo hiyo, kusanifu ujenzi wa mitambo, na kusimika mitambo.

ii. Mradi wa Kufua Umeme Kinyerezi II (MW 240)

Mradi huu unahu ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa MW 240 kwa kutumia gesi asilia katika eneo la Kinyerezi ili kuongeza kiwango cha umeme kwenye Gridi ya Taifa. Gharama za kutekeleza mradi huu ni Dola za Kimarekani milioni 344 ambapo asilimia 85 ya fedha hizo ni mkopo kutoka Benki za Sumitomo Mitsui Banking Corporation (SMBC) ya Japan na Japan Bank for International Cooperation (JBIC) za Japan. Serikali ya Tanzania imetoa Shilingi bilioni 110 katika mradi huo ikiwa ni asilimia 15 ya gharama za mradi. Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 200 fedha za ndani na bilioni 110 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mkandarasi kuanza ujenzi wa ofisi mbalimbali za wakandarasi, kuwapata 'subcontractors' wa mradi, kuagiza vifaa mbalimbali, kujenga misingi ya mitambo na kusimika mitambo.

iii. Mradi wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Kiwira (MW 200) - Mbeya

Mradi umegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni: upanuzi wa mgodi wa chini ya ardhi (underground mine) kutoka uwezo wa kuzalisha tani 150,000 hadi tani 300,000 kwa mwaka; kuanzisha mgodi wa wazi (open cast mine) wenye uwezo wa kuzalisha tani 1,200,000 kwa mwaka; kujenga mtambo wa kufua umeme (coal fired power plant) wenye uwezo wa kuzalisha MW 200; na kujenga njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa kV 400 kutoka Kiwira hadi Mbeya (km 100). Makadirio ya gharama za utekelezaji wa mradi ni dola za kimarekani milioni 498 na utatekeleza kwa ubia kati ya Serikali (kupitia Shirika la Madini la Taifa – STAMICO) na wawekezaji wa sekta binafsi. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 2 kwa ajili ya tathimini ya malipo ya fidia kwa watakaoathirika na mradi, na kuboresha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi.

iv. Miradi ya Uzalishaji Umeme wa Nguvu za Maji (Hydro Eletic Power)

a) Mradi wa Kufua Umeme kwa Kutumia Maji (MW 80) - Rusumo

Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kufua umeme kwa kutumia nguvu ya maji wa MW 80 kwa ushirikiano wa nchi tatu (3) za Tanzania, Rwanda na Burundi. Umeme utakaozalishwa na kituo hiki utagawanywa kwa usawa kati ya nchi hizo. Pia mradi huu utahusisha ujenzi wa njia za usafirishaji umeme wa msongo wa KV 220 kutoka Rusumo hadi kwenye mifumo ya usafirishaji wa umeme kwa nchi husika. Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha upatikanaji wa umeme katika mikoa iliyoko Kaskazini na Kaskazini-Maghribi mwa Tanzania na hivyo kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya umeme katika maeneo hayo. Mradi huu pia utapunguza gharama za uzalishaji umeme kwa kutumia mafuta katika maeneo ya Biharamuulo na Ngara. Gharama za mradi ni dola za Kimarekani Milioni 35 na mradi utafadhiliwa na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB). Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 5 fedha za nje zimetengewa kwa ajili ya: kuanza ulipaji wa fidia kwa baadhi ya wananchi watakaopisha mradi na kusafisha(route clearance) njia ya usafirishaji wa umeme na eneo la ujenzi wa mitambo ya kufua umeme.

b) Mradi wa Kufua Umeme kwa Kutumia Maji (MW 45) - Malagarasi.

Mradi unalenga kujenga kituo cha kuzalisha umeme wa MW 45 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Malagarasi mkoani Kigoma. Mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Tanzania na utakapokamilika utasaidia kuongeza kiwango cha umeme kwenye Gridi ya Taifa na kuongeza upatikanaji wa huduma ya umeme katika maeneo ya Magharibi ya nchi. Gharama za ujenzi wa mtambo ni dola za kimarekani milioni 149.5 na unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 1 fedha za ndani na shilingi bilioni 4 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: Kuajiri Mtaalamu Mshauri kwa ajili ya kuutangaza mradi kwa njia ya ushindani; kufanya usanifu wa mitambo (*technical design*); kutangaza zabuni; kufanya upimaji wa eneo utakapo jengwa mtambo na njia ya usafirishaji wa umeme; na kuajiri wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi.

c) Mradi wa Kufua Umeme kwa Kutumia Maji (MW 87) - Kakono.

Mradi unahusisha ujenzi wa kituo cha kufua umeme wa MW 87 kwa kutumia maji ya mto Kagera katika eneo la Kakono mkoani Kagera. Pia, mradi unahusisha ujenzi wa njia kubwa ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 132 na urefu wa kilometra 38.8 kutoka Kakono hadi Kyaka. Mradi utatekelezwa na TANESCO kwa gharama za dola za Kimarekani milioni 379.4 na utafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 3 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kumwajiri Mtaalamu Mshauri kwa ajili ya kuutangaza mradi kwa njia ya ushindani; kufanya usanifu wa mitambo (*technical design*); kuandaa hati za zabuni (*tender/bidding documents*); upembuzi yakinifu (*survey*) wa eneo utakapojengwa mtambo na njia ya usafirishaji wa umeme; na kuajiri wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi.

v. Uendelezaji wa Nishati ya Joto Ardhi (Geothermal) – (MW 100)-Mbeya

Mradi huu unahusu uendelezaji wa jotoardhi kwenye mlima wa Volcano wa Ngozi Mkoani Mbeya kwa ajili ya kuzalisha umeme wa Megawati 100 (kwa kuanzia). Mradi unatekelezwa na Serikali kuitia Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (Tanzania Geothermal Development Company Limited - TGDC) kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB/CIF) na Kamisheni ya Afrika (African Union Commission).

Katika Mwaka 2016/17, shilingi bilioni 2 fedha za ndani na shilingi bilioni 26 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Shughuli zitakazotekelawa ni: kukamilisha utafiti na tathmini ya mazingira; kukamilisha upembuzi yakinifu katika maeneo ya Kisaki (Morogoro), Luhoi (Pwani); usanifu na ujenzi wa miundombinu ya barabara (madaraja), maji na umeme kuelekea katika maeneo yatakayochorongwa; upatikanaji wa ardhi; na kuanza maandalizi ya awali ya kuchoronga visima vitatu (3) katika eneo la Ziwa Ngozi (Mbeya) ili kutathmini kiwango cha nishati iliyopo na uwezo wake wa kuzalisha umeme.

(b) Miradi ya Usambazaji Umeme

i. Mradi wa Umeme wa Msongo wa KV 400 Iringa - Shinyanga (km 670)

ii. Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga na upanuzi wa vituo vikuu vya kupozea

umeme wa KV 400/220 katika miji ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga. Mradi huu unagharamiwa kwa mikopo kutoka Benki ya Dunia (WB), Benki ya Afrika (AfDB), Benki ya Jumuia ya Ulaya (EIB), Serikali za Japan kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na Jamhuri ya Korea kupitia Shirika la Maendeleo la Korea (EDCF). Mradi utakapokamilika utaboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Singida, Arusha, Shinyanga, Mwanza na Tabora. Aidha, utasaidia uunganishaji wa Gridi za Taifa katika nchi za Kenya na Tanzania yaani East African Power Pool na pia Tanzania na Zambia kwa upande wa Kusini yaani Southern African Power Pool. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 20 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupozea umeme (KV 400/220).

iii. Mradi wa Umeme wa Msongo KV 220 Makambako – Songea

Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa KV 220 kutoka Makambako hadi Songea, yenyere urefu wa kilometra 250, vituo vitatu (3) vya kupozea umeme, ujenzi wa njia za kusambaza umeme wa KV 33 zenye urefu wa kilometra 900, usimikaji wa transforma 250 na ujenzi wa vituo vya kupozea umeme vyenye ukubwa wa KV 220/33 hadi MVA 50 katika vituo vya Madaba na Songea. Aidha, vijiji takribani 250 vitahusishwa ambapo jumla ya wateja wa awali 22,700 wataunganishiwa umeme. Mradi unalenga kuunganisha Mikoa ya Ruvuma na Njombe pamoja na Wilaya zake Namtumbo, Mbinga, Songea Mjini, Songea Vijijini, Njombe na Ludewa katika Gridi ya Taifa. Vile vile, mradi utahusisha kuunganisha umeme kwa wateja wa awali 30,000. Gharama za utekelezaji wa mradi ni dola za kimarekani milioni 82 sawa na shilingi bilioni 172.2. Mradi unatekelezwa na TANESCO kwa fedha za ndani na mkopo kutoka Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA) na benki ya ABSEK ya Sweden. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 22 fedha za ndani na bilioni 20 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme na kuendelea na ujenzi wa njia kubwa ya kusafirisha umeme.

iv. Mradi wa Msongo wa Kv 400 wa Somangafungu – Kinyerezi.

Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 400 kutoka Somangafungu hadi Kinyerezi Dar es Salaam yenyere urefu wa kilomita 198. Kwa upande wa Somangafungu, mradi utaunganishwa na mradi wa kufua umeme wa Kilwa Energy unaotekelizwa na Kampuni binafsi ya Kilwa Energy. Ghrarama ya mradi ni dola za Kimarekani milioni 150 na unafadhiliwa na Serikali pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (DBSA). Katika mwaka 2016/17,

shilingi bilioni 5 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ulipaji fidia kwa wananchi watakaoathiriwa na mradi; kuajiri Mtaalamu Mshauri wa kutayarisha usanifu wa kifundi (*detail design*); na kuajiri msimamizi wa mradi.

v. Mradi wa Msongo wa kV 400 North - East Grid (Dar – Tanga – Arusha)

Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme wa msongo wa kV 400 kutoka Dar es Salaam hadi Arusha kupitia Chalinze na Tanga (kilometra 702) pamoja na kujenga vituo vikuu vya kupozea umeme wa msongo wa kV 400/220/33. Mradi unalenga kusafirisha umeme utakaozalishwa eneo la Kinyerezi – Dar es Salaam na kuunganisha na Gridi ya Taifa ili kuboresha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Aidha, mradi huu utakapokamilika utasaidia uunganishaji wa umeme kwa wateja wapya kufuatia kukua kwa mahitaji ya umeme katika mikoa hiyo iliyo na shughuli nyingi za uchimbaji wa madini na utalii. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 11 fedha za ndani na shilingi bilioni 5 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi, kupata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kusimamia ujenzi wa mradi na kuanza ujenzi wa mradi.

vi. Mradi wa msongo wa Kv 220 wa North – West Kutoka Geita - Nyakanazi

Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 na urefu wa kilometra 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi; upanuzi wa kituo cha kupozea umeme cha Geita pamoja na usambazaji wa umeme kwenye vijiji vinavyopitiwa na mradi. Mradi unalenga kuunganisha maeneo ya Magharibi na Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania katika Gridi ya Taifa. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 1 fedha za ndani na shilingi bilioni 12 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi, kupata mkandarasi na kuanza ujenzi wa mradi.

vii. Mradi wa msongo wa KV 220 Bulyanhulu – Geita.

Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilometra 55 kutoka Bulyanhulu hadi Geita; upanuzi wa kituo cha kupozea umeme cha Bulyanhulu na usambazaji umeme katika vijiji vilivyopo ndani ya eneo la mradi. Mradi unahusisha

ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV 220 yeny urefu wa km 55 pamoja na usambazaji umeme katika vijiji 10 katika wilaya ya Geita. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Uarabuni (BADEA), Opec Fund for International Development (OFID) pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 1 fedha za ndani na shilingi bilioni 5 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi na kuanza utekelezaji wa mradi.

(c) Miradi ya kusambaza umeme vijiji na Makao Makuu ya Wilaya

Mradi huu unasimamiwa na Wakala wa Nishati Vijiji (REA) na unatekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Mradi unahusisha ujenzi wa njia za kusambaza umeme za msongo wa kV 11 na kV 33 zeny urefu wa jumla ya kilometra 25,000; njia za usambazaji umeme za msongo wa Volti 400 na Volti 230 zeny urefu wa jumla ya kilometra 38,000; na ufungaji wa vipoza umeme (distribution transformers) 13,000. Mradi huu umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2016/17 na utakapokamilika, jumla ya wateja 340,000 wataunganishiwa umeme.

Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 534.4 fedha za ndani na shilingi bilioni 53.2 fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. Kazi zitakazofanyika katika mwaka 2016/17 ni: kuandaa mahitaji na usanifu wa mradi; kutafuta wakandarasi watakoatekeleza mradi; na kuanza utekelezaji wa mradi. Kazi nyingine ni pamoja na kukamilisha utekelezaji wa Awamu ya Pili ya mradi wa kupeleka umeme vijiji (REA Turnkey Phase II) ikiwa ni pamoja na kufunga transfoma na kusambaza umeme katika maeneo yaliyopitiwa na miundombinu ya umeme (*densification*). Mradi unalenga kuwaunganishia umeme wananchi kwenye maeneo ambayo tayari yana miundombinu lakini hawapati huduma hiyo ambapo wateja wapatao 200,000 wanatarajiwa kuunganishiwa umeme.

(d) Mradi wa Liquified Natural Gas (LNG)

Mradi unalenga kuendeleza gesi asilia inayozalishwa katika kina kirefu baharini kwa kuichakata gesi hiyo na kuigeuza kuwa kimiminika kwa lengo la kuisafirisha nje ya nchi ikiwa imesindikwa na pia gesi hiyo iweze kutumika ndani ya nchi. Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na Makampuni ya Mafuta ya Kimataifa na wadau wengine. Katika mwaka 2016/17, shilingi milioni 800 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: uhakiki wa uthamini wa mali kwa wananchi watakaopisha mradi; kuandaa Mpango Kazi wa Kuwahamisha Waathirika wa

Mradi (Resettlement Action Plan) ikiwa ni pamoja na kuchora michoro ya viwanja vyta maeneo ya kuhamishia waathiriwa wa mradi; kuanza majadiliano "Host Government Agreement" kwa ajili ya uendelezaji wa mradi; na kuandaa waataalam wa ndani kwa kuwapa mazoezi ya vitendo katika miradi ya LNG inayosimamiwa na BG na Statoil.

(e) Miradi ya Kujenga Miundombinu ya Usambazaji Gesi Asilia (CNG & Piped Natural Gas Distribution Networks) katika Mikoa in Lindi na Mtwara

Mradi unahusisha ujenzi wa mtando wa kusambaza gesi asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa watumiaji wa majumbani, kwenye taasisi mbalimbali na viwandani. Mabomba hayo yataunganishwa katika matoleo ya bomba kubwa la kusafirishia gesi asilia kutoka Mnazi Bay – Mtwara na Songo Songo – Lindi hadi Dar es Salaam. Kwa sasa TPDC imemuajiri Mshauri Mwelekezo kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za kijamii na kimazingira za awali (ESIA). Katika mwaka 2016/17, shilingi milioni 700 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu wa tathmini ya athari za kijamii na kimazingira (ESIA), kukamilisha usanifu wa kina wa kihandisi na kuandaa zabuni ya kumpata mwekezaji.

4.3.2 Kilimo

Serikali imekuwa na programu na mikakati mbalimbali ya kuendeleza sekta ya kilimo ikijumuisha Kilimo Kwanza, Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo - ASDP na Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa. Malengo ya mikakati hiyo ni kuongeza tija, mchango wa sekta katika Pato la Taifa, kasi ya ukuaji wa sekta kwa mwaka, uhakika wa chakula, kuimarisha kilimo cha umwagiliaji na upatikanaji wa uhakika wa malighafi kwa ajili ya viwanda vyta mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Katika mwaka 2016/17 miradi itakayotekelawa ni pamoja na:-

(i) Kilimo cha Mpunga na Miwa

Katika Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa ulioanza kutumika mwaka 2013 mashamba makubwa 25 yaliainishwa kwa ajili ya kilimo cha mpunga na miwa. Malengo ya mfumo huo ni kuongeza uzalishaji wa mpunga kwa tani 290,000 na sukari tani 150,000 ili kutosheleza soko la ndani na kuuza ziada nje ya nchi. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 4.35 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha upatikanaji wa hatimiliki za mashamba makubwa sita yaliyoainishwa chini ya mfumo wa huo; kuwezesha upatikanaji wa mashamba mapya ya uwekezaji katika mikoa ya Katavi, Kigoma, Rukwa, Tabora; Lindi na

Ruvuma; kuandaa kanzidata na mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo kwa vijiji vinavyozunguka mashamba 12 ya uwekezaji; kupima na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo la Ludewa na Rufiji; na kutoa hatimiliki za kimila kwa wakulima wadogo (outgrowers) katika eneo la Kilombero na Rufiji Chini.

(ii) Skimu 78 za Umwagiliaji Mpunga

Mradi unalenga kuongeza uzalishaji wa mpunga kutoka wastani wa tani 4 kwa hekta hadi kufikia tani 8 kwa hekta. Mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na maghala; kuanzisha vikundi vya kilimo na kuwa na mtoa huduma binafsi kwa ajili ya kufundisha jinsi ya kusimamia kitaalam skimu za umwagiliaji. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 1.197 fedha za ndani na bilioni 13.42 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ujenzi wa skimu 63 za umwagiliaji na maghala 53 katika skimu za mpunga; mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji; kukamilisha ujenzi wa skimu 18 za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 18,498 katika wilaya za Mbarali (8), Iringa vijijini (4), Mpanda (2), Mlele (1), Mvomero (1) na Morogoro Vijijini (1); kukamilisha ujenzi maghala sita (6) katika skimu za Mkula (Kilombero), Mkindo (Mvomero), Uturo (Mbarali), Lake tatu (Arumeru), Mombo (Korogwe) na Bagamoyo (Bagamoyo) yanayojengwa kupitia mradi wa PHRD; kuanza ujenzi wa maghala mawili (2) ya Kiloka (Kilosa) na Tulo (Kongwa) na kukamilisha ujenzi wa skimu nne (4) za Mkula (Kilombero), Mkindo (Mvomero), Kiroka (Kilosa) na Tulo (Kongwa).

(iii) Kilimo cha Mahindi

Mfumo wa Matokea Makubwa Sasa uliweka lengo la kujenga maghala 275 ya masoko (Collective Warehouse Based Marketing schemes-COWABAMA) kwa ajili ya mazao ya mahindi katika skimu za umwagiliaji zilizopo katika maeneo mbalimbali nchini. Mradi unalenga kuongeza uzalishaji wa mahindi kwa tani 100,000 ili kukidhi mahitaji ya chakula nchini na kuuza ziada nje ya nchi. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 7.27 fedha za ndani na bilioni 10.55 fedha za nje kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maghala na masoko ya kimkakati ya Mulongo, Sirari, Kabanga, Kahama na Kyerwa; ukarabati wa maghala matano katika skimu za umwagiliaji za Njage, Msolwa, Mvumi, Kigugu na Mbogo zilizopo katika mikoa ya Manyara na Tabora; ununuzi wa vifaa katika maghala 98 ya COWABAMA yaliyopo katika halmashauri 12 nchini; upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maghala katika

mikoa 12 ya Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati na Kanda ya Magharibi; na ukarabati wa magahala 26 katika maeneo yenyé uzalishaji mkubwa.

(iv) Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji

Mradi unalenga kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ili kufikia lengo la hekta milioni moja za umwagiliaji. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 3.887 fedha za ndani na shilingi bilioni 12.02 fedha za nje kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mabwawa saba (7) ya Lwanyo (Mbarali), Mitumbati (Nachingwea), Dongobeshi (Hanang), Kongogo (Bahi), Itagata (Manyoni), Tlawi (Mbulu) na Kasoli (Bariadi); kukamilisha ujenzi skimu 19 za umwagiliaji zenyé jumla ya hekta 10,114 za Namhula (Bunda), Mlandala (Iramba), Rabour (Rorya), Mgambazi na Nyanganga (Uvinza), Kimbande (Nyasa), Kilya na Inamforo (Mwanga), Uhelela (Bahi), Budushi (Nzega), Mwalunili na Igurubi (Igunga), Nyida (Shinyanga), Usoke Mlimani (Urambo), Ngage (Simanjiro), Lutubiga (Busega), Katunguru (Sengerema), Igongwa (Misungwi) na Endagaw (Hanang); kupitia Mpango Kabambe wa Taifa wa umwagiliaji; upembuzi yakinifu wa mabwawa 39 ya umwagiliaji; ujenzi wa skimu za Mbogo na Kigugu (Mvomero) na ukarabati wa skimu za Msolwa - Ujamaa na Njage (Kilombero) na skimu katika shamba la mbegu la Kilangali (Kilosa); na kuhamasisha matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi katika skimu 8 za umwagiliaji kwenye maeneo kame.

(v) Ujenzi na Ukarabati wa Maghala

Mamlaka ya Taifa ya Hifadhi ya Chakula - NFRA imelenga kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao ili kuendana na kasi ya uzalishaji na kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa. Mradi unalenga kuongeza uwezo wa NFRA wa kuhifadhi mazao kutoka tani 246,000 hadi tani 496,000 za nafaka katika kanda za: Arusha (Babati), Dodoma (Dodoma), Makambako (Makambako na Mbozi), Shinyanga (Shinyanga), Songea (Songea) na Sumbawanga (Sumbawanga na Mpanda). Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 61.75 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa maeneo na kukamilisha taratibu za kupata wakandarasi wa ujenzi na kuanza ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa (Silos). Aidha, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ghala la Mbozi lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 za nafaka.



Muonekano wa vihenge vya kisasa - silo complex zitakazojengwa na NFRA

(vi) Kambi ya Vijana ya Kilimo Mkongo - Rufiji

Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuimarisha kambi ya vijana ya Mkongo – Rufiji iliyopo chini ya Mamlaka ya Uendelezaji Bonde la Rufiji (RUBADA). Kazi zitakazotekelawa ni: kuandaa shamba la kilimo la ekari 220, kujenga miundombinu ya umwagiliaji, kupima na kupata hatimiliki, na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana.

(vii) Tafiti za kilimo

Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 854 fedha za ndani na shilingi milioni 53 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha vituo vya utafiti. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na kuzalisha tani 10 za mbegu mama za mpunga; kutafiti teknolojia za kilimo kwa kuzingatia mnyororo wa thamani kwa mazao ya kipaumbele; kukarabati na kuimarisha vituo 12 vya Utafiti nchini; na kuboresha aina 13 za mbegu ya mpunga.

(d) Mifugo

Katika mwaka 2016/17 miradi itakayotekelawa chini ya programu ya kuendeleza sekta ya Kilimo (Agricultural Sector Development Program - ASDP II) ni pamoja na:

(i) Mradi wa Kuimarisha Uzalishaji Katika Sekta ya Mifugo

Mradi unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo yenyewe ubora wa kukidhi viwango vya soko la ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi milioni 791.55 fedha za ndani kwa ajili ya kuimarisha Vituo vya Taifa vya Uhimilishaji (National Artificial Insemination Centre) vya Usa – River (Arusha) na Sao Hill (Iringa); kununua mitamba ili kuimarisha mashamba matano (5) ya kuzalisha mitamba ya Sao Hill, Kitulo, Mabuki, Ngerengere na Nangaramo; kuwezesha NARCO kuendelea na ujenzi wa machinjio ya Ruvu na kununua ng'ombe 1,200; kuanzisha mfumo wa taarifa za mazao ya nyama na maziwa; na kutoa mafunzo kwa wazalishaji na wasindikaji wa maziwa. Aidha, shilingi milioni 208 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa minada miwili (2) ya upili ya Longido na Kirumi na ukarabati wa minada ya Nyamatala na Kasesya ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli.

(ii) Miundombinu ya Maji na Maeneo Malisho

Mradi unalenga kuainisha na kutenga maeneo ya maji na malisho kwa ajili ya mifugo ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa malambo matano (5) ya maji ya mifugo katika wilaya za Lindi, Chunya, Kilindi, Kilosa na Rufiji; kuainisha, kutenga na kupima maeneo ya malisho katika vijiji 50 vya wilaya zenyeye mifugo mingi; kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo yatakayotengwa kwa ajili ya mifugo; kutambua na kutenga maeneo ya nyanda za malisho katika vijiji 50 vya Wilaya za Kilosa, Ngorongoro, Mvomero, Mpanda, Kaliua, Kilombero, Iramba, Kiteto, Igunga, Lindi na Kilindi; na kukarabati miundombinu katika mashamba nane (8) ya malisho.

(iii) Vituo vya Mafunzo na Tafiti za Mifugo na Uvuvi

Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 1.65 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu (3) katika kampasi za Madaba na Kikulula; ukarabati wa darasa moja na hosteli katika Chuo cha Mafunzo ya Mifugo – Morogoro; ukarabati wa maktaba katika vyuo vya Mabuki na Kikulula na kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ili kuongeza wataalam wa uvuvi na teknolojia mbalimbali kuhusu uvuvi na ufugaji wa samaki.

(e) Uvuvi

i. Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi

Mradi unalenga kujenga bandari ya uvuvi ambayo itawezesha meli zinazovua katika bahari kuu kutia nanga nchini ili kuwezesha Serikali kusimamia kwa ufanisi uvuvi katika bahari kuu. Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 500 fedha za ndani na shilingi milioni 24 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu ili kubaini eneo ambalo litafaa kwa ujenzi wa bandari kati ya maeneo mawili (2) yaliyopendekezwa ya Mikindani (Mtwara) na Bagamoyo (Pwani).

ii. Uzalishaji wa Samaki

Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 1 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.5 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha ufugaji wa samaki wa maji baridi katika vituo vitano (5) vya kuzalisha vifaranga vya samaki vya Mwamapuli - Tabora, Ruhila - Songea, Kingolwira - Morogoro, Nyigedi - Lindi na Nyamirembe - Chato na vituo viwili (2) vya samaki wa maji chumvi vya Machui - Tanga na Mbegani - Bagamoyo.

iii. Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi

Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi milioni 400 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.2 fedha za nje kwa ajili kukabiliana na tatizo la uvuvi haramu ambao kwa kiwango kikubwa unahatarisha ustawi wa sekta ya uvuvi.

4.3.3 Miundombinu

A. Reli

a. Ukarabati wa Reli ya kati

(i) Kubadilisha mataruma ya reli na kuweka reli nzito ya kiwango cha ratili 80 kwa yadi

Mradi unalenga kukarabati reli ya kati kwa kubadilisha reli iliyopo na kuweka reli yenye uzito wa ratili 80 kwa yadi ili kuongeza ufanisi. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 47.9 fedha za ndani na shilingi bilioni 57.1 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya malipo ya awali ya mikataba ya kutandika reli nzito za ratili 80 kwa yadi kati ya Lulanguru na Tabora (km 61); kubadilisha km 283 za reli ya kati sehemu ya Dar es Salaam - Kilosa na Tabora-Isaka (km 130); malipo ya awali ya kununulia vipuri vya mtambo wa kuzalisha kokoto wa Tura; ununuzi wa mtambo wa kukagua na kupima njia ya reli; na shughuli za uzalishaji wa mataruma katika Karakana ya Pugu.

(ii) Ukarabati na Ununuzi wa Vichwa vya Treni, Mabehewa na

Vifaa Mbalimbali.

Mradi unalenga kuboresha huduma ya uchukuzi wa abiria na mizigo katika reli ya kati kwa kuimarisha ufanisi na utendaji kazi wa Shirika la Reli Tanzania (TRL). Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 5 kwa ajili ya: kuendelea na uzalishaji upya wa injini za treni katika karakana ya Morogoro; ukarabati wa viberenge na treni za kufanya ukaguzi wa reli; na kukamilisha ununuzi wa mabehewa 22 ya mizigo.

(iii) Ukarabati na uboreshaji wa matawi ya reli ya kati

Mradi unalenga kujenga na kukarabati matawi ya reli ya kati ili kuboresha ufanisi na usalama wa huduma za reli. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya: kutandika reli katika njia ya reli ya Kaliua – Mpanda (km 185) na kujenga daraja moja na makalavati matatu (km 154, km 162, na km 174); na ukarabati wa stesheni na ujenzi wa jengo la kuhifadhi mizigo katika stesheni ya Mpanda.

(iv) Ukarabati wa Njia Kuu ya Reli

Mradi unalenga kukarabati miundombinu na mawasiliano katika njia kuu ya reli ya kati ili kuboresha ufanisi. Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 70.7 fedha za ndani na shilingi bilioni 11 fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Shughuli zitakazotekelzwa ni:-

- Ujenzi wa daraja na matengenezo ili kuzuia tatizo la mafuriko katika maeneo yaliyoathiriwa na mvua kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe na uharibifu wa miundombinu ya reli kati ya stesheni za Godegode na Gulwe,
- Upembusi yakinifu kwenye eneo la km 60 kwa ajili ya kutafuta suluhisho la kudumu kwa eneo linaloathirika mara kwa mara na mafuriko kati ya Kilosa - Gulwe,
- Ujenzi wa madaraja 10 kati ya 38 yaliyo katika hali mbaya katika njia ya Tabora – Kigoma,
- Usanifu na kuanza ujenzi wa madaraja na makalavati 38 yenye uwezo wa tani 25 yaliyo katika hali mbaya kati ya Dar es Salaam – Isaka,
- Kujenga daraja katika eneo la Godegode,
- Kuboresha mfumo wa mawasiliano (awamu ya kwanza) kati ya Dar es Salaam – Dodoma, Tabora – Kigoma, Tabora- Mwanza na Kaliua - Mpanda,
- Kuweka mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia mizigo katika reli (Electronic cargo tracking system), na

- Ujenzi wa mabwawa mawili (2) katika eneo la Godegode - Gulwe na Msagai (km 384).

(v) Ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha - Musoma (km 1,105) pamoja na matawi ya Minjingu na Engaruka

Mradi unalenga kujenga reli ya Tanga – Arusha (km 435) na Arusha – Musoma (km 670) pamoja na matawi mapya ya kuelekea Minjingu na Engaruka kwa kiwango cha standard gauge. Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 9.7 kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa kina wa ujenzi wa njia ya reli kati ya Tanga – Arusha; kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia ya reli kwa kiwango cha standard gauge kati ya Arusha – Musoma, pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu; kuweka mawe 27,070 ya mipaka katika njia na stesheni za reli; kupima viwanja vya reli na kuweka alama na uzio katika maeneo hayo; na kuandaa Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Reli (Railway Master Plan).

(vi) Mradi wa Reli Mtwara – Mbamba Bay na Mchuchuma – Liganga (km 1,000)

Mradi unalenga kujenga njia ya reli kwa kiwango cha standard gauge kati ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi yake kwenda Mchuchuma na Liganga ili kuboresha huduma za uchukuzi wa reli katika ukanda wa Mtwara. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 5 kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali na kumpata mtalaam Elekezi atakayesimamia upatikanaji wa fedha pamoja na ujenzi wa reli.

b. Usafiri wa Treni Dar es Salaam

Mradi unalenga kuboresha usafiri wa abiria na kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 7.5 kwa ajili ya: upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia mpya za reli zikiwemo za maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Bagamoyo; na ujenzi wa mchepuo wa njia ya reli kutoka “Ilala block post” hadi Stesheni ili kuepusha mwingiliano wa treni ya abiria kutoka Stesheni kwenda Ubungo na ile ya mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam.

B. Barabara na Madaraja

Miradi ya barabara na madaraja inatekelezwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa upande wa barabara kuu na za mikoa, utekelezaji wa miradi

ya vivuko na maegesho unaratibiwa na wakala wa ufundu na umeme (TEMESA).

a. Barabara zenyе kufungua fursa za Kiuchumi

- (i) **Barabara ya Itoni – Mkiu – Ludewa – Manda (km 211):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Itoni – Mkiu - Ludewa – Manda (km 211) kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 35.3 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Lusitu – Mawengi yenye urefu wa kilomita 50.
- (ii) **Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 359):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 260) na Tabora – Sikonge – Ipole (km 99) kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili; Tabora – Sikonge (Tabora – Usesula – km 30) na Usesula – Sikonge – Ipole – Koga – Mpanda (km 329). Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 28.6 fedha za ndani na shilingi bilioni 92.3 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kulipa fidia sehemu ya Mpanda – Koga – Ipole; kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tabora – Sikonge – Ipole (Sehemu ya Tabora – Usesula, km 30); na kuanza ujenzi wa sehemu nyingine za barabara hiyo.
- (iii) **Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Rungwa – Itigi - Mkiwa (km 528):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Mbeya hadi Makongolosi (km 115) pamoja na barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (Km 413) kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Mbeya – Lwanjilo (km 36); Lwanjilo-Chunya (km 36) na Chunya – Makongolosi (km 43) kwa barabara ya Mbeya hadi Makongolosi (km 115). Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 45.1 zimetengwa kwa ajili ya: kulipa sehemu ya madai ya wakandarasi wa barabara ya Mbeya – Lwanjilo na Lwanjilo – Chunya; na kuanza ujenzi wa sehemu ya barabara ya Chunya – Makongolosi na sehemu ya Itigi – Mkiwa (km 35).
- (iv) **Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za ndani. Ujenzi wa barabara hii umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35); Tabora – Nyahua (km 85); na Nyahua - Chaya (km 90). Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 79.5 zimetengwa kwa ajili ya: kuendelea na ujenzi wa sehemu za Tabora – Nyahua na Manyoni – Itigi

- Chaya pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nyahua – Chaya.
- (v) **Barabara ya Dodoma – Babati (km 261):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati (km 261) kwa kiwango cha lami. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu nne ambazo ni: Dodoma – Mayamaya (km 43), Mayamaya – Mela (km 99.35), Mela – Bonga (km 88.8) na Bonga – Babati (km 19.2). Ujenzi wa sehemu ya Bonga – Babati ulikamilika Aprili, 2013 na sehemu ya Dodoma – Mayamaya unaendelea; ujenzi wa sehemu hizi mbili unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Aidha, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mayamaya – Bonga (km 188.15) zinaendelea kwa fedha za mkopo nafuu kutoka AfDB na JICA. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 19.26 fedha za ndani na shilingi bilioni 61.8 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Dodoma – Mayamaya, Mayamaya – Mela na Mela – Bonga.
- (vi) **Barabara ya Iringa – Dodoma (km 260):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Dodoma – Mtera – Iringa (km 260) pamoja na barabara ya mchepuo ya Iringa (*Iringa Bypass*) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni: Iringa – Migori (km 95.2); Migori – Fufu Escarpment (km 93.8) na Fufu Escarpment – Dodoma (km 70.9). Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 7.4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya; kulipa sehemu za madai ya Wakandarasi wa barabara ya Migori – Fufu Escarpment, Iringa-Migori na Fufu Escarpment – Dodoma pamoja na kuanza ujenzi wa Iringa bypass.
- (vii) **Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo - Mto wa Mbu (km 338):** Mradi unalenga kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii unatekelezwa kwa sehemu tatu: sehemu ya Loliondo – Mto wa Mbu (km 213) na Makutano – Natta – Mugumu (km125). Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 20 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano – Sanzate na kuanza ujenzi sehemu ya Mto wa Mbu – Loliondo.

(viii) Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (Km

491): Mradi unalenga kujenga kwa kiwango cha lami barabara kati ya Kigoma na Tabora (km 443), ujenzi wa daraja la Mto Malagarasi na barabara za maingilio ya daraja (km 48). Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa barabara za Kidahwe – Uvinza (km 76.6), Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52), Kaliua – Kazilambwa (km 56), Uvinza – Malagarasi (km 51.10), Urambo – Kaliua (km 33) na Kazilambwa – Chagu (km 40). Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 65.5 fedha za ndani na shilingi milioni 358.26 fedha za nje zimetengwa kwa ajili: kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Ndono – Urambo na Kaliua – Kazilambwa; na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Uvinza – Malagarasi na Urambo - Kaliua.

b. Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani

(i) Barabara ya Nyanguge – Musoma (km 183) na mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17) na Bulamba – Kisorya (km 51): Mradi unalenga kukarabati barabara ya Nyanguge – Simiyu (km 80), Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5) na ujenzi kwa kiwango cha lami ya mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17). Aidha, mradi huu unahusisha ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Nansio – Kisorya – Bunda (sehemu ya Kisorya – Bulamba (km 50)), Nyamuswa – Bulamba (km 55), Musoma - Makojo - Busekela (km 92), barabara za kupunguza msongamano katika jiji la Mwanza na barabara ya Makutano - Sirari (km 83).

Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 70.9 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Nyangunge – Simiyu/Mara Border; kuendelea na kazi za ujenzi katika sehemu ya Kisesa – Usagara bypass na barabara ya Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba); kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara za Nyamuswa – Bulamba, Musoma – Makojo – Busekela, Makutano – Sirari na barabara za kupunguza msongamano katika jiji la Mwanza.

(ii) Barabara ya Marangu – Tarakea – Kamwanga/Bomang’ombe – Sanya Juu (Km 173), Arusha – Moshi – Holili (Km 140), KIA - Mererani (26), Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (Km 16.0) na Kiborloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (Km 10.8): Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 46 fedha za ndani na shilingi bilioni 55.4 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipia sehemu ya malipo ya mwisho ya Wakandarasi wa barabara za Rombo Mkoo – Tarakea, Marangu – Rombo Mkoo, Kwa Sadala – Masama - Machame

Jct, Kiborloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia na Mwika – Kilacha; ujenzi wa njia nne kutoka njia mbili za sasa za barabara ya Arusha – Moshi – Holili/Taveta – Voi sehemu ya Sakina – Tengeru (km 14.10) na njia mbili kwa sehemu ya Arusha Bypass (km 42.41); kuendelea na ujenzi wa barabara ya KIA – Mererani; na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Sanya Juu – Kamwanga.

- (iii) **Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242), Lusahunga – Rusumo (km 92) na Nyakasanza – Kobero (km 60):** Mradi unalenga kukarabati wa sehemu ya Isaka – Lusahunga (km 242) kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanyika katika sehemu nne ili kuharakisha utekelezaji: Isaka – Ushirombo (km 132), Ushirombo – Lusahunga (km 110), Lusahunga - Rusumo (km 92) na Nyakasanza - Kobero (km 60). Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 56.4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa malipo ya mwisho ya madai ya mkadarasi wa sehemu ya Isaka – Ushirombo pamoja na mkandarasi wa Rusumo *One Stop Border Post*; kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga; maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero na maandalizi ya ujenzi wa mizani ya kupima magari huku yakitembea (Weigh in Motion Scale) sehemu ya Mwendakulima (Kahama).
- (iv) **Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112) kwa kiwango cha lami. Aidha, unahuishisha usanifu na ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 43.6 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kassanga Port na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya.
- (v) **Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 346.6):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Kidahwe (km 438) kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 77.5 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi sehemu za Sumbawanga – Kanazi (Km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Kizi – Sitalike - Mpanda (km 95) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Mpanda – Mishamo (km 100).
- (vi) **Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 171.8):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Mwigumbi – Maswa –

Bariadi – Lamadi (km 171.8) kwa kiwango cha lami. Kazi za ujenzi zimekamilika kwa sehemu ya Bariadi – Lamadi (km 71.8) na zinaendelea kwa sehemu ya Mwigumbi – Maswa (km 50). Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 46.9 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya mwisho ya mkandarasi wa barabara ya Bariadi – Lamadi na kuendelea na ujenzi sehemu ya Bariadi – Lamadi na sehemu ya Mwigumbi – Maswa.

c. Barabara za Mikoa

Mradi unalenga kukarabati na kuboresha barabara zinazounganisha mikoa nchini. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 30 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa jumla ya kilomita 632.05 kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilomita 23.25 kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja 15.

d. Barabara za Kupunguza Msongamano Mijini (km 111.85)

Mradi unalenga kujenga, kupanua na kukarabati barabara za jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 38.9 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kama ifuatavyo:-

- (i) Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley –Jangwani/Twiga Jct (km 2.7), shilingi milioni 781 zimetengwa kwa ajili ya kumalizia kazi zilizobakia;
- (ii) Tabata Dampo – Kigogo na Ubungo Maziwa – External (km 2.25), shilingi bilioni 2.69 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa sehemu ya Tabata Dampo-Kigogo (km 1.65) na kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa eneo la Ubungo Maziwa – External;
- (iii) Kimara – Kilungule – External/Mandela Road (km 9), shilingi bilioni 4.14 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara;
- (iv) Mbezi (Morogoro Road) –Malamba Mawili – Kinyerezi – Banana (km 14), shilingi bilioni 4.16 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara;
- (v) Tegeta – Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi Mwisho (km 20), shilingi bilioni 4 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi sehemu ya Goba – Mbezi Mwisho (km 7);
- (vi) Tangi Bovu – Goba (km 9), shilingi bilioni 3.39 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi;
- (vii) Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6), shilingi bilioni 1.72 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi;
- (viii) Kibamba – Kisopwa (km 12.0), shilingi bilioni 3.8 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa sehemu ya Kibamba-Mlonganzila (km 4) na kuendelea na ujenzi kwa sehemu iliyobaki;

- (ix) Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7), shilingi bilioni 2.58 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara sehemu ya Kitunda – Moshi Bar (km 3.2);
- (x) Ardhi – Makongo, shilingi bilioni 2.58 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi;
- (xi) Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda (km 2.5), shilingi bilioni 2.58 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea ujenzi.
- (xii) New Bagamoyo (Kawawa Junction – Mwenge-Tegeta: km 17), shilingi bilioni 2.14 zimetengwa amapo bilioni 1.14 ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi sehemu ya Kawawa Junction – Mwenge-km 4.2) na shilingi bilioni 1 ni kwa ajili uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua.
- (xiii) Mwai Kibaki (Old Bagamoyo), shilingi bilioni 4 zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara.

e. Ujenzi wa Barabara za Juu

Mradi unalenga kujenga 'Flyover' ya TAZARA ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Utekelezaji utahusisha: makutano ya barabara za Mandela na Nyerere; kujenga 'Flyover' ya Ubungo kwenye makutano ya barabara za Morogoro na Mandela/Sam Nujoma; kujenga kwa utaratibu wa Usanifu na Kujenga (Design and Build) barabara za juu na kuboresha makutano ya Chang'ombe, Magomeni/Nyerere, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco na maandalizi ya upanuzi wa barabara ya TAZARA – JNIA kuwa njia 6. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 36.7 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii.

(i) Flyover ya TAZARA

Mradi unahusisha ujenzi wa 'flyover' katika makutano ya barabara za Mandela na Nyerere ili kukabiliana na msongamano wa magari. Mradi unatekelezwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa fedha za Serikali pamoja na fedha za msaada kutoka Serikali ya Japan. Mkataba wa ujenzi wenyewe thamani shilingi bilioni 87.156 ulisainiwa Oktoba, 2015 baina ya Serikali na mkandarasi kampuni ya M/s Sumitomo Mitsui Construction Co. Ltd ya Japan na utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 35. Usimamizi wa mradi utafanywa na kampuni za M/s Oriental Consultants Co. Ltd na Eight – Japan Engineering Consultants Inc zote za Japan; mkataba wa usimamizi wa mradi ulisainiwa Oktoba, 2013 na una thamani ya shilingi bilioni 6.28. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 3.98 fedha za ndani na bilioni 16.28 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Flyover ya TAZARA.

(ii) **Flyover ya Ubungo**

Mradi unahusisha ujenzi wa barabara za juu (interchange) katika makutano ya barabara za Morogoro na Mandela eneo la ubungo ili kukabiliana na msongamano wa magari. Mradi unatekelezwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa fedha za Serikali pamoja na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 15 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya malipo ya awali ya Mkandarasi wa ujenzi.



Muonekano wa barabara za juu eneo la ubungo zitakavyoonekana baada ya kukamilika.

(iii) **Maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni/Nyerere, Mwenge, Tabata/Mandela na Kawawa/Morocco**

Mradi unahusisha maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni/Nyerere, Mwenge, Tabata/Mandela na Kawawa/Morocco kwa utaratibu wa usanifu na kujenga (design and Build). Mradi unalenga kuimarisha uchukuzi Dar-es-Salaam na kupunguza msongamano wa magari. Ujenzi wa flyovers kwa awamu unatarajia kuanza baada ya kukamilika kwa maandalizi ya ujenzi (upembuzi yakinifu na usanifu wa kina) na kupatikana kwa fedha za ujenzi. Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 750 zimetengwa kwa ajili ya maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu (Kurasini) na Morocco.

(iv) Barabara ya TAZARA – Uwanja wa Ndege wa J. K. Nyerere (km 6)

Mradi unatekelezwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) na unahusisha upanuzi wa barabara ya TAZARA - Uwanja wa Ndege (km 6) kutoka njia nne zilizopo sasa na kuwa njia sita (6 lanes) ili kukabiliana na msongamano wa magari. Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 750 zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya upanuzi wa barabara ya TAZARA – JNIA kuwa njia 6.

f. Mradi wa Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 200) Sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 100)

Mradi unalenga kujenga barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200) sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 100) kwa viwango vya "Expressway". Aidha, mradi huu unahusisha ukarabati wa sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24). Mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi - Public Private Partnership (PPP), kwa sasa upo katika hatua ya upembuzi yakinifu unaofanywa na Kampuni ya Cheil Engineering Company Limited ya Korea ambayo ndiye Mshauri Mwelekezi (Transaction Adviser). Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 12.62 kwa ajili ya: kukamilisha upembuzi yakinifu na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze km 100; na ukarabati wa sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24).

g. Madaraja

i. Madaraja ya njia kuu

Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 47.23 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa madaraja mbalimbali Nchini. Madaraja hayo ni: Daraja la Kirumi (Mara), Daraja la Nangoo kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru, Daraja la Sibiti kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti, Daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge, Daraja la Kavuu kwenye barabara ya Majimoto – Inyonga, Daraja la Mbutu kwenye barabara ya Igunga – Manonga, Daraja la Ruhekei katika barabara ya Mbanga – Mbamba Bay, Daraja la Ruhuhu (Ruvuma), Daraja la Momba kwenye barabara ya Sitalike – Kilyamatundu/Kamsamba – Mlowo (Rukwa/Mbeya Border), Daraja la Simiyu kwenye barabara Mwanza – Musoma, Daraja la Wami barabara ya Chalinze – Segera, Daraja la Lukuledi II kwenye barabara Matama – Kitangali – Newala, Daraja Jipyia la Selander, Daraja la Mlalakuwa,

ii. Daraja la Mwalimu Nyerere - Kigamboni

Mradi unalenga kujenga daraja la Mwalimu Nyerere - Kigamboni pamoja na

barabara za maingilio ya daraja (approach roads) kwa ajili ya kuunganisha eneo la Vijibweni (kwa upande wa Kigamboni) na Kurasini katika bahari ya Hindi. Barabara za maingilio ya daraja ni pamoja na Mjimwema – Vijibweni (km 10), Tungi – Kibada (km 3.8) na Kibada – Mjimwema (km 1.8). Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 27.2 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya malipo ya mkandarasi wa ujenzi wa daraja na kuanza ujenzi wa barabara za maingilio.

C. **Bandari**

Miradi hii inahusisha pia ujenzi wa bandari mpya (Mbegani na Mwambani) ili kukidhi mahitaji ya sasa na baadaye pamoja uboreshaji wa miundombinu ya bandari zilizopo ili kuongeza uwezo wa bandari hizo kuhudumia mizigo (throughput) pamoja na ufanisi wake. Miradi hii inatekelezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) .

i. **Bandari ya Dar es Salaam**

Bandari ya Dar-es-Salaam ni moja ya bandari muhimu katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kutokana na kuhudumia kwa kiasi kikubwa Nchi za ukanda huu ambazo hazina bahari (Rwanda, DRC, Burundi, Uganda, Zambia na Malawi). Katika kuboresha uwezo na utendaji kazi wa bandari Serikali pamoja na jitihada nyingine inatekeleza miradi ifuatayo:- (a) ujenzi wa gati Na. 13 na 14 katika, (b) uboreshaji wa gati Na. 1 – 7, (c) kuongeza kina cha bahari na kupanua lango la kuingilia meli,na (d) kuboresha mfumo wa uondoshaji mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa kuweka mfumo wa “electronic single window System”. Miradi hii inatekelezwa kwa fedha za Mamlaka ya Bandari pamoja na mkopo kutoka Benki ya Dunia, Department for International Development (DfID) ya Uingereza na Trade Mark East Africa (TMEA) na inategemea kugharimu dola za Kimarekani milioni 600.

- a) **Ujenzi wa gati Na. 13 na 14:** Mradi huu unahusisha ujenzi wa gati mpya mbili (2) kwa ajili ya kuhudumia shehena za makontena. Mradi unalenga kuongeza uwezo wa bandari ya Dar-es-Salaam kuhudumia shehena ya makontena ili kuendana na ukuaji wa mahitaji. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2.3 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mtaalam mwelekezi (Transation Advisor) za kukamilisha maandalizi ya mradi, hususan tafiti na usanifu wa kina (detailed engineering design) ili kutoa picha halisi ya mradi na gharama zake, ikijumuisha uondoshaji wa gati la mafuta (KOJ) na mabomba yake katika eneo linalotarajiwa kujengwa gati namba 13 na 14.

- b) Uboreshaji wa gati Na. 1 – 7:** Mradi huu unahusisha uboreshaji wa gati na 1-7 kwa kuongeza kina, kujenga magati ya kuhudumia mizigo maalum (gati za mizigo ya mchanganyiko-general cargo, gati la kuhudumia shehena za mbolea na nafaka na gati za kushusha magari - RoRo) na kubadilisha gati na 5-7 kuwa gati za makontena. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 30 fedha za ndani na shilingi bilioni 66 fedha za nje kwa ajili ya kuimarisha na kuongeza kina cha gati Na. 1 – 7.
- c) Kuongeza Kina cha Bahari na Kupanua Lango la Kuingilia Meli:** Mradi unalenga kuongeza kina cha bahari pamoja na upana wa lango la kuingilia meli ili kuruhusu meli kubwa zaidi kuingia na kutoka kirahisi katika bandari ya Dar es Salaam. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 96.2 fedha za nje kwa ajili kuanza utekelezaji wa mradi.

ii. Ujenzi wa Bandari ya Mwambani - Tanga

Mradi huu unahusisha ujenzi wa bandari mpya katika eneo la Mwambani (Tanga). Mradi unalenga kuongeza uwezo wa nchi kuhudumia shehena ya mizigo ili kukidhi ukuaji wa mahitaji. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 2 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kuzingatia ujenzi wa reli mpya (Tanga – Arusha - Musoma).

iii. Ujenzi wa bandari ya Mtwara

Mradi huu unahusu ujenzi wa gati nne (4) mpya katika bandari ya Mtwara ili kuongeza uwezo wa bandari hiyo kuhudumia shehena ya mizigo kuendana na ukuaji wa mahitaji unaotokana kwa kiwango kikubwa na shughuli za uendelezaji wa gesi na mafuta Lindi na Mtwara. Mamlaka ya Bandari Tanzania inaendelea na kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya kutekeleza mradi huu kwa awamu. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Mamlaka ya Bandari Tanzania itaanza ujenzi wa gati moja (1) lenye urefu wa mita 300 kwa ajili ya kuhudumia Shehena mchanganyiko (Multi-Purpose Terminal). Gati zingine tatu zitatekelezwa katika awamu ya pili kwa kushirikiana na washirika mbalimbali wa maendeleo na sekta binafsi.

iv. Bandari za Maziwa Makuu

Malengo ni kuboresha miundombinu ya bandari zilizopo katika maziwa makuu (Viktoria, Tanganyika na Nyasa) ili kuboresha huduma za uchukuzi katika maziwa hayo.

- (a) **Ziwa Viktoria;** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 3.05 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa 'Dhow Wharves' ya Mwigobero, upimaji na utoaji fidia kwenye gati la Kyamkwikwi, Lushamba, na Ntama, ujenzi wa gati la Chato, uongezaji kina katika Bandari ya Nansio na Mwanza South na Ukarabati wa 'Link Span' ya bandari ya Mwanza South.
- (b) **Ziwa Tanganyika;** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 10.1 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya uboreshaji wa maegesho ya meli (gati) za kuhudumia abiria pamoja na mizigo katika miji ya Lagosa, Sibwesa, pamoja na Kibirizi, upembuzi yakinifu katika bandari ya Karema pamoja na miundombinu ya barabara kuelekea katika bandari ya Kipili.
- (c) **Ziwa Nyasa;** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 10.8 fedha za ndani kwa zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati la Mbamba Bay, ujenzi wa gati la Ndumbi na ujenzi wa sakafu (pavement) katika bandari ya Kiwira kwa ajili ya maegesho ya vifaa, mizigo na magari.

v. Ununuzi wa vifaa vya kuhudumia meli na mizigo katika bandari zote

Mradi unalenga kununua vifaa vya kuhudumia meli na shehena ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma, kuimarisha usalama wa wafanyakazi na kutoa ulinzi katika bandari zetu. Katika mwaka 2016/2017 shilingi bilioni 77.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa mbalimbali vya kuhudumia meli na shehena, magari ya utawala, vifaa vya ulinzi na usalama bandarini, mitambo mbalimbali ikiwemo ya kuzalisha umeme, boti za kuongozea meli na mizani za kupimia uzito.

D. Usafiri wa Majini

(a) Vivuko na Maegesho

Mradi hii inahusisha ujenzi wa maegesho (landing ramps), ukarabati wa vivuko vilivyopo pamoja na ununuzi wa vivuko vipyta ili kuboresha huduma ya uchukuzi kuititia vivuko katika maeneo mbalimbali. Miradi hii inatekelezwa na Wakala wa Serikali wa Umeme na Ufundji (TEMESA).

- (i) Ujenzi wa maegesho ya vivuko:** Mradi unalenga kujenga na kukarabati maegesho (landing ramps) ili vivuko viweze kuegesha na kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye vivuko kwa urahisi nyakati zote za mwaka. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 9 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa maegesho na majengo ya abiria ya kivuko cha Dar-es-Salaam - Bagamoyo (Pwani), upanuzi wa Maegesho ya Kigamboni, ujenzi wa maegesho ya Bwina ya kivuko cha Chato –

Nkome na ujenzi wa maegesho ya Lindi – Kitunda.

- (ii) **Ununuzi wa vivuko vipyta:** Mradi unalenga kuboresha huduma za uchukuzi wa vivuko katika maeneo mbalimbali. Mradi unatekelezwa na TEMESA na unahusisha ununuzi wa vivuko vipyta, vitendea kazi vya karakana za TEMESA pamoja na mashine za kisasa za kukatia tiketi katika vivuko mbalimbali. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 6.05 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vivuko viwili (2) vitakavyofanya kazi kati ya Kigamboni – Magogoni na Kigongo – Busisi; ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA; ununuzi wa boti za abiria katika vivuko vya Kilambo – Namoto na Mkongo – Utete. Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 411.7 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II (Tanga) na MV Sengerema.

E. Usafiri wa anga

- (i) **Ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa Julius Nyerere:** Mradi huu unahusisha ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Mwl Julius Nyerere; jengo la abiria linatarajiwa kuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 6 kwa mwaka. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 26 fedha za ndani na shilingi bilioni 32 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake.
- (ii) **Kiwanja cha ndege cha Kimataifa Kilimanjaro:** Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 10 za fedha za ndani na bilioni 40 fedha za nje kwa utekelezaji wa mradi huu. Shughuli zitakazotekelawa nii pamoja na ya ukarabati na upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, barabara za viungio, jengo la abiria, ujenzi wa barabara mpya ya kiungio, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ujenzi wa mfumo mpya wa maji taka.
- (iii) **Ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Msalato:** Mradi unalenga ujenzi wa kiwanja kipyta cha ndege cha kimataifa katika eneo la Msalato, Dodoma. Katika mwaka 2016/17 shilingi milioni 70 fedha za ndani na shilingi bilioni 2 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya usanifu wa kina wa ujenzi wa kiwanja.
- (iv) **Kiwanja cha ndege Mwanza:** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni

25.1 fedha za ndani na shilingi bilioni 5 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Shughuli zitakazotekelozwa ni: kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria na kuendelea na kazi za kurefusha na kujenga barabara ya kuruka na kutua ndege (runway), ujenzi wa jengo la mizigo (Cargo terminal), maegesho ya ndege na viungio vyake, jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua.

- (v) **Kiwanja cha ndege cha Songwe:** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 10 fedha za ndani kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Jengo la Abiria na mifumo yake, usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na ulipaji wa madeni.
- (vi) **Kiwanja cha ndege Kigoma:** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2.7 za fedha za ndani na shilingi bilioni 4.2 za fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka), usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, kujenga uzio, na ujenzi wa jengo la uchunguzi wa hali ya hewa (OBS).
- (vii) **Kiwanja cha ndege Tabora:** Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 3.1 fedha za ndani na shilingi bilioni 4.6 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake (barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari), ukarabati wa njia ya pili ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa (OBS), maegesho ya ndege pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.
- (viii) **Kiwanja cha ndege Mtwara.** Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 10 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu na Mpango Kabambe (Concept Design & Master Plan) na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.
- (ix) **Kiwanja cha ndege Sumbawanga:** Mradi unalenga ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Sumbawanga ili kuboresha huduma za usafiri wa anga. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 5.2 fedha za ndani na shilingi bilioni 5.6 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya

ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege **kulipa fidia**.

- (x) **Kiwanja cha ndege Chato (Geita):** Mradi huu unahusisha ujenzi wa kiwanja kipycha cha ndege Chato kwa ajili ya huduma za usafiri wa anga kwa Mkoa wa Geita na maeneo ya jirani. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2 zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kiwanja.
- (xi) **Kiwanja cha ndege Shinyanga:** Mradi unalenga ukarabati na upanuzi wa **kiwanja cha ndege cha Sumbawanga ili kuboresha huduma za usafiri wa anga**. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 2 za fedha za ndani na shilingi bilioni 6.6 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa (OBS), barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, na **kulipa fidia**.

(b) Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

(i) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Mradi unalenga kuunganisha Mikoa na Wilaya zote nchini pamoja na nchi za jirani katika mkongo wa Taifa ili kuboresha upatikanaji wa huduma za uhakika za mawasiliano na matumizi ya TEHAMA. Katika mwaka wa fedha 2016/17 shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya tathimini hali ya miundombinu ya mkongo na mifumo yake ili kubaini fursa za kufanya upanuzi wa miundombinu siku za usoni; tathimini ya athari za kimazingira katika maeneo ambayo awamu za III, IV na V ya mradi wa Mkongo zitatekelezwa; usambazaji wa mitandao ya mkongo katika miji; kuendelea na uunganishaji wa mkongo wa Taifa kwa watumiaji wa mwisho; utoaji wa elimu kwa umma kuhusu matumizi na umuhimu wa Mkongo wa Taifa; na kuwezesha zoezi la kuhuisha kanuni, taratibu, miongozo, viwango na vigezo ya huduma na vifaa vya TEHAMA.

(ii) Mradi wa Program ya Miundombinu ya Kikanda (RCIP): Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 87.7 zimetengwa kwa ajili ya Kujenga uwezo wa kusimamia shughuli za miradi ya matumizi ya TEHAMA,

maboresho ya sheria, sera wezeshi kwa matumizi ya TEHAMA pamoja na mipangilio mbalimbali. Sheria za Usalama wa Mtandao (Cyber Security Laws); Ununuzi wa mkondo wa mawasiliano (*Bandwith*) unaotumika katika taasisi mbalimbali za Serikali nchini;

(iii) Mradi wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta

Mradi unalenga kuanzisha utaratibu wa kutumia anuani za makazi na simbo za posta katika kutambua maeneo mbalimbali ya mitaa. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 3 kwa ajili kufunga alama za majina ya mitaa na namba za nyumba kwa Kata 100 za Mikoa ya Dar-es-Salaam, Mwanza, Zanzibar na Mbeya; kuhamasisha na kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu mradi na faida za matumizi ya anuani za makazi na simbo za posta; kuendesha programu za kujengea uwezo watumishi kuhusu masuala ya matumizi ya anuani za makazi; kuwezesha mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta pamoja na maandalizi ya mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Posta na ufuatiliaji wa utendaji kazi wa mfumo wa Taifa anuani za makazi na simbo za posta.

4.3.4 Huduma za Fedha, Utalii, Biashara na Masoko

(i) Biashara na masoko

(a) Mradi wa Kuboresha mazingira ya uwekezaji na Biashara

Mradi unalenga kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 1.227 fedha za ndani kwa ajili ya: kuendelea kutafuta fursa nafuu za biashara na masoko kwa bidhaa za kilimo na viwandani kupitia majadiliano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa; kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kuzingatia vigezo vya tathmini ya Taasisi za Kimataifa juu ya mazingira bora ya uwekezaji (Ease of Doing Business); kuanzisha mfumo wa usajili wa leseni za biashara, kusajili makampuni, majina ya biashara, na alama za biashara kupitia mitandao ya kompyuta kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); kupitia Sera, Sheria, na Kanuni zinazokinzana katika biashara ili kurahisisha uanzishaji na uendeshaji wa biashara hususan viwanda; kuendelea kushirikiana na Tume ya Ushindani (FCC) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani usio wa haki kwa kuimarisha udhibiti wa uingizaji bidhaa hafifu, bandia au zinazoingia kwa njia zisizo rasmi bila kulipiwa kodi ili kuweka usawa katika ushindani, kumlinda mlaji na kuwezesha kukusanya kodi stahiki; na kuendelea kuimarisha utaratibu wa kutoa huduma kwa wawekezaji kwa mfumo wa One Stop

Centre ili kupunguza urasimu na gharama kwa wawekezaji kupitia TIC, BRELA na EPZA.

(b) Uendelezaji wa shughuli za masoko nchini

Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 5.120 kwa ajili ya kulipia fidia ya ardhi ya Soko la kimkakati la Makambako; kuimarisha Mifumo ya taarifa za masoko (bei, ugavi) ya mazao ya kilimo na mifugo kwa kupanua wigo wa mfumo; kuwaongezea ujuzi maafisa, kununua vitendea kazi vya wakusanya taarifa za masoko kutoka wilaya 113; kufanya uperembaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa zao la korosho katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani na katika maeneo mapya yatakayoanza kutekeleza Mfumo huo; kufanya tafiti za mwenendo wa masoko ya mazao makuu; na kuwawezesha wajasiriamali wa kilimo na mifugo kuzifikia fursa za masoko kwa kuwatengea maeneo ya kuoneshea bidhaa zao; kutoa elimu ya shughuli za viwanda na biashara katika maonesho ya wakulima, hususan matumizi ya vipimo sahihi, upangaji wa madaraja ya mazao, ufungashaji, matumizi ya mashine katika kilimo, umuhimu wa kuhifadhi mazao kwenye maghala, uchakataji wa mazao na matumizi ya nembo za mstari.

(ii) Huduma za Fedha

(a) Benki ya Rasilimali Tanzania

Benki ya Rasilimali Tanzania ni benki inayomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Malengo ya benki hii ni kutoa mikopo ya muda wa kati na mrefu kwa wawekezaji katika maeneo ya kilimo, viwanda, biashara, usafiri, utalii na uchimbaji madini. Katika mwaka 2016/17 Serikali imetenga shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuongeza mtaji wa Benki. Shughuli zitakazotekelawa ni pamoja na kutoa mikopo katika sekta mbalimbali za kiuchumi ambazo benki inaona zitakazochochea ukuaji wa uchumi kwa haraka. Sekta hizo ni kama zifuatazo: Viwanda vitakavyotumia rasilimali za ndani kuongeza thamani; Miundombinu; Kuongeza thamani ya madini ghafi; kuwezesha kampuni za kusambaza gesi kwa matumizi ya viwanda na kuzalisha umeme; Kuwezesha sekta za utoaji wa huduma hususan afya, elimu, upimaji viwanja, ujenzi wa hoteli na nyumba.

(b) Benki ya Maendeleo ya Kilimo

Benki ilipata leseni ya biashara na kuanza shughuli Agusti, 2015. Shughuli za kutoa mikopo zilianza Disemba 2015 kwa majaribio katika mkoa wa Iringa kwa vikundi vya wakulima wa mahindi na kuendelea

katika mikoa ya Njombe, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam na Tanga. Malengo ya Benki ni kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula nchini na kubadilisha dhana ya kilimo kutoka katika kilimo cha kujikimu na kuwa kilimo cha biashara kwa kuwawezesha wananchi katika sekta ya kilimo. Aidha, katika mwaka 2016/17 Benki ya Maendeleo ya Kilimo imepanga: kushirikiana kwa karibu na *Tanzania Merchantile Exchange* katika kuhakikisha wakulima wanaunganishwa na masoko ya uhakika; kuanzisha ofisi za kanda ili kuwawezesha kutoa mikopo nchi nzima na kuwa na usimamizi wa karibu; kushirikiana na MIVARF kuwawezesha taasisi mbalimbali za fedha kutoa mikopo katika sekta ya kilimo; na kuendelea kutoa mafunzo kwa vikundi vya wakulima wadogowadogo nchi nzima kwa kuanza na mikoa ya Iringa, Morogoro, tanga na Pwani.

(c) Benki ya Wanawake Tanzania: Benki ya Wanawake Tanzania ilianza shughuli zake Julai, 2009. Malengo ya benki ni kukwamua vikwazo vingi katika kuwaendeleza wanawake ikiwa ni pamoja na; mila na desturi potofu, sheria kandamizi, mfumo dume unaokandamiza wanawake na kusababisha kukosa fursa ambazo zingeweza kuwapa wanawake uwezo wa kujiendeleza kiuchumi. Katika mwaka 2016/17, Serikali imetenga shilingi milioni 955 kwa ajili ya kuongeza mtaji wa Benki. Aidha, Benki imepanga: kuimarisha huduma kwa wateja kwa kuendelea kutoa huduma za benki katika maeneo mengi zaidi kuititia njia ya wakala wa benki (agency banking); kupanua huduma za benki kwa kufungua vituo vya kutolea mafunzo ya ujasiriamali na mikopo mikoani ambako benki haijafika; kuboresha kipato na ukuaji wa faida kwa kuendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na utunzaji wa kumbukumbu; na kuandaa programu ya kutolea elimu ya wajasiriamali wadogowadogo na wa kati.

(iii) Utalii

a) Utalii House Phase II

Mradi huu unahusu ujenzi wa kitega uchumi katika eneo lililokuwa Ubalozi wa **Marekani Dar es Salaam**. Kutokana na makubaliano kati ya Serikali za Tanzania na Marekani, kila nchi itachangia nusu ya gharama, hivyo Serikali ya Marekani ilijenga **Utalii House Awamu ya I** ambao kwa sasa jengo hilo linatumika. Hivyo, Serikali ya Tanzania inawajibika kujenga Utalii House **Awamu ya pili**. Katika mwaka 2016/17, shilingi milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: kuteua mshauri wa mradi; kuitisha zabuni za uchoraji na **Bills of Quantities**; kuitisha zabuni za ujenzi; kugharamia ujenzi wa ofisi za

muda za mradi; ujenzi wa ghala la kuhifadhi vifaa vya ujenzi; na kuandaa barabara ya kuingizia vifaa vya ujenzi.

b) Mradi wa Ujenzi wa “Theme Park” katika jiji la Dares Salaam

Mradi huu utatoa fursa kwa Sekta ya Utalii kuwa na eneo la kitalii ambalo litakuwa na huduma bora kama vile sehemu ya mapumziko/starehe na burudani sehemu ya kumbukumbu ya historia mbalimbali, hoteli zenyehadhi ya nyota za daraja la juu, migahawa ya kisasa, maduka (*shoping centres*), bustani ya wanyama (*zoo*), michezo ya golf, pamoja na shughuli mbalimbali za kitalii (*climbing walls, skycoaster or tower swing, chess playing area*) zitafanyika katika eneo hilo. Aidha mradi huu umekadirwa kutumia eneo lenye ukubwa wa hekta 10,000 karibu na mwambao wa bahari ya Hindi katika jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2016/17, shilingi milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi kwa kufanya upembuzi yakinifu na kubainisha eneo la mradi.

4.4 Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango

Utekelezaji wa mipango nchini umekuwa na mapungufu makubwa. Mpango unaomalizika muda wake (Juni, 2016) utafikia takribani asilimia 60 ya malengo. Sambamba na dhamira hii, kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17 ni pamoja na kutanzua vikwazo vya utekelezaji na kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango. Aidha, yapo marekebisho yanayopaswa kufanyika ya kisera, sheria na taratibu kusaidia ufanisi wa utekelezaji.

4.5 Miradi Mikubwa ya Kielelezo

Katika vipaumbele, ipo miradi mahsus, kwa maana ya ukubwa wa uwekezaji na matokeo yake katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wenyewe. Miradi hii imepewa sifa ya kuwa miradi ya kielelezo (flagship projects). Usimamizi wa miradi hii utatofautishwa na miradi mingine, ambapo matayarisho na utekelezaji wake utatumia mfumo wa kimaabara wa “Matokeo Makubwa Sasa” na bajeti yake italindwa. Miradi hii itajumuisha:

(i) Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma - Njombe

Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma unatekelezwa kwa ubia kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo (hisa 20%) na kampuni ya Sichuang Hongda Group Limited - SHGL (hisa 80%) ya China kupitia kampuni ya ubia ya Tanzania - China International Mineral Resources Limited (TCIMRL). Mkataba wa makubaliano kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa na kampuni ya SHGL ya kutekeleza mradi kwa ubia ulisainiwa

mwaka 2011 kwa ajili ya uzalishaji wa umeme wa MW 300 kwa awamu ya kwanza. Kwa mujibu wa tafiti za Shirika la Maendeleo la Taifa, eneo la Mchuchuma linakadiriwa kuwa na makaa ya mawe tani milioni 428 kiwango ambacho kinaweza kutumika kwa takribani miaka 500. Mradi unalenga kujenga mgodi wa kuchimba makaa ya mawe kiwango cha tani milioni 3 kwa mwaka. Makaa hayo yatatumika kuzalisha MW 600 za umeme, ambapo MW 250 zitatumika katika mgodi wa chuma - Liganga, na MW 350 zitaingizwa katika Gridi ya Taifa. Aidha, mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Kv 220 kutoka Mchuchuma hadi Liganga. Gharama za mradi hadi kukamilika ni dola za Kimarekani bilioni 1.2 ambazo zitatolewa na kampuni ya SHGL.

Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 5 zimetengwa kwa ajili ya kuanza malipo ya fidia kwa wananchi wa Mundindi na Mkomang'ombe watakaotha maeneo yao kwa ajili ya mradi, kuhamishia wananchi wanaopisha eneo la mradi na **kuwajengea makazi mapya**.

(ii) Mradi wa Chuma Liganga - Njombe

Mradi wa kuzalisha chuma Liganga unatekelezwa na kampuni ya Tanzania – China Mineral Resources Limited, ambayo ni kampuni ya ubia kati ya Serikali kuitia Shirika la Maendeleo la Taifa yenye hisa asilimia 20 na kampuni ya Sichuang Hongda Group Company Limited (SHGL) kutoka China yenye hisa asilimia 80. Mradi wa chuma Liganga utahusisha ujenzi wa mgodi; kiwanda kitakachozalisha tani milioni 1 za chuma kwa mwaka pamoja na ujenzi wa kinu cha kuyeyusha chuma na kutenganisha chuma na madini ya Vanadium na Titanium. Eneo la mradi wa chuma Liganga una ukubwa wa kilometa za mraba 179. Aidha, kwa mujibu wa tafiti zilizofanyika eneo hilo lina akiba ya tani milioni 126 za chuma kiwango ambacho kinatosha kutumika kwa zaidi ya miaka 40. Gharama za mradi hadi kukamilika ni dola za kimarekani bilioni 1.7 fedha ambazo zitatolewa na Kampuni ya SHGL.

Katika mwaka 2016/17, zimetengwa shilingi bilioni 5 kwa ajili ya uthamini wa eneo la kuhamishia wananchi wanaopisha eneo la mradi; kuchangia katika ulipaji wa fidia kwa watakaoathiriwa na mradi na **kuwajengea makazi mapya** na kusimamia utekelezaji wa Kampuni ya ubia. Mradi huu utasimamiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa na unatarajiwa kuanza uzalishaji 2018/19.

(iii) Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Standard Gauge

Mradi huu unahusisha ujenzi wa reli ya kati kutoka Dar – Isaka-Kigali/Keza-Musongati (km 1,661) pamoja na ujenzi wa reli mpya ya kutoka Tabora – Kigoma, Kaliua – Mpanda and Isaka - Mwanza (km 1,220) kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Utekelezaji wa Miradi hii yote unaratibiwa na Shirika Hodhi la Rasilimali za Reli (RAHCO) chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Uchukuzi).



Muonekano wa njia ya reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge itakapokamilika

- (a) Ujenzi wa reli ya Dar-Isaka-Kigali/Keza-Musongati (km 1,661) kwa kiwango cha Standard Gauge:** Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano na nchi za Rwanda na Burundi na utekelezaji wake ulianza mwaka 2005 baada ya nchi hizo kusaini makubaliano (MoU). Mradi huu utatekelezwa kwa mfumo wa ubia baina ya Serikali na sekta binafsi (PPP) na unakadirwa kugharimu dola za Kimarekani bilioni 7.6. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 1,000 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa maeneo machache yakakayotwaliwa, kukamilisha usanifu wa kujenga reli na kuanza ujenzi wa reli.
- (b) Ujenzi wa Reli ya Kati Tabora – Kigoma, Uvinza – Msongati, na Isaka – Mwanza, Kaliua – Mpanda na Mpanda - Karema (km 1,220) kwa Kiwango cha Standard Gauge:** Mradi unalenga kuboresha na kujenga njia ya reli kati ya Tabora – Kigoma (km 411), Isaka – Mwanza (km 249) na Uvinza – Musongati (km 200) kwa kiwango cha

kimataifa (standard gauge) ili iendane na kiwango cha njia ya reli kitakachojengwa kati ya Dar es Salaam – Isaka. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 15 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa kina wa njia ya reli kati ya Tabora – Kigoma na Kaliua -Mpanda; kulipa deni kwa kazi ya usanifu wa kina wa njia ya reli kati ya Isaka – Mwanza; kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa mradi kati ya Uvinza - Msongati na Mpanda-Karema; kulipa fidia eneo la Buhongwa; na fidia ya ardhi kwa ajili ya mradi wa reli kutoka Mpanda – Karema.

(iv) Ununuzi na ukarabati wa meli kwenye Maziwa Makuu

Mradi unalenga kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu kwa kukarabati na kununua meli mpya katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 50.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Kati ya fedha hizi, shilingi bilioni 21 ni kwa ajili ya malipo ya awali (asilimia 50) ya ununuzi wa meli moja mpya ya Ziwa Victoria; shilingi bilioni 20 ni kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa meli ya MV Victoria, shilingi bilioni 5.9 ni kwa ajili ya ukarabati meli ya MV Liemba; na shilingi bilioni 3.6 ni kwa ajili ya ukarabati wa meli ya MV Butiama.

(v) Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania

Ununuzi wa ndege mpya kwa ajili ya Shirika la ndege la Tanzani (ATCL): Mradi unahusisha uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya, kulipa madeni muhimu pamoja na mtaji wa kuanzia wa kuiwezesha ATCL kuendesha shughuli zake. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 500 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ununuzi ndege mpya zisizopungua 3 moja ikiwa ni Bombardier CS300 yenye uwezo wa kubeba abiria 100 – 150 na ndege aina ya Bombardier Q400 yenye uwezo wa kubeba abiria 67 – 88 kila moja.

(vi) Barabara ya Kidahwe – Kanyani – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310)

Mradi unalenga kujenga barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unatekelezwa kwa sehemu mbalimbali ifuatavyo; Nyakanazi – Kibondo (km 50), Kidahwe – Kasulu (km 50) na Nyakanazi – Kasulu/Manyovu (km 210) kwa kiwango cha lami, ambapo ujenzi unaendelea. Katika mwaka

2016/17 shilingi bilioni 60.3 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidahwe – Kasulu na Nyakanazi – Kibondo pamoja na kukamilisha mapitio ya usanifu na kuanza maandalizi ya ujenzi sehemu ya Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 210).

(vii) Barabara ya Masasi - Songea – Mbambabay (km 868.7)

Mradi unalenga kujenga barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 659.7) pamoja na Masasi – Newala – Mtwara (km 209) kwa kiwango cha lami. Utekelezaji wa mradi umegawanyika katika sehemu za Masasi – Mangaka (km 54), Mangaka – Nakapanya – Tunduru (km 146), Mangaka – Mtambaswala (km 65.5), Namtumbo – Kilimasera (km 60.7); Kilimasera – Matemanga (km 68.2), Matemanga – Tunduru (km 58.7), Mbinga – Mbamba Bay (km 66) na Masasi – Newala – Mtwara (km 209). Ujenzi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Africa (AfDB) na Serikali ya Japan kupitia JICA. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 33.6 fedha za ndani na shilingi bilioni 93.2 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za (Mangaka – Nakapanya, Nakapanya – Tunduru, Mangaka – Mtambaswala, na Tunduru – Matemanga); na kuanza ujenzi wa sehemu za Mbinga – Mbambabay na Masasi – Newala – Mtwara.

4.6 Maeneo Mengine Muhimu kwa ukuaji wa Uchumi na Ustawi wa Taifa

4.6.1 Madini

- (a) Mradi wa Dhahabu wa Buhemba:** Shirika la Taifa la Madini - STAMICO lilifanya uchambuzi yakinifu kuona uwezekano wa kujenga kiwanda cha kuchenjua mabaki ya dhahabu katika mgodi wa Buhemba. Ilibainika kuwa katika mabaki ya mchanga wa dhahabu ambayo ni tani 796,400 kuna dhahabu gram 1.07 kwa tani ambazo kwa mabaki yote ya dhahabu wastani wa kilo 852 za dhahabu zitapatikana. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 17.5 zimetengwa kwa ajili ya kununua mashine ya kuchenjua mabaki ya dhahabu, kufanya upembuzi yakinifu katika miamba migumu na kuchoronga miamba migumu.
- (b) Mradi wa Kununua Madini ya Bati:** Katika kuimarishe soko la wachimbaji wadogo wa madini ya bati toka mwaka 2014 STAMICO ilianza kununua madini kutoka kwa wachimbaji wadogo wa vijiji vya Kabingo, Murongo, Syndicate na Rugasha Wilaya ya Kyerwa, Kagera. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 1.12 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa madini hayo.

- (c) **Usimamizi wa Madini na Kuimarisha Taasisi za Madini:** Katika mwaka 2016/17 shughuli zitakazotekelawa ni kutoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo; kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo; ukarabati wa STAMICO, Chuo cha Madini, Dodoma na ofisi ya madini Handeni; na kuwezesha ukaguzi wa migodi.

4.6.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

- (a) **Mradi wa Kujenga, kukarabati na kununua majengo kwa ajili ya balozi za Tanzania:** Mradi unalenga kuboresha huduma kwa kujenga, kukarabati na kununua majengo ya balozi za Tanzania nje ya nchi hususani za ofisi, makazi na kitega uchumi. Katika mwaka 2016/17, shilingi blioni 8.0 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ambalo ni sehemu ya kituo cha mikutano ya kimataifa ya Julius Nyerere; kukamilisha ukarabati wa **jengo la ghorofa 9**, makazi ya Balozi na mkuu wa Utawala Ubalozi wa Tanzania Maputo, Msumbiji; kukarabati makazi ya Balozi na watumishi yaliyopo Stockholm, Sweden; Kukarabati majengo 2i yanayomilikiwa na Serikali yaliyopo Khartoum, Sudan; na kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya Wizara na balozi za Tanzania.
- (b) **Kukamilisha Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja Mipakani:** Vituo vya Utoaji Huduma Pamoja mpakani vimeanzishwa na nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuitia Itifaki za Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja ambavyo vimejengwa katika mipaka ya nchi za jumuiya wanachama. Vituo hivi vina dhana ya kurahisisha taratibu za uhamiaji, forodha, ukaguzi wa ubora wa bidhaa, usalama na ulinzi kwa kutoa huduma hizi katika upande mmoja wa mpaka kwa pamoja bila kulazimika kuitia tena taratibu hizo upande wa pili wa mpaka ili kukuza biashara kwa kupunguza gharama na muda wa kusafirisha bidhaa. Mradi unalenga kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma mipakani kwa kukamilisha vituo ambavyo havijakamilika na miundombinu yake. Aidha, Tanzania ina vituo vingine vya utoaji huduma mpakani mbali na vile vya Afrika Mashariki ambavyo ni Tunduma/Nakonde mpakani mwa Tanzania na Zambia ambacho kinafadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali na TradeMark East Africa (TMEA), Kasumulu/Songwe mpaka wa Tanzania na Malawi na Mtambaswala kwenye mpaka wa Tanzania na Msumbiji. Katika mwaka 2016/17, kazi zitakazotekelawa ni kukamilisha vituo ambavyo havijakamilika na kuanza ujenzi wa vituo vya Tunduma/Nakonde,

Kasumulu/Songwe na Mtambaswala.

4.6.3 Utawala Bora

- (a) **Mradi wa Mfuko wa Bunge:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya ofisi za Bunge Dodoma na Dar es Salaam, na ofisi za Wabunge Majimboni. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 7 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa majengo ya Bunge Dodoma na Dar es Salaam na ujenzi wa ofisi za wabunge majimboni.
- (b) **Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Sekretarieti ya Maadili:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya ofisi za kanda. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 1 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ofisi ya Kanda ya Kusini – Mtwara; maandalizi ya awali ya ujenzi wa ofisi za kanda za Mashariki, Magharibi, Kanda ya ziwa, ya Kati na Nyanda za Juu Kusini; kuendelea kutekeleza Mkakati wa Mapambano dhidi ya Rushwa (awamu ya III); kuendelea kutekeleza Mpango wa Serikali wa Kuendesha Shughuli kwa Uwazi; na kuendelea na maboresho katika sekta ya umma ili kuwezesha utoaji huduma kwa uwajibikaji.
- (c) **Mradi wa Vitambulisho vya Taifa:** Mradi unalenga kuharakisha upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi. Katika mwaka 2016/17 shilingi bilioni 30 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kusajili wananchi katika kanda mbalimbali, ununuzi wa vifaa vya usajili, na kuendeleza mfumo wa mawasiliano kati ya wilaya na makao makuu ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Dar es Salaam.

4.6.4 utoaji Haki na Huduma za Sheria

- (a) **Mradi wa Mfuko wa Mahakama:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya mahakama na nyumba za majaji nchini. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 24 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama Kuu, Kanda za Kigoma na Mara; ukarabati wa majengo ya Makahama Kuu, Kanda ya Mbeya; Ujenzi wa mahakama za wilaya Kilindi, Chato, Bariadi, Kasulu, na Kondoa; ujenzi wa mahakama za mwanzo Longido, Terati (Manyara), Machame (Hai), Njombe Mjini, Makongolosi (Chunya), Ulyankulu (Tabora) na Gairo - (Mvomero), Mtowisa (Sumbawanga) na Mangaka (Mtwara).

- (b) **Mradi wa Telejustice (E-Justice):** Mradi unalenga kukuza matumizi

ya TEHAMA katika uendeshaji wa shughuli za Serikali ili kuboresha huduma za kisheria zinazotolewa kwa umma pamoja na kuongeza uwezo wa Serikali wa kufikisha huduma kwa wananchi wengi zaidi. Pia, mradi unalenga kuunganisha (integration) mfumo wa ndani wa mawasiliano (LAN) kati ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi za haki jinai; kusimika mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu na taarifa mbalimbali za kijinai; na kufunga mfumo wa usikilizaji wa mashauri kwa njia ya *video conferencing*. Katika mwaka 2016/17 zimetengwa shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kukamilisha taarifa ya upembuzi yakinifu ya mradi; kuanza utekelezaji awamu ya kwanza ya mradi huo katika mkoa wa Dar es Salaam.

- (c) **Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali:** Mradi unalenga kuimarisha miundombinu ya ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika mwaka 2016/17, shilingi bilioni 1 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
- (d) **Katiba Mpya:** Kukamilisha taratibu za kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mwaka 2016/17, shughuli zitakazofanyika ni kukamilisha taratibu za kufanyika kwa kura za maoni na kuanzisha mchakato wa marekebisho mbalimbali ili kuweza kutumika.

4.7 Mikakati ya Ushiriki wa Sekta Binafsi

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 utategemea zaidi ushiriki mkubwa wa Sekta Binafsi kutokana na dhana ya kujenga uchumi wa viwanda. Hivyo, Serikali imeweka mikakati ya kujenga na kuboresha miundombinu wezeshi (nishati ya umeme, reli, barabara, bandari, usafiri wa anga na majini), kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kuhamisisha na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma. Jitahada maalum za Serikali katika eneo hili ni pamoja na: kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji (EPZs na SEZs); kuongeza mtaji wa benki ya uwekezaji Tanzania ili kutoa mikopo kwa wawekezaji wa ndani; na kuiwezesha Kituo cha Uwekezaji Tanzania kuwa na ardhi yenye hati miliki kwa ajili ya kuwakodisha wawekezaji wa nje.

Maelezo ya kina kuhusu miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2016/17 yapo katika kitabu cha mpango **Kiambatisho V**.

SURA YA TANO

UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17

5.1 Ugharamiaji wa Miradi

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17 utagharamiwa na Serikali kuitia vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani, misaada na mikopo, Sekta Binafsi na ubia kati ya sekta ya Umma na Binafsi. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo hususan sekta binafsi itahakikisha rasilimali watu na fedha zinapatikana kutekeleza Mpango huu. Aidha, msisitizo utawekwa katika kutenga bajeti na kulinda fedha za kutekeleza miradi mikubwa ya kielelezo iliyoainishwa katika Mpango.

5.2 Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2011/12 – 2015/16

Makadirio ya bajeti ya kutekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 - 2015/16) yalikuwa shilingi triliuni 44.5 ambayo ni wastani wa shilingi triliuni 8.9 kila mwaka. Kati ya fedha hizo shilingi triliuni 2.9 zilitarajiwa kuwa fedha za ndani na shilingi triliuni 6.0 sekta binafsi na washirika wa maendeleo. Katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango huo, fedha za ndani zilizotolewa zilifikia wastani wa shilingi triliuni 2.9 kwa mwaka. Aidha, katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, fedha za maendeleo zilizotolewa ni wastani wa asilimia 26 ya bajeti halisi kwa mwaka ikilinganishwa na lengo la asilimia 35. Kwa upande wa mchango wa sekta binafsi na washirika wa maendeleo haukufikia asilimia 50 kutokana na ushiriki mdogo wa sekta binafsi na wafadhili kutotimiza ahadi zao. **Kielelezo Na. 4.1** kinaeleza mwenendo wa ugharamiaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16).

Kielelezo Na 4.1: Mwenendo wa Ugharamiaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 -2015/16)

| | Mwaka | Makadirio ya FYDP I (Sh. Mil.) | Bajeti Halisi ya Serikali (Sh. Mil.) | Fedha za Maendeleo Ndani na Nje (Sh. Mil.) | Fedha za Maendeleo za Ndani (Sh. Mil.) | Fedha za Maendeleo za Nje (TSh Mil) | Fedha za Maendeleo za Ndani na nje /Bajeti Halisi ya Serikali (%) |
|-----------------------|---------|--------------------------------|--------------------------------------|--|--|-------------------------------------|---|
| Matumizi Halisi | 2010/11 | - | 10,202,602 | 2,749,037 | 984,555 | 1,764,482 | 27% |
| | 2011/12 | 8,473,812 | 12,171,877 | 3,774,722 | 1,872,312 | 1,902,410 | 31% |
| | 2012/13 | 11,878,988 | 14,162,228 | 3,844,291 | 2,277,553 | 1,566,738 | 27% |
| | 2013/14 | 9,917,372 | 15,667,535 | 3,926,043 | 2,121,212 | 1,804,831 | 25% |
| | 2014/15 | 7,901,872 | 16,637,765 | 3,452,855 | 2,264,506 | 1,188,349 | 21% |
| Makadirio ya Matumizi | 2015/16 | 6,314,743 | 22,495,492 | 5,909,053 | 4,246,872 | 1,662,180 | 26% |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango, 2015.

Angalizo: Bajeti halisi ya Serikali inajumuisha fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo.

5.3 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2016/17

Katika mwaka 2016/17, makadirio ya bajeti ya maendeleo ni shilingi bilioni 11,820.503 sawa na asilimia 40 ya bajeti yote. Aidha, fedha za ndani ni shilingi bilioni 8,702.70 sawa na asilimia 74 ya fedha za maendeleo na fedha za nje ni shilingi bilioni 3,117.81 sawa na asilimia 26. Fedha hizo zitatokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo mapato ya ndani, mapato ya nje, ubia kati ya sekta ya umma na binafsi na uwekezaji wa sekta binafsi na mikopo nafuu hususan kutoka katika taasisi za benki za hapa nchini ikiwemo TIB na TADB. Matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa asilimia 6.3 ya Pato la Taifa katika mwaka 2016/17.

Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 itawezesha utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa ufanisi. Katika sheria hiyo imeanishwa kuwa: miradi itakayozingatiwa katika makadirio ya bajeti ni ile inayotokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa; Serikali na Taasisi zote za umma kuandaa bajeti kulingana na Mpango wa muda mrefu na muda wa kati; miradi ya maendeleo itatekelezwa kulingana na vipaumbele vya Taifa vilivyowekwa; na miradi ya maendeleo itakayotekelawa ni ile iliopitishwa na Tume ya Mipango.

5.4 Vyanzo vya Mapato ya Ndani

Katika mwaka 2016/17, Serikali itagharamia miradi ya maendeleo kuitia vyanzo vya ndani vya mapato vilivyopo vikiwemo vya Halmashauri, vyanzo vinya vilivypendekezwa katika maabara ya ukusanyaji wa mapato, ambavyo ni kodi, mapato yasiyo ya kodi, misaada na mikopo, dhamana za mikopo na vyanzo vingine vya mapato ya ndani. Vile vile, Serikali itaendelea kukopa ndani ya nchi kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia ukomo wa kukopa ndani ya nchi usiozidi asilimia 1 ya Pato la Taifa. Serikali inatarajia kukusanya mapato ya ndani ambayo ni asilimia 16.9 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2016/17.

5.5 Vyanzo vya Mapato ya Nje

Taarifa ya Uchambuzi ya Uhimilivu wa Madeni ya mwaka 2015 (Debt Sustainability Analysis) ilioandalishi na Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inaonesha kuwa deni la Taifa linahimilika, hivyo Tanzania itaendelea kukopa mikopo yenye masharti nafuu na kutumia misaada inayotolewa na washirika wa maendeleo kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vile vile, katika mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara ili kufanikisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya miundombinu. Katika mwaka 2016/17, Serikali imepanga kukopa

kiasi cha dola za Kimarekani milioni 800. Aidha, Serikali itaendelea kutumia vyanzo mbalimbali kama hati fungani za miundombinu na akiba, makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi kikanda, hati fungani maalum na kuzingatia ukomo wa uhimilivu wa deni la Taifa katika mchakato wa kukopa fedha nje ya nchi.

5.6 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Katika mwaka 2016/17, idadi ya miradi itakayotekelawa chini ya ubia wa Serikali na Sekta Binafsi (PPP) inatarajiwa kuongezeka kufuatia kukamilika kwa sera, sheria na kanuni za PPP. Kupitia utekelezaji wa PPP, Serikali itapata nafuu katika bajeti ya maendeleo hususan katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu na hivyo kuongeza wigo wa kutekeleza maeneo mengine ya Mpango wa Maendeleo. Serikali itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wadau wa sekta binafsi ili washiriki kikamilifu katika uwekezaji kwa ubia na sekta ya umma.

5.7 Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Utekelezaji wa viwanda nchini kwa kiwango kikubwa utategemea ushiriki wa sekta binafsi. Hivyo, Serikali itaendelea kuandaa mazingira wezeshi kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kupanga mikakati ya kushawishi sekta binafsi za ndani na nje ya nchi kushiriki kuibua na kutekeleza Mpango, kulea utamaduni wa uadilifu na uwajibikaji wa kijamii, kutoa mwongozo na taratibu za sekta binafsi kushiriki katika miradi kwa njia ya ubia na sekta ya umma na kuweka mikakati ya kuvutia uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja.

5.8 Mikopo Nafuu kutoka Taasisi za Fedha Nchini

Kwa kutambua changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa mitaji ya uwekezaji unaochukua muda mrefu, ipo haja ya kusaidia taasisi za fedha za kimaendeleo (DFIs) za ndani, ikiwa ni pamoja na kuzipa nafasi ya kipekee katika kubainisha mikakati muafaka ya kukusanya na kugharamia uwekezaji mkubwa na wa muda mrefu wa miradi ya maendeleo. Serikali itaongeza mitaji katika Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) ili kuwezesha kutafuta fedha zaidi kutoka Benki zingine na kusaidia kutoa mikopo nafuu kwa wawekezaji wa miradi ya maendeleo hapa nchini.

SURA YA SITA

UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

6.1 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17 utazingatia mfumo na mwongozo utakaotumika katika ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ulioainishwa katika mwongozo wa Mpango na Bajeti 2016/17. Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakuwa na malengo ya utekelezaji kwa kila sekta na kuandaa mpango kazi wa mwaka. Utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo utazingatia pia Mwongozo wa Uandaaji na Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Management – Operational Manual) wa mwaka 2015. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha idara za ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ili miradi iliyoanzishwa iweze kuleta tija kwa Taifa.

6.2 Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo

6.2.1 Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa

Katika mwaka 2015/16, utekelezaji wa miradi ya Matokeo Makubwa Sasa ulifuatiliwa na Ofisi ya Rais, Uratibu na Ufuatiliaji wa Miradi – PDB kwa kushirikiana na Vitengo Maalum vya Ufuatiliaji vya Wizara. Sekta zilizofuatiliwa ni Kilimo, Viwanda, Elimu, Uchukuzi, Maji, Nishati, na Fedha. Taarifa za ufuatiliaji wa Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa zinazingatia maeneo ya kipaumbele kupitia viashiria vilivyowekwa katika kila sekta.

6.2.2 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati

Katika kipindi mwaka 2015/16, Wizara ya Fedha na Mipango ilifuatilia miradi ya maendeleo 38 katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Geita, Iringa, Mbeya, Kagera, Morogoro, Mwanza, Singida, Shinyanga, Simiyu na Tabora. Miradi iliyofuatiliwa ilijumuisha ya Umma na Sekta Binafsi, katika maeneo ya viwanda, barabara, bandari, viwanja vya ndege, nishati, maji, umwagiliaji, mifugo, afya na mkongo wa Taifa. Miradi iliyotembelewa iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikijumuisha iliyokamilika, inayoendelea na iliyo katika hatua za maandalizi.

(a) Barabara

Barabara za Isaka - Lusahunga (km 242), Lusahunga - Rusumo (km 90), Iringa - Dodoma (km 259.6) na Manyoni - Itigi (km 70.9): Kwa upande wa barabara ya Isaka - Lusahunga, ukarabati wa barabara eneo la Isaka -

Ushirombo na ujenzi wa miundombinu ya madaraja umekamilika. Aidha, ukarabati wa barabara ya Ushirombo - Lusahunga (km 40) umesimama kutokana na madai ya Mkandarasi ambaye amelazimika kuondoa vifaa eneo la Ushirombo. Kwa upande wa barabara ya Lusahunga - Rusumo, ukarabati wa maeneo yaliyoharibika unaendelea ili kupunguza usumbufu wa watumiaji wa barabara ambayo ina mashimo mengi. Kwa upande wa barabara za Iringa - Dodoma na Manyoni - Itigi ujenzi umekamilika lakini kuna uharibifu wa barabara unaofanywa na wananchi kwa kuchimba na kuchukua kokoto za barabara kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Hata hivyo, mkandarasi ambaye ana madai anaendelea na taratibu za kukamilisha uwekaji wa alama za barabarani ambazo pia ameonesha wasiwasi wa kuchukuliwa na wananchi.

(b) Reli

Reli ya Kati eneo la Kitaraka na Malongwe (km 89): Kazi ya kutandika reli ya ratili 80 kwa yadi ipo katika hatua za mwisho. Hata hivyo, utaratibu wa matengenezo ya mara kwa mara wa reli bado ni changamoto kwa kuwa usimamizi wa reli unaratibiwa makao makuu. **Reli ya Kati ya Isaka – Buhongwa – Mwanza (km 250):** Utekelezaji wa mradi huu bado haujaanza kutokana na ukosefu wa fedha.

(c) Bandari

- (i) **Bandari ya Bukoba:** Miundombinu ya kuhudumia meli bandarini ni chakavu na haitoshelezi kutoa huduma kwa abiria na mizigo. Aidha, bandari imezungukwa na gati za watu binafsi ambao wamevamia eneo la bandari na kuleta ushindani. Ufanisi wa bandari umeathiriwa kwa sababu ya kusuasua kwa usafirishaji kwa njia ya reli ya kati na kukosekana kwa meli za kutosha za abiria na mizigo.
- (ii) **Bandari ya Nansio - Ukerewe:** Bandari inahudumia wastani wa abiria 3,800 (Inwards), abiria 5,000 (outwards) na wastani wa mizigo tani 75 (inwards) na tani 25 (outwards) kwa mwezi. Eneo la bandari lilipanuliwa mwaka 2014 baada ya ununuzi na ulipaji fidia kwa upande wa mashariki mwa bandari ya Nansio na kufikia hekta 2. Bandari ya Nansio ipo chini ya Mamlaka ya Bandari Tanzania tangu mwaka 2006. Katika bandari ya Nansio zilikuwepo meli mbili (2) zilizokuwa zikitoa huduma asubuhi na mchana lakini kwa sasa meli ya Serikali moja imeharibika, hivyo imebaki meli moja tu ya kampuni binafsi ya Nyehunge ambayo inayotoa huduma kuanzia Mwanza mchana na kuanzia Nansio asubuhi. Kwa hivi sasa majengo yamejengwa likiwemo jengo la ofisi ya kisasa, chumba cha mapumziko ya abiria, chumba cha

wageni maalum yaani V.I.P na sehemu ya mgahawa. Hata hivyo, bandari inahitaji maboresho makubwa ya gati na upanuzi eneo la bandari. Aidha, zinahitajika meli 2 zaidi kwa kuwa mahitaji ya usafiri kati ya Mwanza na Ukerewe ni makubwa sana. Pia kuna umuhimu wa kuwa na bandari katika eneo la Ngoma/Kisorya (Ukerewe – Bunda) kwa kuweka gati pande zote mbili na kuongeza kivuko cha pili ili kuimarisha usafiri kati ya Ukerewe na Bunda.

(d) **Viwanja vya Ndege**

Kiwanja cha Ndege cha Songwe: Uwanja wa Songwe uliopo Mbeya ulianza kutumika mwaka 2012. Upembuzi yakinifu uliofanyika mwaka 1998 na usanifu wa kina ulifanyika mwaka 1997 ulikuwa ni kwa ajili ya ndege aina ya Fokker 50. Aidha, kutokana na maendeleo ya kiuchumi na kijamii Serikali iliamua kupanua miundombinu ya kiwanja ili kukidhi matumizi ya ndege kubwa zinazolingana na ukubwa wa Boeing 737 zenyet uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 100 badala ya ndege ndogo zilizoainishwa kwenye usanifu wa awali. Ujenzi wa kiwanja unatarajia kukamilika mwaka 2016. Ujenzi wa jengo hilo ukikamilika uwanja utakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 250,000 kwa mwaka. Changamoto za kiwanja ni pamoja na: kukosekana kwa uzio wa kiwanja; na kutokuwa na *navigational aids* kutokana na ufinyu wa fedha iliyotengwa. Eneo la Mbeya (Songwe) kuwa na ukungu hususan wakati wa asubuhi na hivyo kuwa vigumu kwa marubani wa ndege kuona kiwanja vizuri.

(e) **Nishati**

Miradi ya Kuzalisha Umeme

- (i) **Bwawa la Mtera:** Mradi wa bwawa la mtera ulianza mwaka 1980 kwa lengo la kuzalisha umeme Kidatu na Mtera. Bwawa lina uwezo uwezo wa kujaza maji kina cha mita 698.5 na eneo la kilomita za mraba 660. Uzalishaji wa umeme katika bwawa si wa kuridhisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya hali ya hewa, kilimo cha umwagiliaji, ufgaji holela, uchakavu wa mitambo na upotevu wa maji. Aidha, kukamilika kwa barabara ya Iringa – Dodoma kumeongeza idadi ya magari yanayopita katika daraja la mto Mtera na hivyo kutishia uhai wa daraja na bwawa. Hivyo, kuna haja kwa siku zijazo kudhibiti vihatarishi vya bwawa la Mtera na kutafuta njia mbadala ya magari.

- (ii) **Mradi wa Umeme wa Upepo Singida:** Katika eneo la mradi kimejengwa kituo cha kupima kasi ya upepo ambacho kimewezesha

kubaini uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 100. Aidha, umeme utakaozalishwa utaunganishwa kwenye gridi ya Taifa Singida mjini. Mradi unategemea kuanza baada ya kupatikana mkopo wa dola za Kimarekani milioni 136 kutoka benki ya Exim ya China.

- (iii) **Mradi wa Umeme Rusumo:** Utekelezaji wa mradi huu bado haujaanza. Hata hivyo, makubaliano baina ya Tanzania, Rwanda na Burundi yamesainiwa ambapo kila nchi itapata MW 27. Kwa upande wa Tanzania umeme utaunganishwa kwenye gridi ya Taifa baada ya kukamilika mradi wa kusafirisha umeme KV 220 wa Geita – Nyakanazi.
- (iv) **Kituo cha kuzalisha umeme wa maji Kidatu:** Kituo kina uwezo wa kuzalisha MW 204 katika bwawa lenye mita za ujazo 125. Shughuli zilizotekelze wa ni pamoja na kufunga mitambo mipy ya kupozea hewa, kusafisha handaki ili kuruhusu njia za umeme kuwa salama. Ununuzi wa vali na pampu za maji ya kusafisha mitambo na pampu za maji safi na maji taka na kuendelea kubadilisha mitambo ya kukata umeme na kutenganisha umeme wa mkondo wa KV 220 katika njia ya MG1,T1 na T2. Shughuli zinazoendelea ni kubadili mfumo wa kuongoza mitambo (control system), kubadili mfumo wa upoozaji hewa ndani, kubadilisha mfumo wa *DC power house* na kubadilisha vidhibiti mwendo (speed governor). Changamoto zilizopo ni uchakavu wa mitambo, uhaba wa maji na fedha. Hata hivyo, kuna fursa kubwa ya kuzalisha umeme katika kituo hicho.
- (v) **Kituo cha kuzalisha umeme wa maji Kihansi:** Kituo kipo kwenye bonde la mto rufiji umbali wa kilomita 540 kutoka Dar es Salaam kwenye milima ya Udzungwa. Kituo hiki kina uwezo wa Megawati 180 itokanayo na mitambo mitatu (3) yenye ukubwa wa megawati 60 kila mmoja. Shughuli zilizotekelze wa ni kubadilisha mfumo wa kuongozea mitambo (control system), kubadilisha mfumo wa upoozaji hewa ndani ya *power plant*, kubadilisha mfumo wa *DC power house* na kubadilisha vidhibiti mwendo (speed governor) kwenye mitambo. Changamoto zinazokabili kituo ni uchakavu wa mitambo ambayo inaongeza gharama za uendeshaji na uhaba wa fedha kwa ajili ya kufunga mashine za ziada mbili (2) ili kufikia lengo la mashine tano (5) kwa kituo. Hata hivyo, kituo kina fursa kubwa ya kuzalisha umeme zaidi iwapo bwawa la pili litajengwa na kuongeza mitambo zaidi.

(vi) **Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira - Mbeya:** Mgodi ulianza mwaka 1988 kwa msaada wa Serikali ya China ukiwa na mashapo ya makaa "economical reserve" ya tani milioni 35.14, kati ya hayo mashapo ya kisanifu (proved reserve) ni tani milioni 22.14 na mashapo yanayoweza kuvunwa kwa faida (Mineable reserve) ni tani milioni 14.64 za makaa. Awali mgodi ulilenga kuzalisha makaa ya mawe tani 150,000 kwa mwaka kwa ajili ya nishati ya matumizi ya viwanda vya hapa nchini vya Saruji (Mbeya), Karatasi cha Mgololo (Mufindi), na viwanda vya chai vya Katumba na Musekela (Tukuyu). Mgodi ulibinafsishwa mwaka 2005 kwa Kampuni ya Kiwira Coal Mines Ltd ambapo Serikali ya Tanzania ilimiliki asilimia 30 ya hisa na Tan Power Resources asilimia 70 ya hisa. Mgodi unalenga kuzalisha makaa ya mawe tani milioni moja.

(f) Viwanda

- (i) **Kiwanda cha Alizeti cha Singida Fresh Oil Mill:** Kiwanda kilianzishwa mwaka 2006 na kinamilikiwa na kampuni ya binafsi ambapo kina uwezo wa kusindika tani 200 za alizeti kwa siku. Alizeti inayosindikwa kiwandani inanunuliwa moja kwa moja kutoka kwa wakulima. Kiwanda pia hutoa huduma ya usindikaji wa alizeti kwa wafanyabiashara wengine. Hata hivyo kiwanda bado ni kidogo na kinatumia teknolojia ya nguvu kazi nyingi zaidi (labour intensive). Kiwanda kimeajiri wafanyakazi 16 katika ajira ya masharti ya kudumu na wafanyakazi 90 kwa masharti ya ajira ya muda. Changamoto za kiwanda hiki ni pamoja na mafuta yanayoingizwa nchini ambayo hutozwa kodi ndogo hivyo kusababisha ushindani usio wa haki katika soko la mafuta nchini na kushuka kwa uzalishaji wa zao la alizeti kunakotokana na ubora hafifu wa mbegu na matumizi madogo ya mbolea.
- (ii) **Kiwanda cha Nguo cha 21st Century – Morogoro:** Kiwanda cha 21st Century Textiles Ltd kilianzishwa mwaka 2003 baada ya kubinafsishwa kwa kilichokuwa kiwanda cha nguo cha Morogoro Polyester Textiles Ltd kwa asilimia 100 ya umiliki wa Serikali. Mwekezaji wa kiwanda hicho, amefanya maboresho mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuondoa mitambo ya zamani na kufunga mitambo mipya inayotumia teknolojia ya kisasa na hivyo kusababisha kiwanda kuzalisha bidhaa bora zaidi kwa gharama nafuu. Kutokana na uwekezaji katika mashine na teknolojia hizo, kiwanda kina uwezo wa kuzalisha mita milioni 60 kwa mwaka ilikinganishwa na uzalishaji wa mita milioni 16 kwa mwaka kabla ya kubinafsishwa, pia ufanisi wa kuhudumia wateja umeongezeka

ambapo mteja anaweza kupata bidhaa aliyoagiza katika kipindi cha wiki moja. Aidha, kiwanda kimeweza kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 1,800 ikilinganishwa na ajira 1,260 kabla ya kubinafsishwa. Kiwanda pia kimeweza kutoa ajira zisizo za moja kwa moja zipatazo 10,000. Baadhi ya changamoto za kiwanda ni: uingizaji haramu wa nguo kutoka nje ambazo hazilipiwi kodi na hivyo kuuzwa kwa bei ndogo na kupelekea ushindani usio wa haki katika soko; na kukatika mara kwa mara kwa nishati ya umeme bila taarifa na hivyo kuathiri uzalishaji na mara nyingine uharibifu wa mitambo.

- (iii) **Kiwanda cha Sukari Kilombero – Morogoro:** Kiwanda kilianzishwa mwaka 1962 na kubinafsishwa mwaka 1998 ambapo Serikali ya Tanzania inamiliki asilimia 25 ya hisa zote na makampuni ya Illovo Sugar asilimia 55 na ED&F Man asilimia 20. Kiwanda kimewekeza zaidi ya shilingi bilioni 6.5 kwenye miradi ya huduma za jamii. Kiwanda kinatoa ajira za moja kwa moja 5,000 na kuwawezesha wananchi kati ya 80,000 na 100,000 katika bonde la mto Kilombero kujiajiri katika kilimo cha miwa. Vile vile, kiwanda kimewekeza katika kilimo cha miwa katika eneo lenye jumla ya hekta 10,000. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto ya wafanyabiashara wasio waaminifu huingiza sukari ya viwandani ikiwa na msamaha wa kodi na kuiza kwa matumizi ya kawaida hivyo kuathiri soko la sukari nchini.
- (iv) **Kiwanda cha Karatasi Mufindi (Mufindi Paper Mills) – Iringa:** Kiwanda kilibinafsishwa mwaka 2004 kwa Rai Group kutoka Kenya kwa asilimia 100. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 60,000 za karatasi kwa mwaka na kinatumia miti aina ya *pine eucalyptus* na *black wattle* inayovunwa katika mashamba ya Serikali ya Sao Hills yaliyopo wilayani Mufindi. Kiwanda kinazalisha karatasi aina ya kaki (brown papers) zenyu uzito tofauti kulingana na mahitaji ya soko la ndani na nje. Mwekezaji alifanya ukarabati mkubwa wa mashine ya karatasi na kusimika mashine mpya za kisasa na mitambo ya kufua umeme wa MW 10 ambapo uzalishaji uliongezeka hadi tani 120,000 kwa mwaka. Vile vile, kiwanda kimetoa ajira 746 za kudumu na ajira 595 za muda. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto kubwa tatu zikiwemo: magogo ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa karatasi; na mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji na vijiji vinavyozunguka mashamba ya miti.
- (v) **Kiwanda cha Saruji – Mbeya:** Kiwanda cha saruji Mbeya kilijengwa mwaka 1977 na kuanza uzalishaji mwaka 1983 chini ya usimamizi wa

Serikali. Katika mwaka 1999 kiwanda kilibinafsishwa na kuuzwa kwa kampuni ya CDC ambapo pia kiliuzwa tena mwaka 2001 kwa kampuni ya Lafarge ya Switzerland ambapo Serikali inamiliki hisa asilimia 25, Lafarge asilimia 65 na NSSF asilimia 10. Hivi sasa kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 350,000 kwa mwaka ambapo kati ya hizo asilimia 90 zinauzwa katika soko la ndani na asilimia 10 zinauzwa kwa nchi jirani za Zambia, Malawi, Burundi na DRC. Kiwanda kimetoa ajira za moja kwa moja 340 na ajira 685 zitokanazo na wakandarasi wa kiwanda. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto za: miundombinu mibovu ya usafirishaji hususan reli ya TAZARA; miundombinu hafifu ya kuhudumia mizigo katika bandari ya Kasanga; umeme usio wa uhakika kutoka TANESCO ambao unakatika zaidi ya mara moja kwa siku; na bei kubwa ya makaa ya mawe kutoka TANCOAL.

- (vi) **Kiwanda cha nguo – Mwanza (Mwatex):** Kiwanda cha Mwatex 2001 Limited chenye eneo la hekta 44.5 kilibinafsishwa mwaka 2001. Uzalishaji ulianza rasmi mwaka 2003, hususan kwa kanga, kitenge, kikoi, shuka, sare za shule, mikoba na mafuta ya chakula. Changamoto kubwa ya kiwanda ni tatizo la nishati ya umeme, maji, upatikanaji wa pamba safi na watumishi wenye ujuzi. Katika mwaka 2012 kiwanda kilipunguza idadi ya wafanyakazi kutoka 1,235 hadi 340 ikiwa ni sehemu ya kupuguza gharama za uzalishaji.

(g) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Mtukula Kagera: Kituo cha Mtukula kinaunganisha huduma za Mkongo wa Taifa wa mawasiliano na nchi ya Uganda. Hadi sasa kampuni ya Roke Telecom ya Uganda imeshaunganishwa na bado kuna mahitaji makubwa ya matumizi ya mkongo huo kutoka nchi jirani. Changamoto kubwa ni usimamizi na utunzaji wa miundombinu ya kituo cha mawasiliano kwa kuwa kituo kipo mbali na ofisi za TTCL zilizopo Bukoba mjini na upatikanaji wa fedha.

(h) Kilimo

Skimu ya Umwagiliaji – Idodi (Iringa): Mradi unamifereji ya umwagiliaji 2, mfereji wa Idodi (mita 1,950) na Mbuyuni (mita 1,850). Mradi huu unalenga kuongeza tija ya uzalishaji wa mpunga na utatumika kumwagilia eneo la hekta 600. Ujenzi wa mradi unaendelea na umefikia zaidi ya asilimia 85 ambapo sehemu kubwa ya ujenzi iliyokamilika ni njia kuu. Hata hivyo, usanifu wa skimu ya umwagiliaji wa eneo la mradi haujazingatia njia za michepuko na hivyo kuashiria upotevu mwingu wa maji wakati wa umwagiliaji. **Maghala ya COWABAMA – Iringa:** Ujenzi wa ghalalililopo kijiji cha Ibangamoyo kata ya

Ulanda upo katika hatua za mwisho kukamilika. Hata hivyo, ujenzi wa ghala una changamoto ya nyufa kabla kuanza kutumika. Aidha, ghala ni ndogo na hivyo kutotosheleza mahitaji ya wakulima wa eneo la mradi.

(i) Mifugo

